# Nipashe

Alhamisi Septemba 12, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580021

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Wanawake wanne, mwanamume wafungwa jela kwa ukahaba

UKURASA 3


ama
AFYA NA MAZINGIRA
RC ACHARUKA 'HAIKUBALIKI'...
NUSU WAKAZI MKOA SHINYANGA HAWANA VYOO; MBADALA PORINI, MIFUKO, PAGALA

UKURASA 13

# Vitambulisho vinane uchaguzi wa mitaa

Zimo mpaka leseni za udereva, kadi za bima ya afya, pasi za kusafiria, wapinzani watoa neno...*Uk. 2*



Mbunge wa Bumbuli, January Makamba (kushoto), akiteta jambo na Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Daktari bingwa ataja ugonjwa unaomkabili Askofu Ruwa'ichi

UKURASA 2


### YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**ZIARA YA JPM KITUONI NEEMA KWA ASKARI**

RAIS John Magufuli amefanya ziara ya kushtukiza katika Kituo cha Polisi cha Selander Bridge, jijini Dar es Salaam na kuagiza kupandishwa cheo askari wa kike kutoka koplo hadi kuwa sajenti...

**UKURASA WA 4**

**SIMULIZI MWANASIASA ALIVYOKATWA MAPANGA**

ALIYEKUWA mgombea ubunge katika Jimbo la Vunjo, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Innocent Melek, ameelezea watu wasiojulikana walivyomteka na kumcharanga mapanga sehemu mbalimbali mwilini...

**UKURASA WA 7**

**MIRADI 88 ISIYOTOA MAJI KUKARABATIWA**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amesema imebainika kuna miradi 88 nchini ambayo haitoi maji kutokana na uzembe na ubadhirifu uliofanywa na baadhi ya watendaji na makandarasi wa ovyo.


## Mali za Dangote hatarini kunadiwa

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA: TUTAIVAA ZESCO KIVINGINE UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Ziara ya JPM kituo cha Selander neema kwa askari

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amefanya ziara ya kushtukiza katika Kituo cha Polisi cha Selander Bridge, jijini Dar es Salaam na kuagiza kupandishwa cheo askari wa kike kutoka koplo hadi kuwa sajenti.

Hatua hiyo ya Rais Magufuli ilifuatia ziara hiyo aliyoifanya juzi na askari huyo aliyekuwa akitoa huduma katika kituo hicho, WP 4160 Beatrice Mlanzi, kuonyesha utimilifu katika kazi yake.

Rais Magufuli amekuwa akifanya ziara za kushtukiza mara kwa mara tangu alipoingia madarakani, Novemba 5, 2015, siku moja baada ya kuapishwa alifanya ziara kama hiyo kwa kutembelea Hazina Kuu.

Novemba 9, 2015 Rais Magufuli alifanya ziara ya kushtukiza katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ili kujionea hali ya utoaji huduma, mojawapo ya wagonjwa aliowatembelea na kumjulia hali alikuwa ni Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Helen Kijo Bisimba, ambaye kwa sasa amestaafu.

Mei 28, 2017, akiambatana na mke wake Janeth alifanya ziara nyingine ya kushtukiza MNH na kuwajulia hali wagonjwa waliolazwa katika wodi ya Mwaisela.

Miongoni mwa wagonjwa aliowatembelea ni Mzee Francis Maige (Ngosha) kwa sasa ni marehemu, ambaye ndiye aliyechora nembo ya taifa.

Oktoba 5, 2016 alitembelea Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere (JNIA) sehemu ya kukagulia mizigo na abiria wa uwanja huo eneo la Terminal I na kubaini baadhi ya mashine za ukaguzi zilikuwa hazifanyi kazi.

Pia Mei 15, 2018 alitembelea Bandari ya Dar es Salaam katika matangi ya kuhifadhi mafuta ya kula baada ya kushushwa melini, alikagua uingizwaji na ugawaji wa ulipaji wa ushuru.

Vile vile, Juni 24, mwaka huu alifanya ziara ya kushtukiza katika mradi wa ujenzi wa daraja la baharini eneo la Selander linalokatiza baharini kwa kuunganisha maeneo ya Coco Beach, kujionea maendeleo ya ujenzi wa daraja hilo.

**Miongoni mwa wagonjwa aliowatembelea ni Mzee Francis Maige (Ngosha) kwa sasa ni marehemu, ambaye ndiye aliyechora nembo ya taifa.**

# Vitambulisho 8 kutumika uchaguzi wa serikali mitaa

**Na Gwamaka Alipipi**

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) imetoa mwongozo wa uchaguzi wa viongozi wa vijiji, vitongoji na mitaa unataja vitambulisho vitakavyotumika kupigia kura katika uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Umetaja vitambulisho hivyo kuwa ni cha mpigakura, cha kazi, hati ya kusafiria, kadi ya bima ya afya, cha shule au chuo, mifuko ya hifadhi ya jamii, leseni ya udereva na cha taifa.

Pia mwongozo huo umeelezea sifa za mgombea, mpiga kura, siku ya kuanza kampeni pamoja na utaratibu wa kupiga kura.

Mwongozo vile vile umeelezea namna ya uandikishwaji wa wapigakura, uteuzi wa wasimamizi wa vituo, namna ya kuchukua na kurejesha fomu za kugombea utakavyofanyika.

Mwongozo huo uliowekwa kwenye tovuti ya wizara hiyo na kusainiwa na waziri mwenye dhamana, Selemani Jafo, pia uleleza utaratibu wa kuwasilisha taarifa na matokeo ya uchaguzi huo.

**Sifa za mpigakura**

Umeeleza kuwa mpigakura katika uchaguzi huo ni lazima awe raia wa Tanzania, umri wa miaka 18 au zaidi, mkazi wa kijiji au kitongoji au mtaa ambao uchaguzi unafanyika, hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na serikali au Bodi ya Utabibu, amejiandikisha kupiga kura katika kitongoji au mtaa au kijiji husika.

**Sifa za mgombea**

Mwongozo pia ulitaja sifa za mgombea ni pamoja na; "raia wa Tanzania, ana umri wa miaka 21 au zaidi, anaweza kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza, ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi, ni mwanachama wa chama cha siasa na amedhaminiwa na chama hicho, hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi, hana ugonjwa wa akili.

Pia ilieleza kuwa fomu za kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi huo zitatolewa kuanzia Oktoba 29 hadi Novemba 4, 2019 kuanzia saa 1: 30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

**Kampeni za uchaguzi**

Ulieleza kuwa kampeni zitaanza Novemba 17 hadi 23, vyama vya siasa vyenye wagombea vinaweza kuwateua wanachama wake kuendesha kampeni kwa niaba ya wagombea wa vyama vyao.

Ulieleza kuwa kampeni za uchaguzi zitaanza saa mbili asubuhi na zitamalizika saa 12 jioni ya kila siku ya kampeni.

"Vyombo vya ulinzi na usalama hususani Jeshi la Polisi, Mgambo wenye sare au ofisa yeyote anayesimamia ulinzi, vitatumika katika kuhakikisha kunakuwapo na usalama na utulivu katika mikutano ya kampeni na wakati wa uchaguzi. Vikundi vya ulinzi vya

INAENDELEA UK 8



Rais John Magufuli akimjulia hali Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thadeus Ruwa'ichi anayepatiwa matibabu katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: IKULU**

# Ugonjwa unaomsumbua Askofu Ruwa'ichi watajwa

**Na Mary Geofrey**

DAKTARI Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu wa Tasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Prof. Joseph Kahamba, ameeleza ugonjwa uliompata Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thadeus Ruwa'ichi hadi kusababisha kufanyiwa upasuaji.

Askofu Mkuu Ruwa'ichi alifanyiwa upasuaji usiku wa manane kuamkia juzi katika Taasisi ya Mifupa (MOI).

Alieleza ugonjwa uliompata ni damu kuvimbia kwenye ubongo ambao kitaalam unaitwa 'Chronic Subdural Haematoma'.

Alisema alifanyiwa upasuaji mkubwa wa ubongo na kuondoa uvimbe huo, uliochukua saa nne chini ya madaktari bingwa watatu, na kwamba hali yake inaendelea vizuri wakati akiendelea kuwa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU).

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Prof. Kahamba, alisema hali ya kiongozi huyo wa Kanisa, inaendelea vizuri na anaweza kuzungumza.

"Tunashukuru hali ya mgonjwa inaendelea vizuri tofauti na kabla hatujamfanyia upasuaji. Alifika hapa juzi usiku (Septemba 9) akitokea Hospitali ya Rufani ya KCMC mkoani Kilimanjaro, na tulipewa taarifa na wenzetu kuwa walimfanyia upasuaji, lakini hali yake ikaendelea kuwa mbaya," Prof. Kahamba alisema.

Alisema walipomfikisha MOI walianza kumfanyia vipimo na kubaini tatizo hilo na walianza kumfanyia upasuaji saa 7:00 usiku hadi saa 10:00 alfajiri.

"Leo (jana) hali yake inaendelea vizuri, ameshaamka anajitambua na anafuata maelekezo anayopewa, na anazungumza taratibu baadhi ya maneno," Prof. Kahamba alisema.

Aidha, alisema wameunda timu ya wataalamu saba ambao wanamfanyia uchunguzi wa kina katika kuhakikisha afya yake inarejea kama ilivyokuwa awali.

Aliwataja wataalamu ambao wanamfanyia uchunguzi ni madaktari bingwa watatu wa magonjwa ya ubongo, dawa za usingizi na magonjwa ya ndani.

Alisema wataamu wanne ni wa masuala ya chakula na lishe, mazoezi tiba, watalaamu wa uchunguzi na wauguzi.

"Wataalam hawa saba wa uchunguzi watafanya kazi hiyo ili kuhakikisha afya ya Askofu inarejea katika hali yake ya kawaida na huwa tunafanya kwa wagonjwa wengine wanaopata tatizo kama hili," Prof. Kahamba alisema.

SABABU ZA UGONJWA

Prof. Kahamba alisema sababu za ugojwa huo hazijulikani, lakini ni tatizo linalotokea mara kwa mara kwa watu wengi.

Alitaja baadhi ya mambo yanayosababisha ni kuumia kichwani, shinikizo kubwa la

INAENDELEA UK 8

HABARI KITAIFA



Mwonekana wa sehemu ya ujenzi unaoendelea wa barabara za mpishano (Ubungo Interchange), katika eneo la mataa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanawake wanne, mwanamume jela kwa ukahaba

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WANAWAKE wanne na mwanamume mmoja anayedaiwa kuwa mteja wao wamehukumiwa kifungo cha miezi sita jela na Mahakama ya Mwanzo ya Makole, jijini hapa, ikiwamo kuchapwa viboko vitatu wakati wa kuingia.

Hukumu hiyo inafuatia Jeshi la polisi mkoani hapa

kuendelea na msako wa kuwakamata wanawake wanaodaiwa kuwa makahaba katika maeneo mbalimbali wanayofanya kazi ya kuuza miili yao kama sehemu ya kujiingizia kipato.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, Kamanda wa Polisi, Gilles Muroto, alisema msako wa kinadada wanaojiuza miili yao unaendelea na kuwataka wanaofanya biashara hiyo kuacha mara moja.

Kamanda Muroto aliwataja waliokamatwa na kuhukumiwa kifungo hicho bila

faini na mmoja aliyehukumiwa

miezi mitatu baada ya kukiri kosa, kuwa ni Erica George (24), Lucy Saibati (28), Joyce Ndekwa (30),

Hawa Said (28), na Grolia Michael (29).

Kamanda Muroto alisema, Septemba 8, mwaka huu katika Mtaa wa Uhindini, Kata ya Viwandani, watu hao walikamatwa kwa kosa la kufanya ukahaba kinyume na kifungu cha sheria namba 176 (a), f na g cha kanuni ya adhabu ya sura ya 16.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Mtaa wa Tofiki Uhindini, Alnoor Kassam, alisema baada ya kupata malalamiko kutoka kwa wakazi wa eneo hilo, alikwenda kutoa taarifa polisi.

Alisema baadhi ya nyumba za kulala wageni ambazo zilikuwa zitumika kufanya biashara ya ngono, wamiliki walizifunga kwa hiyari yao wenyewe.

Wakati huohuo, katika tukio lingine Kituo cha Polisi Kati, kilivamiwa na kundi la waendesha pikipiki (boda boda) zaidi ya 70 na kufanya fujo wakitaka kumtoa mahabusu, Bazil Mjungu, ili

wampige baada ya kusababisha ajali ya gari na kumgonga bodaboda.

Waendesha bodaboda hao walitawanywa kwa Amani, lakini walikaidi amri ikiwamo kufunga barabara na kuzingira kituo cha polisi jambo lililosababisha askari kuwatawanya kwa kufyatua risasi hewani.

Watu 20 wamekamatwa kuhusiana na tukio hilo na kufunguliwa mashtaka.

Alisema baada ya upelelezi kukamilika walifikishwa mahakamani kusomewa mashtaka na kupatikana na hatia, walihuhukumiwa kifungo cha miezi sita jela kila mmoja bila faini.

## Mali za Dangote, Bakhresa hatarini kupigwa mnada

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania(TRA) imetangaza kuzipiga mnada mali za kampuni zitakazoshindwa kulipa ushuru wa forodha wa mizigo yao ndani ya siku 30.

Miongoni mwa mali hizo ni za kampuni za wafanyabiashara mabilionea Aliko Dangote na Salim Bakhresa.

Miongoni mwa kampuni kubwa zilizoorodheshwa na TRA kutakiwa kulipa ushuru wa forodha ni Kampuni ya Saruji ya Dangote.

Agizo hilo lilitolewa na TRA, kupitia tangazo lililotelewa kwenye gazeti la Serikali la Daily News la Septemba 9, mwaka huu lenye kurasa 28, toleo namba ISSN 0856-3812 No 12,458.

Katika tangazo hilo, limeitaja kampuni ya saruji ya Dangote mara 19 ikitaja pia mali zilizozuiwa kuwa ni pamoja na vifaa vya kimaabara na mashine za kuzalisha saruji.

Mbali na Dangote, kampuni nyingine zilizotajwa ni pamoja na Salim Bakhresa inayotakiwa kulipia bidhaa zake kama matangi, maboksi na bidhaa nyingine.

Tangazo hilo liliwaorodhesha wadaiwa wengine ni pamoja na Hospitali ya Kairuki, kampuni za simu Airtel na Vodacom, pamoja na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Kampuni nyingine ni Benki ya CRDB, kampuni inayojenga mradi wa Reli ya Kisasa ya Standard Gauge (SGR), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto( Unicef).

Kupitia tangazo hilo, wadaiwa hao wametakiwa kulipa kodi ya forodha ndani ya siku hizo na wasipofanya hivyo, mali zao zitapigwa mnada.

## Hakimu mahakamani kwa tuhuma za rushwa

**Na Mariam Magili, TUDARCo**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) imemfikisha mahakamani Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Magomeni, Omary Abdalah (40), kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 703,000.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kuomba fedha hizo ili kumsaidia mlalamikaji kwenye kesi ya mirathi iliyofunguliwa mahakamani hapo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Takukuru wilayani Kinondoni, Theresia Mnjagira, hakimu huyo amefikishwa mahakamani hapo pamoja na mfanyabiashara George Barongo (37), mkazi wa Kibamba kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 498,000.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kuomba na kupokea rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007.

"Ilidaiwa kuwa mnamo Februari 12, 2017, Abdalah alimtaka mtoa taarifa ampe kiasi cha Sh. milioni moja ili aweze kumsadia kwenye kesi ya mirathi iliyokuwa mbele yake kinyume na utaratibu," alisema.

Vile vile, alisema mlalamikaji alitoa taarifa Takukuru Wilaya ya Kinondoni, Machi mosi, 2017, uchunguzi ulifanyika na kubaini kuwa tuhuma hizo ni za kweli na shauri hilo kuanza upya.

"Uchunguzi dhidi ya tuhuma zote mbili umekamilika na watuhumiwa wamefikishwa katika Mahakama ya Kinondoni kujibu tuhuma zinazowakabili," alibainisha. Katika hatua nyingine, Takukuru imemfikisha mahakamani Katibu wa Kamati ya Upimaji ya viwanja katika Mtaa wa Nyakasangwe, Nerbert Malevu (33) kwa kuomba rushwa ya Sh. milioni 2.5 na kupokea Sh. 500,000.

Ilidaiwa kuwa mnamo Agosti 14, mwaka huu, mtuhumiwa huyo alimtaka mtoa taarifa ampatie fedha hizo ili aweze kumpatia sehemu ya kiwanja ambacho kilikuwa cha mtoa taarifa kabla ya upimaji na kwa madai kuwa sehemu ya kiwanja hicho kiligaiwa mtu mwingine baada ya upimaji.

hakielimu

**EXCITING CAREER OPPORTUNITY**

HakiElimu works to realise equity, quality, human rights and democracy in education by facilitating communities to transform schools and influence policy making; stimulating imaginative public dialogue and organising for change; conducting critical research; policy analysis and advocacy and collaborating with partners to advance common interests and social justice. The overall goal of HakiElimu is: An open, just and democratic society with quality education for all.

HakiElimu is looking for enthusiastic, motivated and result oriented candidates to fill in the following position of **Programme Officer Gender and Violence Against Children**

A. Job Purpose:

To mobilise citizens and the school communities around programmes districts to transform their schools to be gender sensitive, and VAC-free areas in order to promote effective learning for children, especially girls.

B. Specific Responsibilities:

i) Responsible for the designing and promoting of gender and VAC messages in communities and programme schools
ii) Responsible for establishing and facilitating Gender & VAC clubs to promote girls' education and child protection in programme schools
iii) Facilitate Friends to promote gender and child protection in schools
iv) Other duties as required

C. Personal Specifications, Skills and Experience

i) Recommended a minimum of 5 years' experience of work in related positions
ii) First degree in development or other social sciences related courses, Masters degree is an added advantage
iii) Experience in NGO programme cycle management, and field related interventions
iv) A very good understanding of national and international development issues, especially within the education sector and its development programmes.
v) Strong commitment, knowledge and expertise in issues of gender equality
vi) A proven programme officer who can drive and execute her duties to the best level. Able to articulate issues, and communicate clearly to diverse audiences, including partners, staff, Friends of Education, community members, and government officials

How to apply:

The full Job Description and Application form can be downloaded from: www.hakielimu.or.tz.
All applications should be sent to jobs@hakielimu.or.tz by **23rd September 2019.**

NOTE: HakiElimu is committed to keeping children safe from abuse and harm.

Candidates applying for this post will therefore be subject to child safeguarding recruitment procedures and checks. We also promote equal opportunities and strive to be fully representational to all groups.

HakiElimu thus actively encourages qualified women and people with disability to apply.

***Only short-listed candidates will be contacted.***

21545302

# Mitihani darasa la saba yafanyika kwa amani

**Na Romana Mallya**

ULINZI na usalama katika mitihani ya kumaliza darasa la saba unaoendelea leo nchini baada ya kuanza jana, umeimarishwa kila kona, huku wananchi wakizuiwa kupita kwenye maeneo ya shule ambazo wanafunzi wanafanya mtihani huo.

Nipashe jana ilishuhudia katika shule mbalimbali jijini Dar es Salaam ulinzi ukiwa umeimarishwa, huku baadhi yake mageti ya kuingilia kwenye shule yakiwa yamefungwa na polisi wakizuia watu wasiohusika kuingia.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mapambano, Yonas Silvester, aliliambia gazeti hili kuwa hali ni nzuri na mitihani ilifika kwa muda uliopangwa.

"Watoto walifika kwa wakati na sasa wako mapumziko wanasubiria kuingia katika mtihani wao wa pili kwa siku hii ya leo. Mitihani hii itafanyika muda wa siku mbili kwa maana kesho (leo) watamaliza," alisema.

"Watoto walifika kwa wakati na sasa wako mapumziko wanasubiria kuingia katika mtihani wao wa pili kwa siku hii ya leo. Mitihani hii itafanyika muda wa siku mbili kwa maana kesho (leo) watamaliza," alisema.

Gazeti hili lilipita katika Shule za Msingi Shekilango, Kijitonyama, Kisiwani, Kilimani, Tandale Magharibi, Muhalitani, Msisiri ambapo kote hali ilikuwa shwari na wanafunzi hadi saa 8:30 mchana walikuwa kwenye vyumba vya mitihani.

Katika Shule za Msingi Mchangani na Kisiwani, geti la kuingilia lilikuwa limefungwa kuhakikisha watoto wanafanya mitihani yao bila mwingiliano wa watu ndani ya shule hizo.

Kwenye shule ambazo hazina uzio, gazeti hili lilishuhudia askari polisi wakiwarudisha walikotoka wananchi waliokuwa wakitaka kukatisha ndani ya shule hiyo.

Juzi, Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania (Necta) lilitangaza kuanza kufanyika kwa mitihani hiyo kwa muda wa siku mbili kuanzia jana na leo huku likitaja idadi ya watahiniwa waliosajiliwa kuufanya kuwa ni 947,221.

Katibu Mtendaji wa Necta, Dk. Charles Msonde, alisema kuwa kati ya watahiniwa 947,221 waliosajiliwa mwaka huu kufanya mtihani huo ni wa kutoka katika shule 17,051 Tanzania Bara.

Alisema kati yao wavulana ni 451,235 sawa na asilimia 47.64 na wasichana ni 495,986 sawa na asilimia 52.36.

Alisema watahiniwa 902,262 watafanya mtihani huo kwa lugha ya Kiswahili na watahiniwa 44,959 watafanya kwa lugha ya Kiingereza ambayo wamekuwa wakiitumia katika kujifunzia.

"Watahiniwa wenye mahitaji maalum ni 2,678 ambapo kati yao 81 ni wasioona, 780 wenye uoni hafifu, 628 wenye ulemavu wa kusikia, 325 ni wenye ulemavu wa akili na 864 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwilini," alisema.



Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa (katikati), akimtua ndoo ya maji Waziri wa Wizara ya Ushirikiano na Maendeleo Serikali ya Ujerumani, Vera Rosendahl (kulia), baada ya kuzindua rasmi mradi wa maji wenye gharama ya Sh. milioni 331 katika Kijiji cha Ng'ong'ona, jijini Dodoma jana, uliofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la Maendeleo la GIZ. Kushoto ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Simulizi mwanasiasa alivyokatwa mapanga

**Na Mary Geofrey**

MWANASIASA na aliyekuwa mgombea Ubunge katika Jimbo la Vunjo, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Innocent Melek, ameelezea watu wasiojulikana walivyomteka na kumcharanga mapanga sehemu mbalimbali mwilini.

Akizungumza na Nipashe juzi, Maleck alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Jumatano ya wiki iliyopita alipokuwa akirejea nyumbani kwake Goba, jijini Dar es Salaam.

"Ilikuwa saa 5:00 usiku nikiwa narudi nyumbani kwangu nilikutana na watu wawili walikuwa wamesimama barabarani maeneo ya Kizumbi umbali wa mita 300 kufika nyumbani kwangu. Mmoja alikuwa akijifanya kutengeneza pikipiki yake na mmoja akawa ananisimamisha kuniomba msaada," Maleck alisimulia.

Alisema aliamua kusimama kwa ajili ya kuwasaidia kwa sababu aliamini ni vijana wa mtaani kwake na baada ya kusimamisha gari alifungua kioo na ghafla alipigwa na taulo usoni iliyomfanya apoteze fahamu.

"Ghafla baada ya kusimama nilishtukia nimepigwa na kitambaa usoni kama taulo na nikapoteza fahamu kuanzia pale. Inaonyesha baada ya kupoteza fahamu waliendesha gari hadi maeneo ya Kawe," alisema Maleck.

Alisema majira ya saa 7:00 usiku alianza kupata fahamu na kujikuta yuko maeneo ambayo baadaye alielezwa ilikuwa Kawe.

"Inaonyesha walinichukua na gari hadi Kawe ambako waliienda kupekua gari langu kwa muda na mrefu (kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa ndugu walioliona) na kunicharanga mapanga manane, manne maeneo ya kichwani na matatu mgongoni. walinikata na mshipa wa ugoko na maeneo ya miguuni nina majeraha ya kuburuzwa kwenye lami," alisema.

Meleck aliendelea kusimulia kuwa watu hao walipomaliza kumjeruhi waliamini amepoteza maisha ndipo wakamwegesha kwenye gari kichwa kikiwa kwenye siti ya gari lake na miguu ikining'inia kwenye lami.

Alisema akiwa eneo hilo walikuja madereva wa pikipiki ambao walimwona na kwenda kumpatia msaada kisha walimbeba na kumpeleka kituo cha Polisi Kawe kwa ajili ya kupatiwa PF3 (fomu ya matibabu).

"Wakati wote nilikuwa nasikia kila kinachoendelea hadi nilipofikisha Polisi Kawe nilipoteza tena fahamu hadi nilipokwenda kuzinduka nikiwa Hospitali ya Kairuki wakati nikiendelea kupatiwa matibabu," alisema.

Mali alizoibiwa

Malek ambaye pia ni mfanyabiashara, alisema watu hao walichukua fedha taslimu Sh. milioni 11, komputa mpakato moja yenye mambo yake binafsi na masuala ya kisiasa na waliacha moja ya kazini, walichukua simu zake za mkononi mbili na flash mbili.

Alisema watu hao pia walichukua miundo miwili ya nje ya kutunza kumbukumbu za komputa zake.

"Kinachoshangaza zaidi waliacha vitu vyangu vyote vya ofisini ikiwamo EFD mashine jambo linalonipa shaka hasa kwa kitendo cha kunijeruhi vibaya kiasi hiki ilihali walikuwa wana uwezo wa kuchukua kila kitu na kuniacha salama," alisema.

Kwa mujibu wa Meleck, jambo hilo analihusisha na tukio lililowahi kutokea mwaka 2015 wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu. Katika tukio hilo, alisema watu wasiojulikana walivamia nyumba yake, Marangu mkoani Kilimanjaro na kumkata kwa mapanga hadi kumwua baba yake mdogo.

Alisema wakati tukio hilo linatokea hakuwapo nyumbani ndiyo maana hakupata madhara na kwamba hana historia ya kugombana na mtu yoyote.

VYOMBO VYA DOLA

Maleck alisema kutokana na tukio hilo, kuripotiwa Polisi juzi usiku alirudi kituo cha Kawe na kwa ajili kupatiwa hati ya kurejesha namba zake za simu zilizokuwa zimeibwa.

Alisema hajaitwa kuhojiwa wala kuulizwa chochote lakini anaamini wanaendelea na uchunguzi katika kuhakikisha wanawatia hatiani waliohusika katika tukio hilo.

Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Mussa Taibu, alipoulizwa na Nipashe kuhusu tukio hilo, alisema alikuwa safarini wiki iliyopita na bado hajapokea taarifa hiyo. Aliahidi kulifuatilia na kutoa taarifa rasmi kwa mwandishi.



## NGO zakumbushwa kuweka ripoti za fedha wazi

**Joseph Mwendapole**

SERIKALI imerudia kuzikumbusha asasi zisizo za kiserikali kuweka wazi mapato na matumizi yao pamoja na shughuli zote wanazofanya na imezionya zile zinazoendesha mambo yake kwa kificho.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mratibu wa Kisekta kutoka Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Andrew Komba, wakati wa uzinduzi wa wiki ya asasi za kiraia iliyoandaliwa na Foundation for Civil Society (FCS).

Alisema nia ya serikali ni kutaka kujua kama shughuli za asasi hizo zinaenda sambamba na mipango yake ili kuondoa ukinzani unaoweza kutokea kwenye utekelezaji wa baadhi ya mambo baina ya pande hizo mbili.

"Tukisema asasi za kiraia ziweke wazi mambo yake haimaanishi upande wa fedha tu bali hata shughuli nzima mnazofanya kwasababu serikali inaweza ikawa inafanya hivi huku nyinyi mnafanya kinyume chake," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Francis Kiwanga, alisema zaidi ya asasi za kiraia 15 chini ya uratibu wa FCS zinaandaa wiki ya asasi za kiraia itakayofanyika mwezi Oktoba, mkoani Dodoma.

Kiwanga alisema wiki ya azaki inalenga kuunda na kuimarisha muundo endelevu wa kuleta ukuaji unaochagizwa na uhusishwaji makini wa asasi za kiraia katika azma ya kuiletea Tanzania maendeleo.

Kiwanga alisema katika wiki ya asasi za kiraia kutakuwa na matukio mbalimbali yenye lengo la kupaza sauti masuala mbalimbali na kuwezesha utambuzi wa maeneo ya ushirikiano.

Alisema kutakuwa na ufunguzi wa maonyesho ya kazi za asasi mbalimbali yanayolenga kuwahusisha zaidi wananchi wa kawaida, warsha za pamoja na zile za wenye mahitaji maalum na utoaji wa tuzo.

Alisema mwaka jana tukio kama hilo lilifanyika mkoani Dodoma na kaulimbiu yake ilikuwa juhudi za ujenzi wa viwanda Tanzania, watu, sera na utekelezaji na lilileta pamoja washiriki zaidi ya 600 kutoka asasi 400.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe (wa pili kushoto), na viongozi wengine wa chama hicho, wakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, kusikiliza kesi inayowakabili. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shahidi adai Chadema walitoa kauli kuhamasisha maandamano

**Na Hellen Mwango**

MRAKIBU Msaidizi wa Polisi (ASP), Bernard Nyambari (42), amedai mahakamani katika kesi ya uchochezi dhidi ya viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kwamba walitumia maneno na kauli za kuhamasisha maandamano siku ya kufunga kampeni za uchaguzi mdogo katika viwanja vya Buibui, Jimbo la Kinondoni.

Kadhalika, alidai kuwa chanzo cha maandamano hayo yaliyofanywa na viongozi wa chama hicho, uchunguzi ulibaini baada ya kuwahoji watu mbalimbali wakiwamo Mwenyekiti Taifa wa Chadema Freeman Mbowe na wenzake wanane, ndiyo chanzo cha maandamano hayo.

ASP Nyambari ambaye ni shahidi wa nane, alitoa madai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba anayesikiliza kesi hiyo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na jopo la Mawakili wa Serikali Wakuu, Dk. Zainabu Mango, Faraja Nchimbi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Salim Msemo.

Akiongozwa na Dk. Mango, shahidi alidai kuwa akiwa kama mchunguzi wa kesi hiyo, baada ya kuhoji watu mbalimbali siku ya tukio alibaini kwamba viongozi wa Chadema walitoa maneno na kauli za kuhamasisha wanachama wao kuandamana.

Alidai shahidi huyo aliwatambua viongozi wanne wa chama hicho waliokuwa katika maandamano, wafuasi wa chama hicho, Februari 16, mwaka jana eneo la Mkwajuni.

Aliwatambua mahakamani viongozi hao kuwa ni Mbowe, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji, Mbunge wa Jimbo la Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Jimbo la Kibamba, John Mnyika.

Shahidi huyo ambaye kwa sasa ni, Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya ya Kipolisi Mbagala, Benard Nyambari, alieleza hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati akitoa ushahidi wake kwenye kesi hiyo.

Alidai kuwa, eneo la Hananasifu majira ya saa 12:30 jioni pamoja na askari wengine wawili, walisikia kelele zikiashiria vurugu zikitokea eneo la Barabara ya Kawawa.

Alidai akiwa hapo, alipigiwa simu na aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, SSP Kungu Malulu, akimwelekeza aelekee barabara ya Kawawa kuna maandamano.

Alidai walipofika eneo hilo, walikuta kundi kubwa la watu wakiandamana barabarani eneo la Mkwajuni wakielekea kituo cha mabasi ya mwendokasi, wakionekana na jazba na kubishana na polisi waliowataka watawanyike huku waandamanaji hao wakiwajibu polisi kuwa hawaondoki wakitaka wawauwe.

Kadhalika alidai kuwa akiwa kama askari mpelelezi, baada ya maandamano hayo alibaini kuwa chanzo cha maandamano kilikuwa ni hotuba mbalimbali zilizotolewa na viongozi wa Chadema katika mkutano wa kufunga Kampeni za Mgombea Ubunge Jimbo la Kinondoni, zilizofanyikà viwanja vya Buibui, Mwananyamala.

Mbali ya Mbowe, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Katibu Mkuu Taifa, Dk. Vincent Mashinji, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji na Mbunge wa Kawe Halima Mdee.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
10/09/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 11/9/2019 kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEASE CONSTRUCTION & INVESTMENT (EA) LTD** itasafirisha Mzigo kutoka **SUMBAWANGA** kuelekea **KABANGA** kupitia **MPANDA.** Magari yenye namba za usajili **T 550 BES / 474 BCJ**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **16** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.8** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.9** |

3. Njia itakayotumika: **SUMBAWANGA** hadi **KABANGA kupitia MPANDA.** Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115414602



DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUNUNUA VITU MBALIMBALI AMBAVYO SI VYAKULA (NFI's).

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 11.09.2019 HADI TAREHE 24.09.2019 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255627423991 au barua pepe jean.kabore@drc.ngo**

ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 26.09.2019 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA rfq.tza@drc.ngo AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**

215413002

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni upuuzi wanavijiji kumsujudia chatu

**HUKO** mkoani Geita katika Kijiji cha Kasara, wananchi kutoka maeneo mbalimbali wamekusanyika kushuhudia na kumletea zawadi na sadaka chatu aliyeonekana kwa wiki kadhaa.

Taarifa za kumpelekea mnyama huyo zawadi na kumfurahia kwa madai kuwa ameleta neema zimesambaa kwenye mitandao ya kijamii,simu na TV mitandao.

Suala hili linadhihirisha kuwa jamii zetu bado ziko nyuma kwenye utambuzi na uelewa wa masuala ya msingi.

Wananchi wengi wanaendelea kuonyesha kuwa wana uelewa mdogo na hasa pale wanapothubutu kusema kuwa nyoka anawaletea neema.

Kwa mfano wa kumsujudia chatu huyo ambaye huenda amemeza mnyama mkubwa au amejeruhiwa ndiyo maana anashindwa kutembea, inadhihirisha kuwa wananchi wengi wako gizani. Kumpelekea nyoka huyo zawadi na sadaka, kama mbuzi, kafara,mtama na vyakula kwa imani kuwa ujio wake unatoa majibu ya matatizo yao ni kurudi nyuma zaidi kimaendeleo katika zama hizi za sayansi na teknolojia.

Katika madai yao viongozi wanadai nyoka huyo atakapokula sadaka zao ni jibu la matatizo yao kwani wanasumbuliwa na presha, VVU na Ukimwi, kisukari na saratani lakini pia kuna changamoto za upungufu wa mvua na mavuno mashambani.

Kuamini kuwa nyoka ni jawabu la matatizo makubwa ya njaa, maradhi na umasikini ni matokeo ya athari za kukosa elimu, kuwa na uelewa mdogo na ujinga miongoni mwa Watanzania wengi. Ujinga unasababisha wana vijiji kuendelea kuathirika katika maisha yao ya kila siku na hata kutishia hatma ya maisha yao ya siku za usoni.

Kuwa na elimu duni ndiko kunakowafanya watu kuamini kuwa nyoka analeta neema na tiba kwa matatizo yao. Imani hizo ndizo zinazoathiri uchumi, afya na namna ya kufikiria.

Tunaona kuwa kuamini kuwa nyoka analeta neema ni matokeo ya kuwa na uelewa duni pamoja na kujikita zaidi katika masuala ya kiutamaduni badala ya kujishughulisha na mambo muhimu kama kujifunza na kuujua ukweli.

Ni wazi kuwa kama jamii zingekuwa zinajishughulisha kusoma machapisho kama magazeti, vipeperushi na kupata taarifa za muhimu kwa ajili ya maisha watu wangefahamu kuwa magonjwa kama VVU, Ukimwi, saratani na kisukari chanzo chake ni kipi. Aidha, watu wangeweza kufahamu kuwa mabadiliko ya tabia nchi yanayotokea zama hizi ni chanzo cha uhaba wa mvua, mavuno duni na pia wangefahamu jinsi uharibifu wa mazingira unavyohusika na kujua namna ya kuachana na mambo hayo.

Wakati mwingine jamii hizi zinathibitisha kuwa Watanzania tunatoa umuhimu mdogo kwenye elimu badala yake tunaamini zaidi utamaduni na mila.

Tukumbuke ukosefu wa elimu unachangia kurithisha vizazi ujinga , maisha duni na matokeo yake ni kuwa na mwendelezo wa umaskini usiokoma na imani za kishirikina zinazodumaza maendeleo. Uelewa mdogo na imani zisizokuwa na manufaa wakati mwingine umesababisha kutokujiamini na mara nyingi kuishi maisha ya kusaka mchawi na kuhisi kuwa kuna watu wanawaloga wenzao.

Yote hayo yamesababisha mauaji ya albino, wazee na hata watu wanaosingiziwa uchawi katika maeneo mbalimbali.

Imani hizo ndizo zinazoziingiza jamii kwenye fikra kuwa viungo vya wanadamu wenzao ni dawa ya utajiri na yote hayo ni ujinga ambao unakwamisha jamii kuwa na utaalamu na kufanya mambo yanayochangia kujiletea maendeleo.

Tunawaomba wataalamu wa wanyama pori na mabingwa wa nyoka kuwaeleza wananchi ukweli kuhusu nyoka huyo na chanzo cha kulala kwa siku kadhaa katika kijiji cha Kasara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Watumishi wasiobadilika zama hii itawatumbua, jiangalieni

Na Raphael Kibiriti

**KUNA** mabadiliko makubwa ya kiutendaji katika uga wa kiserikali tangu awamu ya tano iingie madarakani mwaka 2015.

Mabadiliko haya yanatoa nuru ya kufikia malengo mbalimbali ya kitaifa yanayolenga ustawi wa Watanzania.

Serikali imelenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025, na ndiyo maana ya jitihada zinazoendelea kufanyika kwa njia tofauti sasa ili kuifikia dhamira hiyo.

Katika hili Muungwana anatoa mifano ya miradi mikubwa ya kimkakati kama ule wa uzalishaji umeme wa Stigler's Gorge, wenye thamani ya takribani Sh. trilioni 6.5 hadi kukamilika kwake.

Mradi huo unatarajiwa kuzalisha megawati 2,115 za umeme na hivyo kumaliza mahitaji ya nishati hiyo kwa wananchi, pia kuchagiza Tanzania inayoongozwa na uchumi wa viwanda.

Kuna mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma, ambao tayari umeshaanza kwa vipande viwili.

Kipande cha kwanza kinaanzia Dar es Salaam hadi Morogoro, chenye umbali wa kilometa 300 na kinatarajiwa kukamilika Novemba mwaka huu.

Kipande cha pili kinatoka Morogoro hadi Makutopora (Manyoni), chenye umbali wa kilometa 422, kikitarajiwa kukamilika Februari 2021.

Serikali pia imenunua ndege nane mpya, hatua iliyoliwezesha Shirika letu la ndege la ATCL, kufufuka na hivyo kuchagiza sekta ya usafiri wa anga na ya utalii kwa ujumla, hatimaye kuongeza pato la taifa.

Na miradi mingi inayolenga kutoa huduma kwa wananchi ikiwamo ya afya, miundombinu ya barabara, taasisi za kielimu, shule, maji na mingine, yote ni katika dhamira ya kustawisha maisha yao.

Kimsingi miradi mingi inaendelea vizuri, kwa wakati, kwa muda uliopangwa na kwa sehemu kubwa hilo limewezekana kutokana na mabadiliko ya kimtazamo kwa watendaji na watumishi wa serikali, taasisi na mashirika ya umma.

Mabadiliko ambayo yamewezeshwa na msimamo madhubuti wa viongozi wakuu kwa maana ya Rais John Magufuli na wasaidizi wake Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Msimamo unaowasisitiza walio katika ofisi za umma kuwa watumishi wa wananchi badala ya watawala.

Matunda yake ni haya ambayo pamoja na mengine, yamewezesha makusanyo ya serikali kupanda hadi kufikia zaidi ya Sh. trilioni moja kwa mwezi, hivyo kuijengea serikali uwezo wa kugharimia miradi yake mbalimbali ya kimkakati.

Pamoja na kwamba wizara, idara, taasisi na mashirika mengi ya umma yameweza kuendana na kasi ya zama hizi za serikali ya awamu ya tano, bado kuna mashirika, idara na taasisi ambazo zinaangushwa na baadhi ya watumishi wake katika suala zima la kuhudumia wananchi.

Ninatolea mfano wa Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) na Shirika la Umeme nchini (Tanesco) ambapo baadhi ya wafanyakazi wake wanayaangusha kwa kutoendana na kasi ya awamu hii.

Kwa mfano Muungwana alimshangaa msoma mita mmoja wa Dawasa, Ofisi ya Boko aliyemtishia kumkatia maji mteja mmoja eneo la Tegeta iwapo hatanunua kifaa kinachoruhusu maji kupita kwenye mita ya maji.

Kifaa hicho cha kwenye mita, mali ya Dawasa kilikuwa kimelegea na hivyo kuruhusu maji mengi yavuje, kitu ambacho ni hasara kwa Dawasa.

Kwamba badala ya Dawasa kukirudishia kifaa hicho, msoma mita akamtaka mteja akinunue halafu atoe taarifa kwa Dawasa ili itume mafundi wa kukifunga!

Wakati msoma mita huyo akimtishia kumfungia maji mteja asiyedaiwa bili na Dawasa, bomba ambalo linapeleka maji eneo hilo lina miezi miwili sasa linavuja na taarifa imeshatolewa kwa Dawasa.

Aidha, msoma mita huyo amekuwa akiliona bomba hilo linavuja mara kwa mara, kwa sababu anapita huko.

Sasa badala ya kuchukua hatua ya kuziba bomba hilo linalopeleka maji kwa wateja wengi, anamgeukia mteja mmoja afanye kazi ambayo kimsingi ni ya Dawasa.

Zipo taarifa pia kwa baadhi ya ofisi za Tanesco kutochukua hatua mapema pale zinapojulishwa uwapo wa nguzo za umeme zilizoanguka, zilizooza ama nyaya za umeme wa Tanesco zilizokatika hadi matatizo yakiwamo ya maafa yanapotokea.

Ni rai basi ya Muungwana kwa idara, taasisi na mashirika ya umma ambayo bado baadhi ya watumishi wake wanafanya kazi kwa mapuuza, kuachana na aina hiyo ya utendaji.

Anaasa hivyo kwa sababu zama hizi ni za kitabu kingine na kwamba serikali na Watanzania kwa ujumla wanataka kukimbia katika dhima nzima ya maendeleo badala ya kutembea.

Na hiyo ni katika dhamira ya kuifanya Tanzania nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025.

## Tembo wabomoa nyumba 39, wala mahindi gunia 30

**Na Mwandishi wetu**

NYUMBA 39 katika vijiji vya Longaloniga, Matale na Mwasengela wilayani Meatu, mkoani Simiyu, zimebomolewa na tembo waliovamia makazi waKitafuta chakula na kula magunia 30 ya mahindi.

Katika tukio hilo, mwananchi mmoja alidondokewa na ukuta akiwa amelala na kujeruhiwa.

Tembo hao waliokuwa kwenye kundi kubwa, walibomoa mahindi yaliyokuwa yamehifadhiwa kwenye maghala.

Tukio hilo lilitokea juzi usiku wakati wananchi hao wakiwa wamelala, na yamekuwa ni matukio ya mara kwa mara na kusababisha madhara ambayo yamewaacha bila chakula.

"Baada ya kubomoa nyumba walikula mahindi, walishiba na kuondoka," alisema mmoja wa waathirika wa tukio hilo.

Mkuu wa wilaya, Dk. Joseph Chilonganya, alisema watafanya utaratibu wa kuwapa kifuta machozi, huku akitaka ambao wana makazi kuwahifadhi walioharibiwa nyumba zao.

"Tunafanya hivi ili ambao vyakula vyao vimeliwa waweze kuwa na chakula na kuendelea na maisha," alisema.

Kamishna wa Taasisi ya Wanyamapori Tanzania (Tawa), Dk. James Wakibara, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kutokusogelea maeneo yaliyohifadhiwa.

"Wanaosogelea sana mipaka ya maeneo yaliyohifadhiwa wanakuwa katika maisha hatarishi, wananchi wanasumbuka unalala ndani hujui kama tembo atakuja au la...vijiji na maeneo yote ambayo yako karibu na hifadhi ni vyema yakapangwa kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi.

Aidha, Tawa alitoa gunia mbili za mahindi kwa kila kaya iliyoathiriwa na tukio hilo.

# Korti kusikiliza rufani ya ardhi dhidi ya Bakwata

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Ardhi, imepanga kuanza kusikiliza rufani iliyofunguliwa na Alphonse Kakweche na Mgainamba Kihakwi dhidi ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata) , wanaidaiwa kujimilikisha hekari 40 zilizopo kijiji cha Chita, Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro.

Kesi hiyo ilitajwa juzi katika mahakama hiyo, ikiyoketi chini ya Jaji Modesta Opiyo.

Kwa mujibu wa hati ya rufani hiyo, walalamikiwa wanadai kuwa wamekata rufani kupinga uamuzi uliotolewa na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kilombero/Ulanga wa Februari 8,2017.

Walalamikiwa wanaomba Mahakama Kuu kufuta uamuzi wa kunyang'anywa umiliki wa hekari hizo ufutwe na warejeshewe ardhi yao.

Kwa mujibu wa hati ya rufani hiyo, walalamikiwa wamewasilisha hoja sita.

Moja, Baraza hilo lilikosea kisheria kusikiliza shauri hilo kwa kuwa halina mamlaka.

Mbili na tatu, lilikosea kimantiki kutoa hukumu kwa kuwapendelea Bakwata bila kuzingatia maoni ya wazee wa Baraza, sheria kama inavyotakiwa kisheria.

Nne, Baraza lilikosea kisheria kwa kutokujali ushahidi wa walalamikaji unaothibitisha umiliki wa ardhi inayobishaniwa.

Tano, Baraza hilo pia lilikosea kwa kuamua ardhi inayobishaniwa ilikuwa imetelekezwa na walalamikaji.

Hoja ya sita kwamba, Baraza hilo lilikosea kuamua kuwa Bakwata ilifuata sheria zinazotakiwa kabla ya kupata ardhi hiyo.

Hata hivyo, mlalamikiwa akijibu hoja za walalamikaji, alidai kuwa baraza hilo lilikuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.

Bakwata imedai kuwa baraza hilo lilikuwa sahihi kwa sababu alifuata taratibu zote za kisheria zinazotakiwa kupata ardhi hiyo.

Mlalamikiwa anaomba mahakama kutupilia mbali rufani hiyo kwa kuwa haina mashiko kisheria.

Rufani hiyo itasikilizwa Desemba 2, mwaka huu mbele ya Jaji Opiyo.



Shughuli za ufagiaji barabarani, kinamama wakiwa sehemu ya waajiriwa. **PICHA: MTANDAO.**

# Miradi 88 isiyotoa maji kukarabatiwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amesema imebainika kuna miradi 88 nchini ambayo haitoi maji kutokana na uzembe na ubadhirifu uliofanywa na baadhi ya watendaji na makandarasi wa ovyo.

Kufuatia hali hiyo, serikali imejipanga kuhakikisha miradi yote ya maji ambayo imejengwa kuanzia mwaka 2010 hadi 2012 ambayo haitoi maji inakarabatiwa ili iweze kutoa maji.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizindua mradi wa maji Ng'ong'ona uliofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa kutumia fedha za walipa kodi wa nchi hiyo.

"Kuna miradi 88 nchini ikiwamo miradi ya vijiji 10 ilianza 2010, na mingine fedha zilikuwapo, lakini yamefanyika mambo ya ovyo sana wameenda mahali hakuna maji wakachimba visima," alisema na kuongeza kwamba miradi hiyo iliwekewa mabomba mabovu.

"Ukienda Mwanza, Mbeya, Mtwara kila unakokwenda kuna tatizo hili limesababishwa na watendaji tuliowaamini na makandarasi wa ovyo, hili halikubaliki na hata Mwenyezi Mungu hatakuelewa," alisema.

Alisema wameanza kuishughulikia miradi hiyo kupitia mamlaka za maji kwa gharama nafuu.

Alisisitiza serikali itahakikisha miradi yote ambayo haitoi maji itakarabatiwa kwa gharama nafuu na hawatachukua makandarasi matapeli na wa ovyo.

"Tunatayarisha wataalamu wa mamlaka za maji mbalimbali nchini kufanya kazi ya kukarabati miradi hii na wanafanya kazi vizuri na kwa bei nafuu," alisema.

Alisisitiza kila kilichoahidiwa kinatekelezwa, na kwamba kuna miradi inajengwa nchini ili kutatua tatizo la maji na kutekeleza ahadi zilizoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ya mwaka 2015-2020.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanalinda miradi na miundombinu na wasikubali watu kukata mabomba kwa kuwa haikubaliki.

Akizungumzia kuhusu mradi huo, Prof. Mbarawa alisema ulianza mwaka 2013 ni wa muda mrefu na ulitokana na uzembe, uhuni na ubadhirifu mkubwa ulifanywa na watendaji na mkandarasi aliyekuwa amepatiwa kazi hiyo.

"Hii ni aibu na fedheha haikutokea bure, wakati huo fedha ilikuwapo na hii imetokea kwasababu kuna watu walifanya uzembe, kuanzia mhandisi wa halmashauri hata wakurugenzi waliokuwapo hadi Wizara ya Maji," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Dodoma (DUWASA), Mhandisi David Pallangyo, alisema mradi huo uliotekelezwa kwa gharama ya Sh. milioni 331 awali ulikuwa unatekelezwa chini ya programu ya miradi ya vijiji 10 ukiwa unasimamiwa na halmashauri ya jiji.

"Novemba 2017 Duwasa ilipokea mradi huo kutoka manispaa kutokana na mkandarasi aliyekuwapo kutotekeleza majukumu yake ipasavyo, hivyo tuliwasiliana na wadau wa maendeleo ambao ni Shirika la Maendeleo ya Ujerumani GIZ wakatekeleza mradi huo," alisema mkurugenzi.

Alisema utekelezaji rasmi ulianza Januari 2019 na ulipangwa kukamilika mei 2019, lakini kutokana na baadhi ya changamoto ikiwamo kuchelewa kwa kutolewa kwa msamaha wa kodi VAT ulikamilika Julai 2019.

Mwakilishi wa GIZ, Vera Rosendahi, alisema serikali imefadhili mradi huo kwa kushirikiana na Duwasa na kuahidi kuendelea kushirikiana ili kutekeleza miradi mingine.

# Vitambulisho 8 kutumika uchaguzi wa serikali mitaa

INATOKA UK 2

jadi au binafsi au vya mashabiki wa vyama vya siasa havitaruhusiwa kutumika kwenye maeneo ya mikutano ya kampeni au ya uchaguzi," ulieleza mwongozo huo.

**Utaratibu wa kupiga kura**

Mwongozo huo pia ulieleza kuwa kabla ya msimamizi wa kituo hajampatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, atajiridhisha kama jina lake limeorodheshwa katika orodha ya wapigakura na baada ya kuridhika atamtaka mpigakura ajitambulishe kwa kutumia kitambulisho.

"Vitambulisho vitakavyotumika ni cha mpigakura, cha kazi, hati ya kusafiria, kadi ya bima ya afya, cha shule au chuo, cha mifuko ya hifadhi ya jamii, leseni ya udereva na cha taifa," ulieleza mwongozo huo.

**Sifa za wasimamizi wasaidizi**

Mwongozo huo ulieleza kuwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi na maofisa wengine watakaoteuliwa watakuwa na sifa zifuatazo: "Wasiwe na dhamana au uongozi katika chama chochote cha siasa, wawe ni watumishi katika utumishi wa umma, wawe na uadilifu."

Ulieleza kuwa uteuzi wa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi utafanyika kuanzia Septemba 16 hadi 22, 2019.

**Pingamizi la wagombea**

Mwongozo huo ulieleza kuwa msimamizi wa uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi za uongozi katika ngazi zote kuanzia Novemba 5, 2019.

"Mgombea au mtu aliyeomba kuteuliwa anaweza kuweka pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea na litawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi kuanzia Novemba 5 hadi 6 , 2019 na msimamizi atasikiliza na kutoa uamuzi kuanzia Novemba 5 hadi 7.

**Utaratibu wa kutangaza matokeo**

Ulieleza kuwa matokeo uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa, yatatangazwa katika ngazi ya mtaa husika, na kwamba matokeo yatajazwa kwenye fomu maalum ambayo itasainiwa na wagombea au wawakilishi wao pamoja na msimamizi wa kituo na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

Ulieleza kuwa nakala za matokeo ya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Vijiji kutoka katika vitongoji zitawasilishwa Ofisi ya Serikali ya Kijiji kwa ajili ya kujumlishwa na kutangazwa washindi.

**Maoni ya vyama**

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mawasiliano ya Umma wa Chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu, alisema walishirikishwa kwenye maoni katika mkutano uliofanyika Aprili, mjini Dodoma na uchambuzi ulifanyika kuhusu kanuni na waliunga mkono vitambulisho hivyo kutumika katika uchaguzi huo.

"Tulipendekeza kuwapo na wigo kwa wapigakura, hivyo hatuna wasiwasi na vitambulisho hivyo kutumika," alisema Shaibu.

Alisema kwenye kikao hicho walitoa maoni yao kwenye maeneo yenye shida na yasiyokuwa na shida.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tumaini Makene, alisema kikubwa vitambulisho hivyo vilenge kumsaidia mwananchi mwenye haki ya kupiga kura.Alisema Chadema inachohitaji ni kuona mwananchi mwenye sifa anaruhusiwa kupiga kura kwa mujibu wa kanuni.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, alisema: "Tunafuata sheria, kanuni na taratibu zinazotumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa."



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Mbunge wa Viti Maalum, Salma Kikwete, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Ugonjwa unaomsumbua Askofu Ruwa'ichi watajwa

INATOKA UK 2

damu linaloweza kusababisha mishipa ya damu kupasuka na matumizi ya dawa zikiwamo za kupunguza maumivu ambazo zinasababisha damu kulainishwa na kuvimbia kichwnai.

Prof. Kahamba alisema mgonjwa asipopata matibabu ya haraka, damu inaendelea kuvunja kichwani, ujazo wa damu unapoendelea kuzidi unapeleka mgandamizo kwenye ubongo na athari kuongezeka na kusababisha mgonjwa kupoteza maisha.

"Mgonjwa wa namna hii inapaswa kupata matibabu ya haraka iwezekanavyo na mtu akishagundua ugonjwa huu unapaswa kupata matibabu ya dharura," Prof. Kahamba alisema.

Alitaja dalili za kuwa na ugonjwa huo ni kulingana na tatizo lipo upande upi wa kichwa, lakini dalili za kawaida ni kuumwa kichwa, kizunguzungu, dalili za kutapika na kukosa nguvu kwenye mkono na mguu mmoja.

VIONGOZI WAMIMINIKA KUMUONA

Alisema idadi ya viongozi wa Serikali wakitanguliwa na Rais John Magufuli walienda kumjulia hali juzi na Mwakilishi wa Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Fancis, Askofu Mkuu, Marek Solczynski ambaye aliendа jana.

Wengine ni Askofu Mkuu mstaafu, Muadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Eusebius Nzigilwa na maaskofu wengine.

Alisema watawashauri ndugu zake watengeneze kitabu cha watu wanaoenda kumuona ili waandike salamu zao za kumtamkia afya njema na kumuombea badala ya kuingia wodini.

Alisema kwa sababu yupo ICU anapaswa kupata muda mzuri wa kupumzika kwa ajili ya kuangalia afya yake na kwamba wanazuia kumuona kwa sababu ya kuhofia maambukizi ya magonjwa.

Prof. Kahamba aliwataka waumini wa kanisa hilo kuwa watulivu na kumuacha kiongozi huyo apumzike wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

Ni siku 27 tangu Askofu Ruwaichi ashike wadhifa huo, baada ya Muadhama Polycarp Kardinali Pengo kung'atuka Agosti 15, mwaka huu baada ya Papa Francisko kuridhia ombi lake.

## Faida 6 Tanzania kuridhia itifaki ya Sadc wagunduzi wa mbegu

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imelieleza Bunge faida sita za Tanzania karidhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Akiwasilisha azimio la kuridhia itifaki hiyo, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema itifaki iliandaliwa na nchi wanachama wa Sadc Mei 2017 kwa lengo la kutoa mwongozo kuhusu kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea ili kuhamasisha ugunduzi wa mbegu mpya katika ukanda wa Sadc.

Hasunga alizitaja faida sita za kuridhia itifaki hiyo kuwa ni pamoja na kuweka mfumo wa kulinda hakimiliki za wagunduzi wa mbegu unaokubalika na umetekelezwa katika nchi za Sadc na hivyo kuimarisha uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine.

Alisema hakimiliki itakayotolewa chini ya itifaki ya Sadc itatambulika ndani ya nchi zote wanachama wa jumuiya hiyo, hivyo kuchochea uwekezaji katika nyanya mpya za utafiti na ugunduzi wa mbegu mpya na sekta binafsi.

Alisema faida ya tatu ya kuridhia itifaki hiyo ni kupanga wigo na kurahisisha biashara ya mbegu na hivyo kuhamasisha ushindani katika tasnia ya mbegu.

Hasunga alisema faida ya nne ni kuhamasisha na kutoa fursa za utafiti unalenga kuongeza uzalishaji wa mbegu mpya na hatimaye kuwezesha wakulima kupata mbegu bora.

"Karidhia itifaki hii pia kutakuwa na matokeo chanya ya kuongeza upatikanaji wa mbegu bora, kupunguza gharama za usafirishaji na hivyo kupunguza bei ya mbegu kwa mkulima."

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuhusu azimio hilo, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, alisema kuna haja serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya vituo vya utafiti ili kuwezesha watafiti kufanya utafiti kwa fedha za ndani badala ya kutegemea fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Pia alisema ni muhimu sera na sheria zinazohusiana na mbegu zikafanyiwa marekebisho ili kuendana na maudhui ya itifaki hii.

Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Kilimo, Pascal Haonga (Chadema), alisema ni wazi Tanzania imechelewa katika kuhakikisha mbegu za asili zinaboreshwa na zinapata hakimiliki ili kuhakikisha wakulima wanapata mazao mengi na bora.

## HABARI KITAIFA

# Wakulima watakiwa kulima miti kibiashara

**Na Mwandishi Wetu,** MUFINDI

WAKULIMA wilayani Mufindi mkoani Iringa, wametakiwa kutumia mbinu mpya za kilimo cha miti ambacho kimekuwa na faida kubwa katika siku za hivi karibuni kwa mikoa ya Ndanda za Juu Kusini.

Kilimo hiki ambacho ni cha kibiashara zaidi kimeanza kuonyesha mwanga wa kuwatoa wakulima kutoka kwenye dimbwi la umaskini.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, mmoja wa wakulima wa miti katika kijiji cha Nzinyi wilayani Mufindi, mkoani Iringa, Aidan Fitavangu, alibainisha kuwa kilimo hicho kimeanza kuwaletea matunda.

Fitavangu ambaye ameanza kunufaika na kilimo cha miti, alisema hivi sasa wakulima wengi wanatumia mbinu za kisasa za kilimo kama vile kupanda kwa nafasi, jambo ambalo ni muhimu katika kupata mavuno bora.

"Ukitumia mbegu bora na kufuata kanuni zote za kilimo bora kama vile kupalilia, kutumia mbolea na kuacha nafasi matokeo yake ni makubwa na kwa muda mfupi," alisema.

Kwa mujibu wa wataalamu, mti uliopandwa kwa kuacha nafasi inayotakiwa una uwezo mkubwa zaidi wa kutoa mazao bora katika kipindi fulani.

Mwakilishi kutoka Jambe Agro, Steven Sallu, alisema kanuni bora ni pamoja na kuandaa shamba, kupanda kwa wakati, kuacha nafasi na kuchenga ni muhimu sana katika kupata mazao bora.

Alisema kampuni yake inasimamia miradi kadhaa ya uelimishaji ili kuwawezesha wakulima wa miti kuwa na ujuzi unaotakiwa.

"Pamoja na kusambaza mbegu za miti zilizoboreshwa, pia tunatoa elimu kwa wakulima kuwawezesha kupata mazao bora," alisema.

Aliongeza lengo la kampuni yake ni kuwawezesha wakulima wa miti ili kutumia fursa katika sekta ya misitu kiendelevu.

Matumizi ya mbegu bora ni muhimu kwa kuongeza ukuaji na ubora wa shamba. Ili kupata ubora huo, mkulima anahitaji eneo la kuzalisha mbegu bora na eneo la kitalu cha miche.

# Diwani aliyepiga trafiki jela mwaka na siku mbili

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya Mkoa wa Kigoma imemhukumu Diwani wa Mwanga Kaskazini (ACT-Wazalendo) Clayton Revocatus (34) maarufu 'Baba Revo', kutumikia kifungo cha mwaka mmoja na siku mbili jela kwa kosa la kumshambulia askari polisi wa kikosi cha usalama barabarani.

Askari huyo ni mwenye namba F8350 PC Msafiri kwa kumpiga ngumi na makofi sehemu mbalimbali za mwili wake.

Hukumu hiyo imetolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kenneth Mtembei, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo bila ya kuacha shaka yoyote.

Hakimu Mtembei alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa viongozi wengine wenye tabia ya kuwapiga watumishi wa serikali kama yake.

Alisema upande wa utetezi wa mshtakiwa ulikuwa umekata rufani kupinga adhabu ya miezi mitano iliyotolewa na Mahakama ya Mwanzo Mwandiga dhidi ya mshtakiwa huyo.

**Upande wa utetezi wa mshtakiwa huyo ulipeleka mahakamani sababu tano za rufani yao sababu ya kwanza ni kesi haikuthibitika kwa kiwango cha sheria.**

Alisema upande wa utetezi wa mshtakiwa huyo ulipeleka mahakamani sababu tano za rufani yao sababu ya kwanza ni kesi haikuthibitika kwa kiwango cha sheria, sababu ya pili Mahakama ya Mwanzo Mwandiga ilikosea kuwaruhusu washauri wa mahakama hiyo kuuliza maswali ya kuwachanganya mashahidi.

Sababu ya tatu ni Mahakama ya Mwandiga ilikuwa inamwingilia mshtakiwa wakati wa utetezi wake na sababu ya nne ni mahakama hiyo, haikuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na sababu ya tano ni Mahakama ya Mwandiga ilishindwa kuandika maoni ya washauri wa mahakama hiyo katika mwenendo mzima wa kesi hiyo.

Aidha, alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Masanja akijibu hoja tano za rufani hiyo kuwa sababu zao zote tano walizozitoa hazina ukweli.

Hakimu Mtembei alisema alipitia pande zote pamoja na hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Mwanzo Mwandiga na kubaini kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwandiga alifanya kazi yake vizuri na mahakama inaona maamuzi yaliyotolewa na mahakama ni sahihi.

Alisema: "Mahakama hii inatengua maamuzi ya Mahakama ya Mwanzo Mwandiga kwa sababu kitendo alichokifanya mshtakiwa wakati akijua yeye ni kiongozi wa wananchi ni kibaya sana kwa jamii kumshambulia askari polisi akiwa kwenye majukumu yake, siyo kitendo kizuri kwa kiongozi yeyote yule hata kwa mwananchi wa kawaida."

Alisema kutoa adhabu siyo kumkomoa bali ni kutengua maamuzi ya Mahakama ya Mwanzo Mwandiga ya adhabu ya miezi mitano jela na kwenda mwaka mmoja na siku mbili jela ili iwe fundisho kwake na kwa viongozi wengine wenye tabia ya kuwapiga watumishi wa serikali na akimaliza kifungo hicho atakuwa raia mwema kwa jamii.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Precision Air, Patrick Mwanri (kushoto), akikabidhi mfano wa tiketi ya ndege kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutangaza ushirikiano katika kuboresha huduma kwa watu wenye ulemavu, ambapo imetoa tiketi 120 kwa CCBRT, kwa ajili ya matumizi ya shughuli zake za kuwezesha kliniki za matibabu katika mikoa mbalimbali. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri aipa tano NEMC kuharakisha utoaji vyeti

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe amelipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kuharakisha kutoka vyeti vya tathmini ya athari kwa mazingira (TAM).

Waziri Kamwelwe aliliambia kwamba baada ya Rais John Magufuli kuiagiza NEMC kutoa vibali ya tathmini ya athari kwa mazingira ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo, yamekuwapo mabadiliko makubwa katika utendaji wa baraza hilo.

Akijibu swali la Mbunge wa Lulindi, Jerome Bwanausi (CCM), waziri alisema baada ya agizo la Rais, iko kila sababu ya "kusifu mabadiliko makubwa ambayo yamefanywa na baraza katika kutoa vibali hivyo kwa miradi ya maendeleo. NEMC wanatoa vibali hivyo haraka sana."

Alisema miradi ya maendeleo ambayo imenufaika na utoaji wa vibali hivyo kwa haraka ni pamoja na miradi katika kata za Sindano, Lupajo, Lipumburu, Mchauru na Mapili zilizo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Kamwelwe alisema hivi sasa miradi ya maendeleo, hasa ya ujenzi, inatekelezwa kwa wakati baada ya serikali kuziondoa changamoto zilizokuwa zikikwamisha utekelezaji, ikiwamo kuchelewa kutolewa kwa vibali vya tathmini ya athari kwa mazingira.

"Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa hivi sasa NEMC inatoa vibali vya tathmini ya athari kwa mazingira kwa haraka sana.

"Tangu Rais alipoitaka NEMC kuacha kuchelewesha vibali hivyo alipotembelea Kiwanda cha Makaa ya Mawe kule Mtwara, hivi sasa tatizo la ucheleweshaji wa vibali umebaki kuwa ni historia, vibali vyote vinatolewa kwa wakati," alisemaWaziri Kamwelwe.

# Mahakama 30 kujengwa mwaka huu

BUNGE limeelezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/20, serikali imepanga kujenga mahakama za wilaya 30 nchini.


Hayo yalielezwa jana bungeni na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Gimbi Masaba.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali itajenga lini Mahakama ya Wilaya ya Itilima ili kuwaondolea usumbufu unaowakumba wananchi hali inayowalazimu kwenda wilaya ya jirani ya Bariadi kupata huduma hiyo.

Akijibu, Dk. Mahiga alikiri wilaya hiyo kutokuwa na mahakama na wananchi kulazimika kusafiri umbali mrefu wa takriban kilomita 37 kufuata huduma hiyo Wilaya ya Bariadi.

**Hii inatokana na ukweli kwamba Mahakama ya Tanzania bado inakabiliwa na uhaba wa majengo katika maeneo mengi.**

Alisema changamoto hiyo ipo katika wilaya 27 nchini ambazo zinapata huduma katika wilaya za jirani.




"Hii inatokana na ukweli kwamba Mahakama ya Tanzania bado inakabiliwa na uhaba wa majengo katika maeneo mengi," alisema.

Hata hivyo, alisema mahakama imejiwekea mkakati wa kutatua changamoto hiyo hatua kwa hatua kupitia mpango wake wa miaka mitano wa kujenga na kukarabati majengo ya mahakama kwa ngazi zote.

Alifafanua kuwa Mahakama ya Wilaya ya Itilima ipo kwenye mpango wa kujengwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na mahakama nyingine.

Alitaja wilaya zingine zilizopo kwenye mpango huo ni Busega, Kyerwa, Missenyi, Gairo, Mbogwe, Songwe, Rufiji, Kibiti, Nyang'wale, Mvomero, Uyui, Kaliua, Uvinza, Buhigwe, Kakonko, Chamwino, Chemba, Ikungi, Mkalama, Butiama, Rorya, Ubungo, Malinyi, Tanganyika, Mkinga, Kilosa, Kilombero, Hanang na Nkasi.

Aidha, aliishukuru Wilaya ya Itilima kwa kutoa kiwanja kwa ajili ya kujenga mahakama hiyo chenye ukubwa wa mita za mraba 5,028 na kutoa wito kwa wilaya zingine hizo kutoa viwanja ili kujengewa majengo ya mahakama.



Ndugu wa Wabunge Seif Gulamali wa Manonga na Hussein Amar wa Nyang'wale, wakitambulishwa Bungeni, jijini Dodoma jana. Seif na Amar ni wajukuu wa Mzee Gulamali aliyefariki dunia mwaka 1990 na kuacha watoto 30 na wajukuu zaidi ya 60. **PICHA: SANULA ATHANAS**

# Sababu za mimba shuleni kupungua

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema sheria na makatazo mbalimbali juu ya wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa shuleni yamesaidia kupunguza mimba kwa wanafunzi kwenye maeneo mengi nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, William Ole Nasha, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Aida Khenan.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji matamko na makatazo hayo yamesaidia kwa kiasi gani kuhusu wanafunzi wanaopata ujauzito.

Akijibu, Ole Nasha alisema matamko na makatazo kuhusu wanafunzi wanaopata ujauzito yanatokana na Kanuni za Elimu za mwaka 2002, Kanuni namba 4 ya Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, Sura ya 353 inayobainisha makosa ya wanafunzi shuleni.

Aidha, alisema yanazingatia marekebisho ya Sheria ya Elimu Namba 25 ya Mwaka 1978 yaliyofanyika mwaka 2016, ambapo mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kumpa mimba mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari atahukumiwa kifungo cha miaka 30 jela.

"Sheria pia inatoa adhabu kwa mtu yeyote anayesaidia mhalifu aliyempa mwanafunzi mimba," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema sheria na makatazo hayo yamesaidia pia jamii kujua adhabu kwa mtu yeyote atakayempa mimba mwanafunzi, ambapo baadhi ya kesi zimefunguliwa na wahusika wamehukumiwa kifungo.

"Jamii pia imeweza kufahamu adhabu ambazo zinatolewa na kukiuka matakwa ya sheria na pia elimu, matamko na sheria vimepunguza mimba za wanafunzi kwenye maeneo mengi nchini na jamii kufahamu umuhimu wa kulinda hadhi na usalama wa mtoto wa kike," alisema.

Ole Nasha alisema serikali imeweka mikakati ya kupunguza changamoto kwa watoto wa kike ikiwa ni pamoja na kujenga mabweni na hosteli katika maeneo ambayo wanafunzi wanalazimika kutembea umbali mrefu.

"Aidha, serikali imeweka mpango wa kusaidia wasichana wanaoacha shule kwa sababu mbalimbali ili waweze kuendelea na masomo, "alisema.

Alieleza kuwa mpango huo ni kutoa elimu kupitia vituo vya elimu nje ya mfumo rasmi vinavyoratibiwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), pamoja na vyuo vya maendeleo ya wananchi (FDC).

Alitoa wito kwa jamii kuendelea kutoa ushirikiano wa kuwalinda watoto wa kike na kuhakikisha kuwa taarifa zinatolewa kwa mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa mtu yeyote anayesababisha mtoto wa kike kukosa elimu anaadhibiwa.

# Mfumo wa pamoja ununuzi wa viuatilifu

SERIKALI imesema inakusudia kuandaa mfumo wa pamoja wa kununua viuatilifu kwa ajili ya matumizi ya msimu wa 2020/21 ikiwamo vya ugonjwa wa fungi unaolikabili zao la korosho.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Uzini (CCM), Salum Mwinyi Rehani, ambaye alisema dawa ya Sulphur ndiyo dawa ya udhibiti wa fungue (fungi) kwenye mazao ya korosho na mazao mengine.

Alisema serikali imeunda mfumo wa kuagiza dawa hiyo ya kupuliza kwa njia bubu na mwaka jana baadhi ya wakulima waliathirika kwa kuchelewa na kupata dawa feki.

"Je, ni lini serikali itakuwa tayari kuleta dawa mbadala ambazo ni rahisi zaidi? Je, ni lini serikali itakaa na vyama vya msingi ili kupanga ratiba ya kuagiza na kuleta dawa na kupiga na pia kuzuia dawa za msimu uliopita," alisema.

Akijibu maswali hayo, Mgumba alisema viuatilifu vingine kwa ugonjwa huo ni pamoja na triadimenol, hexaconazole, tebuconazole, penconazole, pecoxystrobin na proquinazid vitanunuliwa.

Hata hivyo, alisema serikali itaendelea kuhimiza matumizi ya dawa kwa kuwa kiuatilifu hicho hakihitaji ujuzi mwingi wakati wa kukitumia shambani kwa kuwa kimezoeleka.

"Vile vile hakiingii ndani ya mmea na hivyo kufanya korosho inayozalishwa kuwa na sifa ya kilimo hai," alisema.

Alieleza serikali kupitia Bodi ya Korosho itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyama vya msingi katika kutathmini mahitaji ya viuatilifu na ratiba ya uagizaji wa viuatilifu hivyo.

Aidha, alisema serikali kupitia TPRI itaongeza udhibiti katika ukaguzi wa viuatilifu nchini ili kuviondoa sokoni visivyo na sifa.

Awali, alifafanua kuwa serikali haijaanzisha mfumo bubu wa ununuzi wa salfa na kwamba korosho huathiriwa na magonjwa ya aina mbalimbali yakiwamo yale yanayosababishwa na fungi.

Alitaja miongoni mwa magonjwa tishio kwa zao hilo ni ubwiriunga, blaiti, chule na mnyauko fusari.

"Hata hivyo, magonjwa hayo yamekwisha kupatiwa tiba isipokuwa mnyauko fusari. Serikali inaendelea na utafiti kupitia taasisi zake ili kupata kinga na tiba stahiki za magonjwa na wadudu wanaoshambulia zao hili nchini," alisema.

# Wizara yajipanga mfumo wa takwimu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imejipanga kuwa na mfumo mmoja wa takwimu za utafiti wa magonjwa mbalimbali ya binadamu ili kuondoa mkanganyiko uliopo kwenye taasisi mbalimbali nchini.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Faustine Ndugulile, alisema hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akifungua kongamano linalohusu udhibiti wa maambukizo ya virusi vya Ukimwi (VVU), lililoshirikisha taasisi mbalimbali za utafiti na wadau wa Ukimwi.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Taasisi ya Utafiti wa Tiba Afrika (Amref) na Mfuko wa Rais wa Marekani wa Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi (Perfar).

Alisema kumekuwapo na takwimu tofauti ambazo zinachanganya, hivyo kushindwa kuelewa ni zipi ambazo ni halisi kuhusu maambukizo mapya ya VVU na kuzitaka taasisi zinazojihusisha na utafiti kutumia mfumo wa serikali.

"Taasisi hizi zimekuwa zikikusanya takwimu na kuzipeleka kwenye mashirika ya nje ya nchi kuzitolea taarifa wakati zinatambua kuwa takwimu hizo ni za nchini tu, hivyo kuanzia sasa takwimu zote zitaratibiwa na NIMR," alisema.

Aidha, alisema ziko takwimu za utafiti mbalimbali lakini zimekuwa hazifanyiwi kazi na wala hazisaidii serikali, bali zinatumika kutolea taarifa kwenye makongamano tu.

Kutokana na utaratibu huo unaokiuka mfumo wa serikali wa utoaji taarifa, alisema kuanzia sasa lazima taasisi zote zinazojihusisha na utafiti wa Ukimwi, zishirikiane na NIMR ambayo itakuwa ikiratibu utafiti mbalimbali na kuingiza matokeo yake kwenye mfumo mmoja wa serikali.

Dk. Ndugulile alisema serikali imefanya maboresho mengi ikiwamo kuwa na mfumo mmoja wa takwimu, kuongeza muda wa kuchukua dawa za kufubaza makali ya Ukimwi kutoka miezi mitatu hadi sita, kutoa dawa kinga kwa makundi maalumu, yakiwamo wanaotumia dawa za kulevya, wanaofanya mapenzi ya jinsia moja na kinadada wanaojiuza.

# Wahofiwa kukatisha masomo kisa vyoo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANAFUNZI wa Shule ya awali na Msingi Dudumera katika Halmashauri ya Babati mkoani Manyara, wapo hatarini kukatiza masomo kwa sababu ya uhaba wa matundu ya vyoo na wengine kutokuwa rafiki na matundu yaliopo.

**Wanafunzi wengine wa awali wakiona hakuna vyoo wanavyoweza kutumia wengine wanaenda kujisaidia vichakani kwa sababu ya ile hofu ya kuogopa vyoo kuwa vikubwa.**

Hayo yalisemwa juzi na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Mussa Mkumbo, alipozungumza na Nipashe juu ya ubora wa matundu ya vyoo walivyo navyo, kama yanafaa kwa matumizi ya wanafunzi wa awali.

Alisema shule hiyo ina matundu 10 ya vyoo ambayo yanatumiwa na wanafunzi 95 wa awali na wanafunzi wengine 518, kuanzia darasa la kwanza hadi la saba.

"Sasa kutokana na upungufu wa matundu haya, kunahitajika jitihada za makusudi kwa serikali na wadau wa elimu katika halmashauri ili wanafunzi wetu wasikatize masomo sababu ya ukosefu wa vyoo," alisema.

Mkumbo alisema matundu ya vyoo yaliyopo ni machache na hayaendani na umri wa watoto wanaosoma elimu ya awali kwa kuwa ni vyoo vya shimo ambavyo watoto wa awali wanaweza kutumbukia.

"Kama shule haina vyoo vinavyofaa wanafunzi wa awali, wanaweza kuogopa na kuacha shule maana watakuwa wanawaza jinsi wanavyojaribu kuingia chooni na kushindwa kujisaidia," alisema na kuongeza:

"Wanafunzi wengine wa awali wakiona hakuna vyoo wanavyoweza kutumia wengine wanaenda kujisaidia vichakani kwa sababu ya ile hofu ya kuogopa vyoo kuwa vikubwa."

Aidha, alisema katika shule yake wameshindwa kuwa na matundu ya vyoo ya kutosha na vinavyofaa kwa matumizi ya wanafunzi wa awali kutokana na mvutano wa wanakijiji walio nao wa zaidi ya miaka miwili ambao unawafanya miundombinu ya vyoo iendelee kuwa tatizo shuleni hapo.

Pia alisema ukosefu wa ujenzi wa vyoo rafiki kwa wanafunzi wa awali una madhara kwa wanafunzi kwa kuwa wanaweza kukata tamaa kwenda shuleni wakihofia vyoo hivyo na kuchukia shule sababu mazingira si rafiki.

Naye Mwalimu wa Shule ya Awali, Jemima Njidile, alikiri kuwa shule hiyo haina vyoo vizuri vya wanafunzi wa awali, kwani kwao inakuwa changamoto na inawalazimu kuwasindikiza chooni wanapohitaji kwenda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Hamisi Malinga, alikiri kuwapo kwa mvutano wa wazazi ambao umesababishwa na masuala ya kisiasa, kutokana na Kijiji cha Mawemailo kuongozwa na upinzani ambao unapinga kila kitu cha maendeleo.

Malinga alisema jukumu la ujenzi wa miundombinu ya vyoo ni la wananchi kwa asilimia 100 na serikali haiwezi kuchangia kila kitu.

Kwa upande wake, Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji cha Mawemairo, Jumanne Mustafa alisema wao hawavutani juu ya ujenzi wa vyoo, bali walisitisha kuchangia vyoo kutokana na michango kuwa mingi, hivyo wanasubiri uchaguzi wa serikali za mitaa ufanyike ili viongozi watakaopatikana walisimamie suala hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula (watatu kulia), akipeana mkono na viongozi wa mashirika ya ECLAT Foundation na Upendo Society, baada ya kukabidhiwa nyumba ya walimu, matundu 23 ya vyoo na madarasa ya Shule ya Msingi Kimelok, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Uanzishaji misitu wasaidia kuokoa ikolojia Gombe

**Novatus Makunga,** ARUSHA

UANZISHAJI wa misitu yenye ukubwa wa hekta 116,693 katika vijiji 58 vya Wilaya ya Tanganyika umesaidia kuokoa ikolojia ya Gombe ambayo ni maarufu kwa upatikanaji wa sokwe mtu.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Huduma za Uhifadhi wa Taasisi ya Kimataifa ya Jane Goodall, Dk. Shadrack Kamenya, katika mada ya

umuhimu wa misitu ya jamii kwenye mkutano wa kisayansi wa maeneo tengefu uliofanyika mjini hapa.

Alisema hatua hiyo imesaidia katika kuhifadhi eneo tengefu la misitu la Gombe- Masito Ugalla katika Mkoa wa Kigoma.

Dk. Kamenya alisema mbali na misitu hiyo kuhifadhi mazingira, pia imekuwa ikiwaingizia kipato wananchi wa vijiji hivyo kwa ufugaji wa nyuki na nishati kwa ajili ya kupikia na dawa mbalimbali za tiba mbadala.

Alisema hivi sasa kuna vikundi vya wafugaji nyuki 19 vyenye wanachama 365 ambavyo vilianzishwa kwa kupatiwa zaidi ya mizinga 500 na taasisi ya Jane Goodall.

Alisema kijiji cha Vikonge katika Kata ya Tongwe Halmashauri ya Mpanda ndicho chenye msitu mkubwa zaidi wenye hekta 16,717.

Aidha, Dk. Kamenya alisema pia wanawawezesha kupitia Benki ya Jamii ya Uhifadhi ya Mazingira (Cocoba) kwa kuwapatia mitaji ya kuendeshea shughuli za uzalishaji.


"Benki hizi zinawawezesha kuendesha shughuli mbalimbali, hivyo kuacha kushiriki katika uharibifu wa mazingira, huku wakiwa wakereketwa wa kulinda misitu na uhifadhi," alisema.

Alizitaja shughuli hizo kuwa ni pamoja na ukulima wa mazao ya chakula na biashara ambayo ni mahindi, mhogo, maharage, viazi vitamu na michikichi.

Dk. Kamenya alitaja soko kubwa la mazao hayo kuwa ni pamoja ni ndani na nje ya nchi ikiwamo Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Zambia.

Akizungumzia uhifadhi wa sokwe mtu, Dk. Kamenya alisema hivi sasa kuna jumuiya tatu za wanyama hao ambazo zilianza kubainishwa na mtafiti wa sokwe mtu, Dk. Jane Goodall kuanzia mwaka 1960.

Alisema jumuyia kubwa zaidi ambayo inaishi katikati ya Hifadhi ya Taifa ya Gombe inafahamika kwa jina la Kasakela ikiwa na sokwe 56 ikifuatiwa na Mitumba yenye sokwe 27 inayoishi kaskazini mwa hifadhi hiyo na ya tatu ni Kalande yenye sokwe kati ya sita na tisa iliyoko kusini.





# Kichanga chaokotwa hai shimo la choo

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MTOTO mchanga anayekadiriwa kuwa na umri wa siku moja, ameokotwa akiwa hai karibu na shimo la choo, baada ya mama yake mzazi kumtupa kwa kisingizio cha kukabiliwa na ukata wa fedha.

Mtoto huyo aliokotwa na wasamaria wema juzi baada ya kutupwa na mama yake, Rabia Yunisi (19), mkazi wa Kijiji cha Merali, Sanya Juu wilayani Siha, muda mfupi baada ya kuzaliwa.

Akizungumzia tukio hilo, Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani humo, Peter Msaka, alisema mtoto huyo kwa sasa anaendelea vizuri na analelewa katika kituo kimoja kilichoko Machame Wilaya ya Hai.

"Ni kweli huyo mtoto aliokotwa na wasamaria wema waliokuwa wakienda shambani majira ya asubuhi pembezoni mwa choo baada ya kusikia kikilia. Walipojaribu kutafuta sauti inatokea wapi, ndipo wakagundua alikuwa amelazwa chini akiwa amefunikwa na nguo gubigubi," alieleza Msaka.

**Amenieleza kwamba jambo lingine lililomsukuma kumtupa mtoto huyo ni mwanamume aliyezaa naye alimkimbia na kumwachia mtoto wa kwanza na kulazimika kutunzwa na wazazi wake.**

Mmoja wa wasaidizi wa kisheria wa Wilaya ya Siha, Hamza Munisi, anayefanya Shirika la Kwieco, alisema wamekuwa mstari wa mbele kutoa elimu kuhusu ukatili wa aina hiyo na kuwasihi wanawake wanaotupa watoto kwa madai ya ugumu wa maisha, kuheshimu haki za binadamu kwa kuwa vichanga hivyo navyo vina haki ya kuishi na kulindwa.

Asia Mzava, Mjumbe wa Serikali ya Kijiji hicho, alisema alipigiwa simu na wasamaria wema na kujulishwa kuwa wana wasiwasi na binti ambaye ni jirani yao kwamba huenda amehusika katika utoaji mimba kwa kuwa alikuwa mjamzito.

Baada ya taarifa hiyo, mjumbe huyo alisema majira ya usiku aliamua kumfuata binti huyo na kumhoji kuhusu ujauzito aliokuwa nao ameupeleka wapi na kujibiwa na binti huyo kuwa hakuwa mjamzito.

Hata hivyo, alisema alipombana zaidi na kumtishia kumpeleka Hospitali ya Wilaya kufanyiwa uchunguzi, alipokubali alikuwa mjamzito na alijifungua na kumtelekeza mtoto huyo chooni.

"Huyo binti huyo amenieleza kisa kizima kilichomsababisha aamue kumtupa mtoto huyo na kumkana si wake kwamba ni kutokana na ukali wa mama yake mzazi (jina limehifadhiwa) ambaye aliwahi kumpa maneno makali alipojifungua mtoto wa kwanza ambayo akikumbuka yanamuumiza.

"Amenieleza kwamba jambo lingine lililomsukuma kumtupa mtoto huyo ni mwanamume aliyezaa naye alimkimbia na kumwachia mtoto wa kwanza na kulazimika kutunzwa na wazazi wake, hivyo akaona hali itakuwa mbaya na anaweza kufukuzwa nyumbani," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Arfaxard Nkinda, alipoulizwa kuhusu hatua zilizochukuliwa, alisema uamuzi wao waliofanya ni kumkamata na kumfikisha Kituo Kikuu cha Polisi Sanya Juu na pia kumpeleka mtoto huyo hospitali ya wilaya kwa ajili ya uchunguzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Hamis Issah, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema hana taarifa ya kukamatwa kwa mama huyo.

# Mtoto atoweka nyumbani kwao

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Malindi, Same mkoani Kilimanjaro, Silasi Enea (16), ametoweka nyumbani kwao na hajulikani aliko kwa mwezi mmoja sasa.

Akizungumza na Nipashe juzi, baba mzazi wa mtoto huyo, Enea Msisili, alisema mwanawe alitoweka nyumbani kwao Agosti 9, mwaka huu, majira ya asubuhi alipoaga kuwa anakwenda shuleni.

"Mtoto wangu anaishi na bibi yake mzaa mama yake, Lenasa Msuya, maeneo ya Makanya Same. Siku hiyo alivaa nguo za shule shati jeupe, suruali ya kijivu na sweta jekundu na kuaga anaenda shuleni," alisema.

Alisema cha ajabu muda wake wa kurudi nyumbani ulipofika, hakurudi na ndipo jitihada za kumtafuta kwa ndugu, jamaa na marafiki zilipoanza kufanyika, bila kuzaa matunda hadi sasa.

Kwa mujibu wa Msisili, walijaribu kuulizia shuleni kwake lakini cha kusikitisha walielezwa na uongozi wa shule kwamba siku hiyo hata shuleni hakufika.

Alisema mtoto huyo (pichani) hana tabia ya kuondoka nyumbani bila kuaga au kulala nje ya nyumbani na ni mtoto mwadilifu na heshima, hivyo wameshangaa kitendo cha kupotea hadi leo.

"Tumeotoa taarifa Kituo cha Polisi Makanya na kupewa RB/ 157/2019 na namba za Polisi 0787059587/0754563751 kwa yoyote atakayemwona atoe taarifa kwenye namba hizo," alisema.



Katibu Mtendaji wa chama cha wanawake watumishi wastaafu wa serikali katika Manispaa ya Moshi, Delphina Iria, akisoma risala kwa niaba ya wastaafu wenzake kwa Diwani wa Kata ya Bomambuzi, Juma Raibu (hayupo pichani), wakati wa mkutano maalumu wa chama hicho, mjini Moshi mkoani Kilimanjaro, jana. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wasomesha watoto wa familia maskini

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

WAKULIMA wa kahawa katika Kata ya Nanjara, Useri, wilayani Rombo, wameamua kuacha 'kumbukumbu isiyofutika' ya kuchanga fedha za kusomesha watoto 12 kutoka familia za wasiojiweza kiuchumi, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kwa kipindi cha miaka 10.

Katibu wa Chama cha Ushirika wa Mazao cha Tarakea Amcos, Bertha Shirima, alisema ushirika huo licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama kuchelewa kuanza kwa miradi ya ujenzi wa maduka makubwa mawili ya pembejeo na vifaa vya ujenzi, waliamua kuwekeza katika elimu.

"Hata kabla ya Rais wetu John Magufuli kutangaza serikali itagharamia utekelezaji wa elimu bila malipo, sisi Tarakea Amcos tuliwalipia watoto 12 waliokuwa na mazingira magumu sehemu ya ada ya shule kila mwaka, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne," alisema.

Chama hicho kimetoa rai kwa wakazi wa Rombo kuweka akiba za kuwasomesha watoto wao hadi chuo kikuu badala ya kuiachia serikali mzigo wa kusomesha hata wale wenye uwezo.

"Tatizo lililoko nchini na hasa Rombo, wazazi wengi wanawasomesha watoto wao hadi kidato cha sita tu na wanategemea serikali iwasomeshe elimu ya juu au kupata ufadhili nje ya nchi. Hii imesababisha wanafunzi wengi wanakimbilia vyuo vya serikali na hata kusababisha wale wasio na uwezo kukosa nafasi," alisisitiza.

Alisema hiyo pia inachangia vijana wengi wanaokosa fursa za masoko nchini katika vyuo vya serikali na vile vya binafsi na hushirikiana na wazazi wao kutafuta ufadhili wa masomo ya nje ya nchi bila kuzingatia aina ya masomo na mazingira wanayoenda kusoma.

"Matokeo ya haya, wanafunzi wanalazimika kusoma lugha za watu kwanza na pia kulazimika kuishi maisha magumu katika nchi hizo. Kama mzazi angekuwa amejipanga angempeleka chuo cha bei rahisi, lakini pia vilivyopo si mazingira salama ya kuishi," alisema Shirima.

Pia wakulima hao wamevuka vigingi vya ukata wa fedha na kufanikiwa kujenga ukumbi wa kisasa wa mikutano unaochukua zaidi ya watu 300 wakiwa wamekaa vitini kwa gharama ya Sh. milioni 20 na kisha kutumia Sh. milioni tano kujenga uzio kuzunguka eneo hilo.

Chama hicho ndicho kinachosotea hati miliki ya ardhi bila mafanikio baada ya kupambania kwa miaka 13, huku kikielekeza kilio chake idara ya ardhi ya wilaya hiyo na Serikali ya Kijiji cha Kibaoni.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 12, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Wafundishwa staili nne za kuepuka maambukizi mapya

Ukurasa 14



Wodi mpya inayolamba Sh.mil 400 DC akilia na mabusha, ukosefu vyoo

Ukurasa 18



RC Zambi, DC Rukia waangukia kauli 'tume zichoka mimba shuleni'

Ukurasa 19




Wajadili kwa vipengele dhana ukatili wa mtoto, ushirikiano

Ukurasa 20




RC ACHARUKA 'HAIKUBALIKI'...

# NUSU WAKAZI MKOA SHINYANGA HAWANA VYOO; MBADALA PORINI, MIFUKO, PAGALA

Ukurasa 16



Victor Vescovo, akiwa ndani ya chombo chake. **PICHA: MTANDAO.**

## Bahari zote ana rekodi, sasa Km. 5.5

**NA JONATHAN AMOS**

BINGWA wa kuzama baharini, Victor Vescovo, amekuwa kinara duniani kuweza kufika kina kirefu zaidi majini, katika kila bahari, kuliko mwogeleaji mwingine duniani.

Safari yenye kina kirefu zaidi alichozama wakati huu katika bahari ya Arctic, ni urefu wa kilomita 5.5 ambayo ni sawa na maili 3.4.

Katika miezi 10 iliyopita, Vescovo alizama katika bahari za Pacific, Hindi, Bahari ya Kusini na Atlantic analieleza hilo kwa kauli: "Nimetokea kwenye falsafa inayosema tumeletwa hapa si kuishi tu au kuridhika tu, ila ni kutoa mchango aina fulani.

"Njia niliyochagua ni kuwa na safari na kufanya jambo linayoweza kutusogeza mbele kama viumbe."

Huko nyuma, akiongozwa na wataalamu wa Jeshi la Marekani, aliwezeshwa safari za angani na kupanda milima katika mabara mbalimbali duniani.

AFYA

VITA VYA EBOLA

# Wafundishwa staili nne za kuepuka maambukizi mapya

- Maofisa 'wawinda' wagonjwa mpakani
- Elimu kwenye mabasi, malori, bodaboda
- Shida iko soko jirani, kusalimiana ovyo

**Na Augusta Njoji, aliyekuwa Mtukula**

EBOLA imo katika virusi hatari zaidi duniani. Kwa hivi karibuni, ni homa inayokuwa tishio kwa nchi za maziwa makuu, ikiwamo Tanzania.

Wataalamu wa afya wanasema kuepuka ebola ni rahisi, iwapo mtu atafuata tahadhari nne muhimu.

Njia hizo, kwanza ni kunawa kwa sabuni na maji na kila baada ya shughuli anajikausha na taulo ili kuviua virusi hivyo vya ebola.

Njia ya pili, inatajwa kuepuka kusalimiana kwa mikono au kugusana kwa njia yoyote na mtu unayemshuku kuwa ana maradhi ya ebola, kwa kuwa maji ya mwili kama vile mkojo na kinyesi, matapishi, kamasi, mate, machozi na mbegu za kiume na maji ya uke vyote, vinaeneza ugonjwa huo.

Njia ya tatu, inatajwa ni kuepuka miili ya wafu ambao mtu anaodhani wamefariki kutokana na kuugua ebola. Mtu anatakiwa asiuguse mwili huo, kwa kuwa hata kama amefariki anaweza kupata maambukizi ya ebola.

Njia ya nne, ni kuepuka kuwinda, kugusa au kula nyama ya porini, mfano popo, nyani na sokwe. Hao, wanasayansi wanaamini kwamba ndiyo chanzo cha maambukizi kwa binadamu.



Ofisa Afya katika mpaka wa Rusumo, kati ya Tanzania na Rwanda, Oswald Kimasi, akionyesha kifaa cha kubaini wagonjwa wa ebola.

### Dodoso la ziara

Katika kuangalia uimarishaji wa huduma za afya mipakani, Ofisa Afya katika Mpaka wa Rusumo, kati ya Tanzania na Rwanda, Oswald Kimasi, anasema kutokana na tishio kubwa la ugonjwa huo, ni vyema wananchi wakazingatia kanuni hizo za kujiepusha na kupata Ebola.

> "Tuna vikaratasi maalum tunavitoa kwa mtu ambaye tayari tumemfanyia 'scanning.' Hivyo, anapokwenda kwa Ofisa Uhamiaji...

Anataja dalili za ugonjwa, mtu anakuwa na joto kali mwilini zaidi ya nyuzi joto 38, ikiambtana na maumivu ya misuli na viungo, vidonda kooni, kuumwa kichwa, uchovu, kichefuchefu, kutapika na kuharisha na mtu anaweza kutokwa na damu.

### Udhibiti mipakani

Kiomasi anasema, katika mpaka wa Rusumo wamejipanga kwa kiwango kikubwa kudhibiti ugonjwa huo usiingie nchini na inapotokea abiria anashukiwa kuwa na dalili za ebola, wanachukua taarifa zake na anapelekwa katika hospitali ya wilaya, ambako ikithibitika sio, anaruhusiwa kuendelea na safari.

"Tuna vikaratasi maalum tunavitoa kwa mtu ambaye tayari tumemfanyia 'scanning.' Hivyo, anapokwenda kwa Ofisa Uhamiaji au TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) anaonyesha kikaratasi hicho, ndipo anaendelea kupewa huduma na kama hatapita kukaguliwa hapa, kule akienda lazima arudishwe hapa kupimwa,"anasema.

Anasema ushirikiano uliopo ni wa kila siku kwa maofisa wote wa TRA, Uhamiaji, Polisi, walinzi na madereva wa pikipiki na magari.

"Watu wanaotoka Kongo (DRC) tumewawekea fomu maalum ili kuonyesha atafikia wapi akiwa Tanzania na siku atakazokaa na kurejea nchini kwake, ili kufuatilia kwa karibu kudhibiti ugonjwa huo,"anasema.

Ofisa Afya Mfawidhi katika Mpaka wa Mtukula, kati ya Tanzania na Uganda, Mathew Godfrey, anasema serikali imeshatoa vitendea kazi

Inaendelea Uk.15

AFYA



Eneo maalum la kuwaweka wanaohisiwa na ugonjwa wa Ebola. **PICHA ZOTE: AGUSTA NJOJI.**

# Wafundishwa staili nne za kuepuka maambukizi mapya

**Inaendelea Uk.14**

vya kukabiliana na ugonjwa huo na kwamba wamejipanga vya kutosha kuhakikisha hauingii nchini.

"Tunafanya 'sensation' (hisia) kwa abiria, madereva na watu wote wanaohusika kwenye magari yanayopita kwenye mpaka wetu," anasema Godfrey.

Anaongeza:"Pia jamii inayotuzunguka ikiwamo madereva wa bodaboda tumewaeleza wakiona au kumhisi mgonjwa mwenye dalili za kuwa na joto kali, kutapika, viungo kuuma na kutokwa na damu sehemu za mwili watoe taarifa kwenye ofisi iliyopo mpakani."

Godfrey anasema, waendesha pikipiki wamepewa elimu ya utoaji taarifa wanapomhisi mgonjwa mwenye dalili hizo na anafafanua zaidi: "Kutokana na kusambaa pia kwa kushikana tunatoa huduma hapa mpakani ya kunawa mikono ili kuchukua tahadhari kama wanapokuwa safarini wameshikana na mgonjwa wa Ebola.

"Ikitokea tumempata anayehisiwa wa ugonjwa wa ebola, kuna eneo maalum tunamhifadhi na kutoa taarifa kwa hospitali ya wilaya wanamchukua na kumpeleka sehemu husika," anasema.

Godfrey anasema, kondakta au dereva wamekuwa wakitoa taarifa kabla ya kufika kilomita 20 mpakani, kama gari lake linapokuwa salama hakuna mgonjwa au kama kuna mgonjwa wanayemhisi.

"Baada ya taarifa hiyo wanapofika mpakani tunakagua abiria mmoja mmoja kwa kupima joto na kudhibitisha kama kilichosemwa na abiria au dereva kipi salama, Joto la mtu mwenye dalili au anayehisiwa akikutwa na nyuzi joto 38 au zaidi na tunapima mmoja mmoja kwa kutumia 'hand scanner' (sakana na mkononi) ambayo tumeletewa na Wizara," anasema.



Ofisa Afya Mfawidhi wa mpaka wa Mtukula, kati ya Tanzania na Uganda, Mathew Godfrey, akifafanua jambo kuhusu udhibiti wa ebola mpakani.

**Waziri Ummy**

Kutokana na tishio la ugonjwa huo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema ni ugonjwa ulio hatarini kusambaa haraka kati ya nchi moja na nyingine, hivyo kunahitajika mikakati ya pamoja kimataifa kuudhibiti.

Anasema, kuwapo mwingiliano mkubwa wa watu kutoka nchi jirani za Uganda na Congo, eneo la mipaka rasmi na isiyo rasmi hasa katika mikoa ya Kagera, Mwanza na Kigoma, kunaiweka nchi katika tishio la kupata maambukizi ya ebola.

Waziri anaitaja mikoa iliyo hatarini kutokana na mwingiliano wa watu kibiashara na kifamilia ni Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Dodoma na Dar es Salaam, hali inayoiweka nchi nzima kwenye tishio hilo.

"Wizara inapenda kutoa tahadhari ya ugonjwa huu kwa wananchi katika mikoa yote ya Tanzania, pia kuwataka kuchukua hatua stahiki za kujikinga na kudhibiti ugonjwa huo usiingie nchini mwetu," anasema Ummy.

Katika mkakati wa kiwizara, waziri alitoa wito kwa wananchi watakapoona dalili za ugonjwa huo, kupiga simu ya bure anayoitaja '0800110124' au '0800110125' au kutoka taarifa kwa mamlaka za serikali ya mitaa na vituo vya kutoa huduma za afya.

**Ushauri TRA**

Ofisa Mfawidhi wa TRA kwenye mpaka wa Mtukula, William Mkenda, anasema kuwapo mwingiliano wa watu kwenye masoko ya mipaka ya kuingilia Tanzania, kunapaswa kukatolewa elimu ya kutosha kwa wananchi wanaozunguka katika namna ya kuukabili ugonjwa huo.

Anasema, elimu hiyo inapaswa itolewe kwa viongozi wa serikali za mitaa wa maeneo hayo, kwa wao ni rahisi kubaini dalili kabla ya haya kuingia eneo la mpaka.

"Mtu anavyoambiwa mpakani anaweza kufikiri mpaka unatenganishwa na ukuta au kizuizi watu wa jamii moja na wengine wasionane, lakini si hivyo. Ukiona uhalisia wa mpaka ni watu wanaoweza kuingiliana kwa namna fulani kubwa sana," anasema Mkenda

"Hapa ndani kwenye mpaka tumejipanga vizuri, lakini inatakiwa elimu itolewe kwa hawa viongozi wa serikali za mitaa, kwa kuwa kuna watu wanatoka sokoni upande mmoja kwenda mwingine. Ni rahisi wao kumuona mtu hatua za awali na kutoa taarifa kabla ya kukutana na mtu mwingine," anasema

Anaendelea kuwa maofisa wa idara mbalimbali katika mpaka huo walipatiwa elimu mwaka jana, mara baada ya ebola kuibuka nchini DRC, hivyo kila mmoja anashiriki kuhakikisha ugonjwa hauingii nchini.

"Pia hivi karibuni nchini Uganda kuna watu walishukiwa kuwa na maambukizi ya ebola. Kulikuwapo utayari hapa mpakani, iliendeshwa na watu wa Idara ya Afya juu ya kumtambua mtu mwenye ugonjwa huo na kutoa taarifa na kukabiliana," anaeleza.

**Madereva wafunguka**

Dereva wa Lori kutoka nchini DRC, Ally Mpame, anasema nchini kwao wamejipanga kwa kiwango kikubwa kuudhibiti ugonjwa huo na rai yake ya awali, ni kwamba watu wasipende kushikana mikono, ili kuepuka maambukizi .

"Nawashauri madereva wenzangu ambao tunaenda kwenye nchi hizo kuhakikisha kila tunapoingia na kutoka, tunaangaliwa afya zetu ili tusiingize ebola nchini Tanzania," anasema.

Ushauri mwingine ni mwendesha pikipiki kutoka nchini Rwanda, Damasent Twisent, anasema katika mpaka wa Rusumo, waendesha pikipiki wanaobeba abiria nao wanapimwa afya kila wanapobeba abiria, badala ya abiria pekee kupimwa.

Tangu mwezi Agosti mwaka jana hadi sasa, nchini DRC, takwimu zinaonyesha kulikuwapo wagonjwa 2,997 waliothibitishwa kuwa na ugonjwa huo na kati yao kuna vifo 1,998, ambavyo ni sawa na asilimia 67 ya wagonjwa wote.

Aidha, kati ya waliofariki kutokana na ugonjwa huo, taarifa zinaonyesha watu 130 ambao ni sawa na asilimia saba, ni watumishi wa afya.

Nchini Uganda, kunaelezwa kwamba Agosti 29 mwaka huu, kumethibitisha kifo cha msichana wa miaka tisa, aliyekuwa akisafiri na mama yake kutoka nchini DRC.

RC ACHARUKA 'HAIKUBALIKI'...

# NUSU WAKAZI MKOA SHINYANGA HAWANA VYOO; MBADALA PORINI, MIFUKO, PAGALA

- Kwanini? Eti uchuro kuchangia na wakwe
- Operesheni 'lazima choo' kupita kila nyumba
- Magari majitaka manispaa yatapisha porini

**Na Marco Maduhu, Shinyanga**

KAMPENI ya usafi wa mazingira kitaifa nchini Tanzania, ilizinduliwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, Mei 5. 2012 Mjini Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro

Inaelezwa, usafi wa mazingira hauishii katika mazingira, katika kufagia, kufyeka nyasi na kuzibua mitaro michafu tu, bali hata kaya kuwa na choo kuhakikisha magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu hayapewi nafasi kuhatarisha afya za wananchi.

Rais Dk. John Magufuli, mara tu baada ya kuingia madarakani, aliagiza kufanyika usafi nchi nzima kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi, ili kuhakikisha wananchi wanakuwa katika mazingira safi kiafya.

Takwimu za mkoa zinaonyesha nusu pekee (asilimia 50.6) ya wanajamii hao ndio wenye vyoo bora na waliobaki kuviweka kama maonyesho kwa ajili ya kumridhisha bwana afya wakati wa ukaguzi wa vyoo.

Nini tatizo? Kuna mila potofu kuwa wanajamii hawapo tayari kuchangia choo kimoja na wakwe zao, jambo linalomkera zaidi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack.

Anaamua kulivalia njuga suala hilo, la ujenzi wa choo na kuzindua kampeni ya 'nyumba ni choo' inayolenga kuhakikisha hadi kufikia mwezi Desemba mwaka huu, kila kaya mkoani inakuwa na choo bora kinachotumiwa.

Mkuu wa Mkoa huyo anasema: "Haiwezekani wananchi waendelee kuishi kwenye nyumba zao bila ya kuwa na choo. Ni aibu sana kwenda kujisaidia vichakani; baba, mama, watoto pamoja na wageni wanaofika kwenye familia hiyo, hatimaye kuchafua mazingira.

"Suala la kaya kutokuwa na choo kwenye mkoa wangu sikubaliani nalo, hivyo naagiza maofisa afya wote wa mitaa mniletee mpango wenu kazi, ili tuanze kukagua choo nyumba kwa nyumba, na ambayo tutaikuta haina choo tutaichukulia hatua. Lengo letu hadi kufikia Desemba (2019) kaya zote ziwe na huduma ya choo."

Anaongeza: "Kwa vile tunaelekea kwenye kipindi cha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, nawaomba sana wanasiasa wasije wakatuingilia kwenye zoezi hili, hasa pale tutakapokuwa tukiwakamata wananchi wasio na vyoo na kuanza kuwakingia kifua eti tuwaache ni wapiga kura wao, kwani hatutaki mzaha kwenye jambo hili."

**Ofisa Afya**

Neema Simba ni Ofisa Afya wa Mkoa wa Shinyanga, anasema kuwapo wakazi milioni 1.8 wanaopatikana katika kaya 284,701, lakini wanaotumia vyoo bora ni kaya 129,820 sawa na asilimia 50.6 na wasio na vyoo kabisa ni kaya 7,195 sawa na asilimia 5.5.

Anataja takwimu za kaya zenye vyoo bora kwa kila halmashauri sita za mkoa huo, katika Mji Kahama, kuna kaya 55,708 lakini wenye vyoo ni asilimia 75; Msalala kuna kaya 42,920 na wanaotumia vyoo ni asilimia 57,3 na wasio na vyoo asilimia 4.4.

Halmashauri ya Ushetu, wanaotumia vyoo ni asilimia 20.9; Shinyanga Manispaa wenye vyoo ni asilimia 64.7; Shinyanga Vijijini wanaotumia vyoo ni asilimia 19.7; Halmashauri ya Wilaya Kishapu, wanaotumia vyoo ni asilimia 71.

"Kampeni hii ya 'Nyumba ni Choo' ya kupita nyumba kwa nyumba kukagua choo, itasaidia kwa kiasi kikubwa kuondokana na tatizo la watu kujenga nyumba zao, bila ya kuwa na huduma ya choo, hatimaye kuondoa wasiwasi mkubwa wa kupatwa na magonjwa ya mlipuko, hasa kwenye kipindi cha mvua," anasema ofisa afya.



Mkuu wa Mkoa Shinyanga, Zainabu Telack (wa pili kutoka kushoto), akiongoza maandamano ya uzinduzi wa kuhamasisha wananchi wa Mkoa wa Shinyanga. kujenga vyoo bora. Wanaofuatia kushoto kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, Katibu Tawala wa Mkoa, Albert Msovela. Wa kwanza kushoto, ni Mrisho Mpoto, Balozi wa Kampeni ya 'Nyumba ni Choo'.

> "Suala la kaya kutokuwa na choo kwenye mkoa wangu sikubaliani nalo, hivyo naagiza maofisa afya wote wa mitaa mniletee mpango wenu kazi, ili tuanze kukagua choo nyumba kwa nyumba, na ambayo tutaikuta haina choo tutaichukulia hatua. Lengo letu hadi kufikia Desemba (2019) kaya zote ziwe na huduma ya choo."




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, akiwa na Balozi wa Kampeni ya 'Nyumba ni Choo,' Mrisho Mpoto. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

Wakazi wasemavyo

Jonasi Apolo ni mkazi wa Shinyanga, anasema tatizo la nyumba nyingi kutokuwa na choo si vijijini pekee kama baadhi wanavyodhani, bali hata mjini kuna tatizo la kukosekana vyoo, hasa kwenye nyumba za kupanga, ambako wanajisaidia katika mifuko na mapagala ya majengo.

Apolo anafafanua matatizo ya vyoo katika nyumba wanazoishi mijini, akisema: "Hapa mjini kuna nyumba nyingi hazina vyoo kabisa, hasa hizi ambazo tunapanga. Utakuta watu wote wanatoka mmoja mmoja kwenda kujisaidia ambako hakujulikani, pamoja wengine kwenye mapagala."

Mkazi wa mjini Shinyanga, Protas Nzelano, anaipongeza operesheni hiyo ya Mkuu wa Mkoa, kusaka nyumba kwa nyumba vyoo bora, itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza uchafuzi wa mazingira.

"Namuomba Mkuu wa Mkoa kwenye kampeni hii ya ujenzi wa vyoo kwenye makazi ya watu aunde kabisa 'task force' (kikosi kazi) watu wakamatwe. Haiwezekani mtu unajenga nyumba, halafu hakuna choo, eti unakwenda kujisaidia vichakani. Hii ni dharau kwa kuchafua mazingira kwa makusudi," anasema Nzelano.

**Mrisho Mpoto**

Balozi wa Kampeni ya 'Nyumba ni Choo' ni msanii, Mrisho Mpoto, anasema wapo mkoani Shinyanga kuungana na serikali kuhakikisha wakazi wote nyumba zao zinakuwa na choo na kuacha tabia ya kujisaidia vichakani wakichafua mazingira.

Anasema mwaka 1961 wakati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alipowezesha Tanganyika kupata uhuru, alianza kupigana na maadui watatu, ambao ni Ujinga, Umaskini na Maradhi na mwaka 1973 ikaanzishwa kampeni 'Mtu ni Afya.'

Mpoto analalamika kwamba, hadi sasa imetimu miaka 58 sawa na nusu karne, akilaumu kuwa ni jambo la aibu kubwa.

"Mpango wa Dunia hadi kufikia Mwaka (2030) nyumba zote nchini ziwe na vyoo bora, lakini Mpango wa Tanzania kufikia (2022) nyumba zote zinatakiwa ziwe na vyoo. Ndio maana tunafanya kampeni hii kwenye mikoa yote kuhamasisha wananchi wajenge vyoo kwenye nyumba zao.

"Kampeni hii ya usafi wa mazingira ya kuhamasisha wananchi wajenge vyoo bora, pia tumeifanya kwenye mikoa ya Tanga, Morogoro, Mbeya, Songea, Kagera, Mwanza, Geita, Mara, na sasa tupo Shinyanga, ambayo tutahamasisha ndani ya siku 21 watu wajenge vyoo kwenye nyumba zao," anaongeza.

Pia, rai yake ni Watanzania waitikie wito wa kampeni hiyo ya nyumba kwa vyoo, ili nchi iondokane na suala la kujadili ujenzi wa vyoo kila kukicha, jambo ambalo katika sura ta pili, linafungua mlango viongozi kujadili mengine yahusuyo nchi.

**Mratibu wizarani**

Mratibu wa Uhamasishaji Kampeni ya 'Nyumba ni Choo' kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Elizabeth Malingumu, anasema kwenye utoaji wa hamasa hiyo, watazunguka mkoa mzima wa Shinyanga, kutoa elimu ya umuhimu wa kuwa na choo.

Anasema jamii nyingine hasa za maeneo ya vijijini, wengi wameshaathiriwa na mila zilizopitwa na wakati, wakiwamini katika kujisaidia vichakani, jambo linalohitaji juu ya umuhimu wa matumizi ya choo.

"Kampeni yetu hii ya 'Nyumba ni Choo' tutazunguka nchi nzima. Kuna baadhi ya mikoa tayari tumeshapita na sasa tupo hapa Shinyanga. Lengo letu ni kuhamasisha usafi wa mazingira, kwa wananchi kujenga vyoo bora kwenye nyumba zao, na kuacha kujisaidia ovyo na kusababisha

Inaendelea Uk.20





Mkurugenzi Mkuu WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus. **PICHA: MAKTABA.**

# WHO: Kila sekunde 40 yupo anayejiua duniani

- Wawazidi wanaouawa; wanaume zaidi; vijana chanzo namba 2

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limesema karibu wastani wa watu 800,000 hujiua kila mwaka duniani, ikiwa ni kiasi kinachowazidi wanaokufa ama kwa vita na mauaji, akiyataja kuwa mauaji ya mtu dhidi ya mwingine au saratani ya matiti.

Katika ripoti yake mpya, WHO inasema viwango vya wastani wa kujiua duniani vimepungua, ikilinganishwa na kipindi kati ya mwaka 2010 na 2016.

Hata hivyo, ikirejea watu wanaojiua, idadi imeendelea kuwa ileile, kutokana na ongezeko la idadi ya watu duniani.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus, anasema katika taarifa kuwa licha ya hatua zilizopigwa, wastani uliopo kuna mtu anafariki kila sekunde 40 kutokana na kujiua.

Takwimu za mwaka 2016 ambao ndiyo wa mwisho kutolewa kuhusu kujiua, zilionyesha kuwa kwa kila watu kulikuwapo watu 100,000 wanaojiua na katika vifo hivyo kuna wastani wa vifo 10.5 vinavyotokana na kujiua.

Inagawa inaelezwa wastani wa viwango vya kujiua duniani vilipungua kwa takriban asilimia 10 kuanzia 2010 hadi 2016, Kanda ya Amerika ilionyesha ongezeko la viwango hivyo kwa asilimia sita, katika kipindi cha miaka sita.

Mtaalamu kutoka Kitengo cha Afya ya Akili cha WHO, Alexander Fleischmann, anasema mauaji ya kujiua ni tatizo kubwa la afya ya jamii na kutoa wito wake ni hatua zichukuliwe kushughulikia tatizo hilo.

"Ni muhimu wakati wote katika kuzuia vifo vya kujiua, kwamba tunawashikilia watu wanaotuzunguka. Tunapaswa kuchukulia kwa uzito mtu anaposema hataki tena kuishi au hata wanaposema kwa uthabiti kwamba wanataka kujitoa uhai wao.

"Kila moja wetu ana jukumu katika kuzuia vifo vya kujiua. Hivyo, sote tunaweza kujitolea kuwasikiliza watu wanaotuzunguka wanapokuwa kwenye huzuni au wanataka msaada wetu," anasema.

Ripoti hiyo ya WHO, inasema idadi ya mataifa yaliyo na mikakati kuzuwia watu kujiua imeongezeka katika kipindi cha miaka mitano tangu kuchapishwa ripoti ya kwanza ya dunia ya WHO.

Idadi ya jumla ya mataifa yaliyo na mikakati hiyo, ambayo ni 38, inalaezwa kuwa bado ndogo sana na kuongeza kuwa serikali zinahitaji kujifunga kuanzisha mikakati hiyo.

Kujiua kulishika nafasi ya pili katika vyanzo vya kusababisha vifo vingi miongoni mwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-29, baada ya majeraha yanayotokana na ajali za barabarani.

Mbinu zinazotumiwa zaidi katika kujiua ni pamoja na kujinyonga na kujipiga risasi, hususani katika maeneo ya vijini, kunywa dawa za sumu za kuulia wadudu.

Ripoti inabainisha kuwa, mauaji zaidi yanatokea katika mataifa maskini na yenye maendeleo ya kati, ambako idadi kubwa ya watu duniani wanaishi, pia viwango ni vikubwa zaidi katika mataifa tajiri.

Baada ya Guyana, Russia inatajwa kuwa ya pili kwa idadi kubwa ya watu wanaojiua. Mataifa mengine yaliyoko kwenye orodha hiyo ni pamoja na Lithuania, Lesotho, Uganda, Sri Lanka, Korea Kusini, India, Japan na Marekani.

Katika nchi nyingi, wanaume wana uwezekano mkubwa zaidi wa kujiua kuliko wanawake. Ni katika mataifa matano tu ya Bangladesh, China, Lesotho, Morocco na Myanmar, ambako wanawake zaidi wanajiua kuliko wanaume.

**DW**

AFYA



Jengo la wodi mpya ya kinamama na watoto, katika Hospitali ya Wilaya Nachingwea. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA.**

MAGEUZI NACHINGWEA MPYA

# Wodi mpya inayolamba Sh. mil 400 DC akilia na mabusha, ukosefu vyoo

- Sep 30 kicheko kinamama, watoto
- RC: Naagiza wanavijiji mbadilike
- Mrisho Mpoto kuendesha kampeni

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa Nachingwea**

KATIKA kuhakikisha changamoto za afya zinaendelea kupatiwa ufumbuzi Wilaya ya Nachingwea, inayoendelea na ujenzi wa jengo la wodi ya mama na mtoto baada ya kupokea Sh. milioni 400 kutoka serikali kuu.

Jengo hilo litakapokamilika, linatarajiwa kuwa na chumba cha upasuaji, sehemu ya akina mama kusubiria kabla ya kujifungua, sehemu ya kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum na vyumba vingine muhimu.

Hatua ya serikali kutoa kiasi hicho cha fedha inaelezwa na mkuu wa wilaya hiyo, Rukia Muwango kuwa inalenga kuboresha huduma ya afya kwa mama na mtoto wilayani Nachingwea.

"Serikali kuu imetuongezea kasi ya kuboresha huduma ya afya wilayani kwetu, hivyo sisi viongozi hatuna budi kusimamia ujenzi wa wodi na kuhakikisha unakamilika, kisha kuanza kutumika," anasema Muwango.

Mkuu huyo wa wilaya anasema, lengo la ujenzi ni kuhakikisha wananchi Nachingwea wanapata huduma kwenye mazingira bora na rafiki.

**JENGO LIMEKAMILIKA**

Msimamizi wa ujenzi wa jengo hilo, Mhandisi Khalifa Kimbendera, anasema ni mradi unaotarajiwa kukamilika tarehe 30 ya mwezi huu, iwapo ratiba itaenda kama walivyopanga. Ni ujenzi ulioanza Aprili mwaka huu na unaendelea vizuri, matarajio yaliyopo ni kukabidhi mradi kupisha hatua nyingine.

"Suala la kutumika siyo la kwangu, kwani hii inategemea kama vifaa vya kutolea huduma vitakuwepo, lakini suala la ujenzi ni kwamba tumepanga kukamilisha Septemba 30," anasema mhandisi huyo wa halmashauri.

Anafafanua kuwa, katika nafasi yake ya uhandisi anasimamia ujenzi tu na suala la kuanza kutumika, ni hatua iliyoko kwenye mamlaka nyingine, akidokeza inategemea la uwekaji wa vifaa vya kutoa huduma mbalimbali, hasa za mama na mtoto.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango.

**ZAHANATI ZILIZOPO**

Kuhusu ujenzi wa zahanati, mkuu wa wilaya anasema kwa muda mrefu umekuwa ukiendelea katika vijiji mbalimbali vya Nachingwea, ikiwamo vituo vya afya na lengo ni kusogeza huduma za afya karibu na wananchi waliko.

Rukia anasema, hadi sasa wilaya ina jumla ya zahanati 39 na vituo vitatu vya afya, ambavyo vipo kata za Kilimarondo, Nambambo na Ruponda, huku juhudi zikiendelea kujenga kituo cha afya.

"Nachingwea ina kata 36, lakini ina zanahati 39, kwa hiyo tumevuka malengo ya ujenzi wa zahanati kwa kila kijiji na sasa tunaelekeza nguvu katika kujenga vituo vya afya na wodi ya mama na mtoto," anasema.

Anasema, mbali na ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, wameanza kupunguza kero ya maji kwa kuchimba visima 150 kwenye maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo kongwe.

"Maji nayo ni afya, watu wakinywa yasiyo salama wanakuwa katika hatari, ndio maana huku kwetu kuna kampuni ya Gain inaendelea kuchimba visima virefu vya maji, lengo ni kupata maji safi na salama," anasema.

Mama Rukia, anasema kwa muda mrefu wananchi wamekuwa wakilalamika kwamba wanatembea umbali mrefu kufuata maji na kujikuta wakipoteza muda, hivyo hatua ya kuchimba visima ni mkombozi kwao.

Anasema, uhaba wa maji safi na salama ni tatizo ambalo yeye na viongozi wenzake wanaendelea kulitafutia suluhisho ili kuhakikisha vijiji vyote vinapata huduma hiyo muhimu, tena maeneo ya karibu.

**KILIO CHA MABUSHA**

Mkuu wa wilaya anasema, mabusha na tezi dume ni magonjwa yanayowasumbua wakazi wa wilaya yake, hususan wanaume, akitoa takwimu, kwamba mwezi Julai mwaka huu, jumla ya watu 150 walifanyiwa upasuaji wa mabusha na wengine waligundulika kuwa na tezi dume.

Anasema matibabu hayo yalitolewa bure na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ili kuwasaidia wakazi wa Nachingwea, ambao ni sehemu ya wakazi wa mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani, wanaosumbuliwa na maradhi hayo.

"Kabla ya upasuaji, madaktari walikuwa wanawapima afya zao, lakini wengi wao walibainika kuwa na magonjwa hayo mawili wakawaacha. Kwa maelezo ya kitaalam ni kwamba, mwenye tezi dume hawezi kupasuliwa busha," anasema.

Rukia anasema tatizo la tezi dume na mabusha ni kubwa na kwa sasa anahangaika kutafuta wadau mbalimbali wamsaaidie kufanikisha kampeni ya kutokomeza magonjwa hayo mawili.

"Nilisimamia kampeni ya upasuaji wa mabusha, sasa sina budi kusimamia hata hilo la ugonjwa wa tezi dume, kwani tatizo hili ni kubwa sana huku kwetu, hivyo ndivyo madaktari walibaini," anasema.

**VYOO TATIZO**

Akizungumza mjini hapa hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, anasema wilayani Nachingwea kuna watu wengi wasio na vyoo bora, hivyo anaagiza kila mkazi asiye na choo bora ahakikishe anakiboresha haraka iwezekavyo.

Huku akiwanyooshea kidole kinababa ambao ndio vichwa vya nyumba kwa kauli; "Haiwezekani mtu anajiita mwanaume, wakati nyumbani hana choo au ana choo kibovu, ambacho wakati wowote kinaweza kuhatarisha maisha kwa uzembe wake mwenyewe

"Kumbukeni nyumba ni choo na kuna kampeni zimekuwa zinaendelea zinazohusiana na ujenzi wa vyoo bora, lakini inashangaza nyie bado mko nyuma katika ujenzi wa vyoo hata hapa mjini."

Agizo lake wakazi wa Nachingwea wabadilike kuwa watu wa kisasa wanaoenda na wakati kwa kulinda afya zao, badala ya kuridhika na maisha walio nayo kila siku, huku bila ya vyoo bora.

Katika hilo, Mkuu Wilaya Rukia, anasema tatizo hilo na vyoo bora vipo kwa kiwango asilimia 56, akitoa sababu baadhi ya watu ni wagumu kuelewa umuhimu wa vyoo bora.

"Wito wangu ni kwamba choo ni ustaarabu, pia ni afya na ni muhimu kukitumia. Kwa hiyo, kila mmoja wetu awe na choo bora na kukitumia kikamilifu kwa afya yake," anasema.

Katika kufanikisha ujenzi wa vyoo bora, ana mpango wa kumwita Balozi wa Kampeni ya 'Nyumba ni Choo' msanii Mrisho Mpoto, afike Nachingwea kwa ajili ya kuendesha kampeni ya kujenga vyoo bora.

Mkuu wa Wilaya, naamini kwamba ni hatua inayoweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kuwabadilisha wakazi wa Nachingwea na hatimaye wakajenga vyoo vinavyotakiwa kwa ajili ya afya bora.

AFYA

MAGEUZI NACHINGWEA MPYA

# RC Zambi, DC Rukia waangukia kauli ‘tumezichoka mimba shuleni’

- Miezi 8 mimba100, nusu iko Nachingwea
- Mabinti wa sekondari, msingi wachuana

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa Nachingwea**

MIMBA kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari bado ni tatizo kubwa mkoani Lindi. Si msamiati mpya hata kidogo. Ni malalamiko yanayochukua sura ya kero na mateso.

Ni kwa kipindi cha miezi nane, kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu, jumla ya wanafunzi 100 wamepewa ujauzito, hata kugeuka kero kubwa kwa Mkuu wa Mkoa, Godfrey Zambi, anayekuwa ‘mbogo’kufikia hatua ya kuwaagiza wakuu wa wilaya na wasaidizi wote kuhakikisha inachukuliwa hatua kali kumlinda binti.

Hapo kinachosimamiwa zaidi, Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na marekebisho yake ya mwaka 1995 na 2002, inayomnyima haki kuendelea na masomo. Ni mwanzo wa safari nyingine inayomuondoa katika ndoto ya kwanza ya mategemeo na kudumbukia katika katika ndoto nyingine ya kukata tamaa.

Zambi, aliyewahi kuwa mbunge wa Mbozi, anataja sababu za mimba hizo ni wazazi kuwapa watoto wao uhuru kupita kiasi na wengine kukubali ‘kumalizana’ na wanaowapa watoto mimba, kwa mabadilishano ya ‘chochote.’

Mkuu huyo wa mkoa, anatoa mfano wa mwanafunzi wa darasa la tatu wilayani Kilwa, aliyepata mimba huku babu yake akisaidia kumtafutia wanaume, jambo analolieleza kwamba ni kero kubwa, hatua ambayo sheria inapaswa ichukue mkondo wake.

“Inasikitisha kuona serikali ikikazania watoto wa kike kupata elimu, kuna watu wanaendelea kuwapa mimba na kukatisha ndoto zao, huku baadhi ya wazazi wanashiriki kuficha wahusika wa mimba hizo,” anasema Zambi.

Anasema suala ya jando na unyago, lina mchango mkubwa akisisitiza kwamba hazuii sherehe za mila na desturi, lakini angalizo lake ni kwamba nazo zisiingilie masomo ya watoto.

“Marufuku kupeleka watoto katika jando na unyago wakati shule zinaendelea na masomo,” anasema na kuongeza: “Sizuii mila na desturi zenu, bali ninachotaka ni kuwatoa watoto shuleni na kuwapeleka kwenye mambo hayo.”

Anawataja pia walimu kwamba wanahusika katika mimba hizo, ama kuwatisha wanafunzi au kuwadanganya kwa ahadi ya kuwasaidia katika masomo, kumbe lengo ni kuwaharibia na mwisho wa safari wanawakimbia.

“Mkoa wa Lindi kuna zaidi ya walimu kumi wamewapa mimba wanafunzi na kukimbia vituo vyao vya kazi na hadi sasa hawajulikani walipo, lakini vyombo vya dola vinaendelea kuwatafuta,” anasema. Zambi, pia anawataja madereva wa bodaboda kuwa wahusika wakubwa wa tatizo la mimba. Hapo nako anawaagiza wakuu wote wa wilaya na watendaji, kuhakikisha mimba hizo zinakoma ndani ya Lindi.

Katika tamko lake hilo kali, kwenye sherehe za hitimisho la kampeni ya ‘Wiki ya Elimu ya Mlipa Kodi na Tozo za Serikali’ wilayani Nachingwea, anataja mahali hapo kuna mimba zaidi ya 50 za wanafunzi.

**DC AKIRI TATIZO**

Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango, ambaye alikuwa mwenyeji wa hafla husika, anakiri tatizo na analitolea ufafanuzi kwamba walimu wilayani kwake wanajitahidi kuwadhibiti wanafunzi, lakini wazazi ndio



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi na kulia ni mwenyeji wake, Mkuu wa Wilaya, Rukia Muwango, mjini Nachingwea, hivi karibuni katika hafla mojawapo,. **PICHA: SABATO KASIKA.**

> “Tunajitahidi kukabiliana nao, kwani kweli kuna changamoto nyingi, zikiwamo baadhi ya wazazi kuwasimamisha masomo watoto wao wakati wa msimu wa mavuno ya korosho,” anaeleza Rukia.

mzizi wa tatizo.

Anaunga mkono hoja ya mkuu wa mkoa kwenye suala la jando na unyago, kwamba lina sehemu kubwa katika kuchangia mimba, kwa vile watoto wanaotoka kwenye matukio hayo wana hulka ya kujaribu kile walichofundishwa.

“Ndio maana mwaka huu tukaamua kuweka kambi za taaluma kwa shule za msingi na sekondari, ili watoto wa kike wasipate nafasi ya kwenda kwenye mambo hayo ya jando na unyago,” anasema.

Kwa mujibu wa kalenda ya mila iliyoko Nachingwea, kila mwezi Agosti ya mwaka, hufanyika sherehe za jando na unyago, ambayo hutawala hisia za bajeti na imani katika kuifanikisha, watoto wengi wakipiga kambi kwa wiki kadhaa.

Ni aina ya sherehe za kimila zinazotawala imani za wilaya jirani kama vile Ruangwa na Liwale mkoani Lindi, Masasi Mkoa wa Mtwara na Tunduru, Ruvuma, ambako kuna malalamiko ya aina hiyo.

Rukia anafafanua kuwa yeye na viongozi wenzake wanaendelea kujitahidi kutumia njia mbalimbali, kuhakikisha tatizo la mimba wilayani humo linaisha na anawaomba wadau wote wa elimu kuunga mkono juhudi zinazofanyika.

“Tunajitahidi kukabiliana nao, kwani kweli kuna changamoto nyingi, zikiwamo baadhi ya wazazi kuwasimamisha masomo watoto wao wakati wa msimu wa mavuno ya korosho,” anaeleza Rukia.

Anasema katika mazingira hayo ya mavuno ya korosho, kuna baadhi ya wanafunzi wanaangukia katika mimba, kwa sababu ndani ya mazingira ya vijijini, baadhi ya wazazi hawawafuatilii kwa karibuni watoto wao.

“Sisi kwa upande wetu kama serikali tunajitahidi sana kufuatilia tatizo hili, lakini bahati mbaya kuna maeneo huwa tunakosa ushirikiano, hali inayosababisha liendelee kuwapo, lakini tunapambana nalo,” anaeleza mkuu wa wilaya huyo.

Pia, anaungana na mkuu wa mkoa kwenye suala la jando na unyago, kwamba lina sehemu kubwa katika kuchangia kuwapo mimba, kwa vile watoto wanaotoka kwenye matukio hayo anapenda kujaribu kile walichofundishwa.

“Ndio maana mwaka huu, tukaamua kuweka kambi za taaluma kwa shule za msingi na sekondari ili watoto wa kike wasipate nafasi ya kwenda kwenye mambo hayo ya jando na unyago,” anasema.

Anafafanua kuwa yeye na viongozi wenzake wanajitahidi kwa kutumia njia mbalimbali, kuhakikisha tatizo la mimba wilayani humo linaisha na anaomba wadau wote wa elimu kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali.

# Wajadili kwa vipengele dhana ukatili wa mtoto, ushirikiano

- Ushahidi; mfumo maisha; mabinti kazi

NA YASMINE PROTACE

USHIRIKIANO baina ya pande mbili katika jambo lolote, mara nyingi ndio chanzo cha mafanikio kwa lolote. Hivyo upatikanaji haki, usawa na maendeleo, siku zote ndio mzizi wa kuwapo ushirikiano huo.

Mtazamo wa tafakuri hiyo ndio msingi wa kufanikiwa kupatikana haki yake, ikiwamo katika eneo la unyama wa kijinsia.

Hivi karibuni, asasi ya TGNP Mtandao ililijadili hilo, hasa kupata mtazamo sahihi hatua bora kuchukuliwa, binti anapofanyiwa unyama wa kijinsia.

Jamii inaelekezwa kufahamu kuwa mtu anapofanyiwa ukatili, lazima atoe taarifa polisi ili aweze kufanikiwa kupata haki yake.

Katika kulichakata hilo, asasi hiyo jijini Dar es Salaam, iliandaa mkutano uliowashirikisha walimu, maofisa maendeleo jamii na walimu wanaosimamia vilabu vya haki katika maeneo yao.

Jane Dotto, anasema wazazi na walezi mara zote ni chanzo cha kusababisha kesi za kingono kushindwa kuendelea, kwa sababu ya kushindwa kutoa ushirikiano unaostahili katika kufanikisha ushahidi.

Anasema mtoto anapofanyiwa ukatili huo, ni haki yake kufikishwa hospitali kwa ajili ya matibabu zaidi, lakini anatoa angalizo la malalamiko kwamba: "Kumekuwapo tabia ya baadhi ya jamii, mtoto anapofanyiwa ukatili, hatoi ushirikiano kwa polisi. Hali hiyo inachangia kesi kuishia jiani"

Jane anasema kwamba mtoto anapofanyiwa ukatili, anaathirika kisaikolojia, hivyo inastahili kupatiwa haki zake na kusisitiza karatasi ya Polisi inayomruhusu akatibiwe iitwayo PF3' inatolewa bure.

Kwa mujibu wa Jane, ambaye yupo Polisi, Dawati la Jinsia, anawataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawachunguza watoto hasa wakati wa kuoga.

Ofisa Elimu Vielelezo katika Manspaa ya Ilala, Amina Maulidi, anasema mtindo wa maisha nao ni moja ya sababu zinazochangia ukatili wa kijnsia kutokea katika jamii.




Rehema Mwateba, akionyesha namba za simu za kumlinda mtoto dhidi ya matukio ya kingono.. **PICHA : YASMINE PROTACE**

Amina, ambaye pia ni Kamishna wa Skauti Mkoa wa Dar es Salaam, anasema baadhi ya familia za mijini, zina tabia ya kuwaachia majukumu yote mabinti waliowaajiri.

"Unakuta mtu anatoka nyumbani asubuhi, anarudi usiku hajui mtoto kashinda jana asubuhi anaondoka na kurudi usiku. Yeye anakuwa 'bize' kutafuta pesa, lakini suala la mtoto halimhusu," anasema.

Anataja ukatili mwingine anaodai unafanywa na mabiti waajiriwa maarufu kama 'madada wa kazi' mzizi wake ni kwamba hawalipwi kwa wakati.

Pia, Amina anautaja ukatili mwingine umekuwa ukifanywa na ndugu wa karibu hata walimu, jambo analowasilisha maoni kwamba ni vyema kuwapa fursa ya watoto kusikilizwa.

Kamishna huyo wa Skauti, anataja mbinu nyingi za kuwafuatilia watoto ni kujenga utamaduni wa kukagua maeneo mbalimbali ya miili yao.

Mdau wa TGNP Mtandao, Rehema Mwateba, anaeleza sababu ya kukusanya wadau hao, akiwataja waalikwa kuwa makundi mbalimbali, kila moja kwa nafasi yake kutambulisha kampeni yao ya '1_5_5'..

Anawataja kuwa ni walimu wa vilabu vya shule zinazofuatilia mustakabali wa jinsia na watoto, maofisa elimu na wa maendeleo ya jamii, wanaopambana na ukatili wa jinsia, kwamba ni makundi ya wadau akitaka kubadilishana mawazo nao katika vita vya kutokomeza ukatili wa kingono, unaonekana kuongezeka nchini. Rehema anasema, matokeo ya sensa ya mwaka 2012 yanaonyesha watoto wenye umri hadi kufikia miaka 18 ni nusu ya wakazi nchini, hivyo wingi wao ni sababu kamili inayohakikisha misingi imara ya taifa lenye afya njema kimwili, kiakili na kisaikolojia.

Anaongeza kuwa Tanzania imeridhia mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusu ulinzi wa mtoto, ulinzi wa ustawi wa mtoto ukipewa kipaumbele.

Kuna miongozo inayotajwa kuwa pamoja na Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa TGNP Mtandao (MTAKUWWA), 2017/2022.

Rehema anasonga mbali kuwa, kuna tamko la kumlinda mtoto katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977; na Sheria ya Haki ya Mtoto, 2009 na wao wana Mpango Kazi wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto unaolenga kupungua ukatili kwa asilimia 50.

# NUSU WAKAZI MKOA SHINYANGA HAWANA VYOO; MBADALA PORINI, MIFUKO, PAGALA

Inatoka Uk.16

uchafuzi wa mazingira," anasema Malingumu.

"Vyoo bora ambavyo tunataka wananchi wavijenge, ni vile ambavyo vina paa juu, mlango, sakafu chini, kuna maji na sabuni ya kunawia mikono, pamoja na bomba la kupumulia, ili kuondoa harufu chooni," ameongeza.

**Mdau Mwakilishi**

Elisekile Bwile, Mwakilishi wa shirika la maendeleo kutoka Uholanzi (SNV), wanaohusika na miradi ya uboreshaji mazingira, anasema mkoa Shinyanga wanashirikiana kikamilifu na serikali katika kutunza usafi wa mazingira.

Anasema, katika utunzaji usafi huo wa mazingira, wanatekeleza mradi wa Shinyanga Mjini, ambako hakuna mfumo wa kuhifadhi majitaka, vinyesi vinavyonywa vyooni, badala yake hupelekwa kumwagwa porini, hali inayoangukia uchafuzi wa mazingira.

Ushauri wa ofisa huyo, ni kwamba wananchi wa mkoani Shinyanga wanapojenga vyoo vyao waweke mfumo mzuri utakaosaidia onyonyaji wa majitaka, vyoo vitakapojaa vinyesi.





## Kilio vyumba maalum wasichana chasikika

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kujenga vyumba maalum kwenye shule za msingi na sekondari kwa ajili ya watoto wa kike kujisitiri wanapokuwa katika hedhi pamoja na kuboresha miundombinu ya maji.

Walitoa ombi hilo jana kwa nyakati tofauti, huku wakisema serikali imejikita zaidi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo na kusahau kujenga vyumba maalum kwa ajili ya kujisitiri mtoto wa kike hali ambayo imechangia utoro shuleni.

Mmoja wa wananchi kutoka Kata ya Maendeleo, Bupe Mwaihojo, alisema kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa vyumba maalum vya watoto wa kike kujisitiri wanapokuwa hedhi kwenye shule za sekondari katika wilaya hiyo. Alisema matokeo ya changamoto hiyo yamesababisha utoro kwa watoto kwa kuwa hulazimika kuvunja vipindi vya darasani kwenda nyumbani ili kujisitiri.

Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya, Shirley Swai, alisema wanaendelea kuhamasisha ujenzi wa vyumba maalum vya watoto wa kike kujisitiri kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (Unicef).

Alisema shule ambazo zinaendelea na ujenzi wa vyoo wahakikishe kuna chumba kwa ajili ya watoto wa kike na kuwaomba wananchi kuendelea na ujenzi kwenye maeneo ambayo serikali haijatenga fedha ili kumsaidia mtoto huyo.

Mhandisi wa Maji wilayani humo, Vivian Mndolwa, alisema asilimia 47 ya wananchi hawapati huduma ya majisafi na salama na kwamba vijiji 13 tayari viko kwenye mpango wa kupatiwa huduma hiyo.

Mndolwa alisema miongoni mwa maeneo yatakayopewa kipaumbele ni kwenye shule za msingi na sekondari hususani kwenye vyumba vya kujisitiri watoto wa kike.

Alisema serikali inaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya maji katika eneo la Ilota ambapo kiasi cha Sh. milioni 700 zimetengwa.

"Tunaendelea kusisitiza wananchi kuendelea kutunza miundombinu ya maji. Kumekuwa na uharibifu mkubwa kwenye vyanzo hali inayosababisha watu wengine kukosa huduma hiyo," alisema.

# Wapata mafunzo uzalishaji vyakula

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA 825 kutoka Kata za Inyala, Itewe na Utengule Usongwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji wa vyakula vyenye virutubisho vya mboga na matunda kwenye skimu za umwagiliaji ili kuimarisha afya ya mama na mtoto.

Akizungumza juzi, Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Damas Massawe, alisema lengo ya kutoa mafunzo hayo ni kuongeza uzalishaji wa virutubisho ambavyo vitasaidia kuondoa udumavu kwa watoto.

Massawe alisema idara yake katika utekelezaji wa shughuli za lishe kipindi cha robo ya kwanza ya Julai hadi Septemba 2018/19 imesimamia uzalishaji wa vyakula vyenye virutubisho ili kuimarisha afya ya mama na mtoto.

**Katika kuongeza uzalishaji idara hiyo ilitumia maofisa ugani kutoka ngazi za vijiji na kata kutoa elimu kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile Feed the Future.**

Alisema katika kuongeza uzalishaji idara hiyo ilitumia maofisa ugani kutoka ngazi za vijiji na kata kutoa elimu kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile Feed the Future.

"Tulibaini baadhi ya sababu ambazo zinachangia udumavu kwa watoto kuwa ni kukosa viini lishe kutoka kwenye matunda na mboga, hivyo idara ya kilimo katika kupunguza tatizo hilo, tuliandaa mafunzo kwa wakulima kujua namna ya kuongeza virutubisho kwa watoto hao," alisema Massawe.

Alisema katika kukabiliana na udumavu kwa watoto, idara hiyo inakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa vitendea kazi kama vile pikipiki kwa maofisa kilimo kwenye kata na vijiji pamoja na ubovu wa gari la idara hali inayosababiha kutofanya kazi kwa ufanisi.

Alisema idara imejipanga kuongeza jitihada za kuwezesha uzalishaji wenye tija kwenye kilimo cha mboga na matunda kwa kuwa ndicho chenye vyakula muhimu vya lishe kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta zisizo za kiserikali zilizoko ndani ya halmashauri hiyo.

Mmoja wa wanufaika hao, Mbukwa Mwasandube, kutoka kata ya Ijombe, alisema sababu iliyochangia udumavu kwa watoto ni mtindo wa maisha kutokana na wazazi kuwa na shughuli nyingi za uzalishaji na ujasiriamali na kusahau wajibu wao kwa watoto.

Alisema ili kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto, serikali kwa kushirikiana na taasisi zingine inapaswa kutoa elimu ya umuhimu wa malezi kwa watoto hasa kwenye lishe.

"Serikali kupitia idara mbalimbali imejitahidi kutoa elimu ya wazazi na walezi kuzingatia milo kamili na kuzalisha vyakula vyenye virutubisho, lakini wamesahau elimu ya malezi kwa watoto," alisema Mwasandube.



Wachuuzi wakiwa wamepanga bidhaa zao katika mazingira hatarishi kiafya kutokana na matope mengi yaliyowazingira katika eneo la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waafikiana kuanzisha mnada wa mahindi

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

WADAU wa Kilimo katika Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe wamekubaliana kuanzisha mnada wa pamoja ambao utatumika kuuzia mazao yao hususan mahindi ambayo soko lake si la uhakika.

Makubaliano hayo yaliafikiwa hivi karibuni wilayani humo wakati wa kikao cha kujadili changamoto ya masoko kwenye zao hilo.

Baadhi ya wadau wa kilimo walisema ili mzalishaji anufaike lazima kuanzisha mnada ambao utawakusanya wakulima wa kutoka maeneo mbalimbali.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), mkoani Songwe, Charles Chenza, alisema ni wakati mwafaka wa kumsaidia mkulima ili anufaike kwa kuhakikisha anatengenezewa mazingira rafiki ya kuuzia mazao yake.

Chenza alisema kuwapo kwa mnada wa pamoja kutawasaidia wakulima kuuza mazao kwa bei ya pamoja na kuiomba serikali kusimamia suala hilo ili kuwazuia madalali ambao huwanyonya wakulima.

Aliitaka serikali kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko pamoja na Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuwa wateja wakubwa kwenye minada hiyo ambayo alishauri kuwekwa kwenye maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo ili kuwasaidia pia wakulima wanaookaa kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

"Tukiweka minada kwa kila kata katika wilaya hii hakika tutakuwa tumewasaidia sana wakulima kunufaika na kilimo cha mahindi kwani watauza mazao yao kwa pamoja na kwa bei waliyokubaliana. Tuzidi kuiomba serikali kupitia NFRA kununua kwa wingi mazao yetu," alisema Chenza.

Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Wilaya ya Mbozi, Richard Sirili, alisema ili kupata wateja wa uhakika na kuuza mazao yao bila shida ni muhimu wakulima kuzingatia kilimo cha kisasa ambacho kinazingatia mbegu bora, kulima kwa wakati na kufuata ushauri wa maofisa kilimo.

Diwani wa Idiwili, Christopher Ntandala, aliishauri serikali kuanzisha kituo kikubwa cha ununuzi wa zao hilo (one stop centre) ambacho kitakuwa kinakusanya mahindi ya wakulima wote wa Mbozi na kuuza kwa pamoja.

Alisema kituo hicho kitakuwa chini ya serikali na kitakuwa na jukumu la kukagua ubora na kutafuta soko la uhakika na kwamba wakati wa kuuza na kununua kuwe na utaratibu wa upashanaji habari.

Mkulima Julius Mwampashe, kwa upande wake aliitaka serikali kurejesha mfumo wa zamani wa ugawaji mbolea za ruzuku, kwa madai kuwa mabadaliko ya sasa yanamkandamiza mkulima kutokana na kuwapo kwa mawakala wasiozingatia bei elekezi.



HABARI DODOMA

# Wenye ulemavu wataka usajili magari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Kamati ya Taifa ya Usalama Barabarani kwa Watu wenye Ulemavu, Jutoram Kabatele, amesema wamepeleka mapendekezo kwa serikali kuanzisha utaratibu wa vyombo vya moto vinavyoendeshwa na watu wenye ulemavu kuwa na namba tofauti za usajili.

Kabatele aliyasema hayo jana wakati wa utoaji wa elimu kwa wakazi wa Jiji la Dodoma kuhusu alama sita mpya maalumu za usalama barabarani za kuwalinda makundi ya watu wenye ulemavu. Alisema katika alama hizo sita za usalama barabarani, moja ni kwa ajili ya utambuzi wa vyombo vya moto vinaendeshwa na watu wa kundi hilo.

Kabatale alisema pamoja na kubuni alama hizo ambazo zitawasaidia watu wenye ulemavu katika kuwalinda na ajali, iko haja vyombo vya moto vinavyoendeshwa na watu wenye ulemavu kuwa na namba tofauti na zile za kawaida.

**Sheria na sera za walemavu zinaeleza wazi kuwa watu wenye ulemavu wanatakiwa kupata huduma za usafiri katika mazingira ya usalama.**

"Tumeshapeleka mapendekezo yetu serikali na sasa tunazungumza na watu wa TRA kuwa ni lazima sisi tuwe na namba tofauti na watu wengine wa kawaida. Inaweza kuwa hata WT AZT 801, ikimaanisha 'Walemavu Tanzania'. Hili suala ni la kisheria si kama tunaomba hisani," alisema Kabatele.

Akizungumza kuhusu alama tano kwa ajili ya kuwalinda watu wenye ulemavu barabarani, alisema amezibuni ili kuwasaidia watu wa kundi hilo kuepukana na changamoto ambazo wamekuwa wakizipata maeneo mbalimbali nchini.

"Kama leo hii mnyama anazo alama zake barabarani kwa nini mimi mlemavu nikose. Alama hizi zitawasaidia makundi ya watu wenye ulemavu wa viungo, wenye ualbino, viziwi, walemavu wa akili pamoja na wenye ulemavu wa macho," alisema.

Pia alisema sheria na sera za walemavu zinaeleza wazi kuwa watu wenye ulemavu wanatakiwa kupata huduma za usafiri katika mazingira ya usalama.

"Mlemavu anatakiwa anaposafiri asipate usumbufu wowote kwa mujibu wa sheria yetu, lakini hivi sasa ukienda katika vituo vya mabasi unakutana na changamoto nyingine ikiwamo mabasi kuwa na ngazi ndefu, lakini wakati watu wanapokwenda kuchimba dawa mimi kama mlemavu siwezi kwenda nabaki ndani ya basi kama mlinzi," alisema.

Aidha, alisema mafunzo hayo ya alama sita mpya za usalama barabarani kwa watu wenye ulemavu yatatolewa katika mikoa ya Dar es Saalam, Dodoma na visiwani Zanzibar, kwa ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la The Foundation For Civil Society (FCS).




Mwenyekiti wa usalama barabarani kwa watu wenye ulemavu na mbunifu wa alama hizo, Jetoram Mahala, akitoa elimu ya usalama barabarani kwa wakazi wa Jiji la Dodoma (hawapo pichani), jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Utamaduni sasa kuvutia watalii

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka Watanzania kutumia rasilimali ya urithi wa utamaduni walio nao kama bidhaa katika soko la utalii nchini.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Tamasha la Urithi, Profesa Martine Mhando, wakati akizungumza kuhusiana na tamasha hilo ambalo litatanguliwa na lile la 'Jamafest' linalotarajia kufanyika mwezi mzima kutangaza vivutio vya utalii.

Prof. Mhando alisema utekelezaji wa tamasha la urithi utafungua ukurasa mpya katika kuongeza wigo wa mazao ya utali, hivyo ni vyema jamii ikatumia nafasi hiyo kwenda kuonyesha bidhaa za asili walizo nazo.

Alisema tamasha la urithi linapaswa kuwa na tija kwa jamii kutokana na kujumuisha wadau kutoka sehemu mbalimbali ambao wataona utalii uliopo ndani ya nchi katika mikoa ambayo tamasha litafanyika kwa lengo la kutangaza utalii uliopo ndani ya mkoa husika.

Mwenyekiti huyo alisema kwa kuzingatia wingi na ubora wa vivutio vya utalii, watalii wa kigeni wanaotembelea nchini wamefikia milioni 1.5 na kuna uwezekano wakaongezeka iwapo jitihada za kila mkoa zitafanyika kutangaza utalii katika eneo husika.

Alisema ni vyema jamii ikatumia fursa ya tamasha la urithi na lile la Jamafest kupanua wigo wa kutangaza bidhaa zilizopo jambo ambalo itasaidia kuongeza idadi ya watalii kutembelea nchini.

Prof. Mhando alisema sekta ya utalii ni kichocheo cha kukua kwa sekta zingine za uchumi hususani uchukuzi, viwanda na biashara, kilimo, kazi za ufundi wa mikono ambazo huchangia katika kuongeza ajira.

Aliongeza kuwa pamoja na Tanzania kuwa na vivutio vingi vya urithi vya kitamaduni, utalii unapaswa kupewa kipaumbele cha kuendelezwa na kutangazwa vya kutosha ili kushawishi watalii kuja kuangalia uwekezaji katika vivutio vilivyopo.

# Asilimia 65 vijana wanufaika mafunzo ya ajira

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASILIMIA 65 ya vijana jijini Dodoma wamenufaika na mafunzo ya mpango wa 'Jiandalie Ajira' yanayoendeshwa na Taasisi ya Ujasiriamali na Ushindani Tanzania (TECC) ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri pindi wanapohitimu elimu.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa Fedha wa TECC, Godwin Lemunga, katika ufunguzi wa mafunzo ya saba ya kujengeana uwezo katika mambo mbalimbali ya ujasiriamali.

Lemunga alisema vijana wengi wa kike na wa kiume wamenufaika na mafunzo yanayotolewa na TECC ambayo yamewasaidia wengi kwenda kujiajiri kupitia biashara mbalimbali wanazofanya kikiwamo kilimo cha mboga na ufugaji wa samaki.

"Vijana wengi wamenufaika na mafunzo kupitia mradi huu unaoendeshwa chini ya Taasisi ya Vijana ya Marekani (IYF)," alisema Lemunga.

Alisema lengo kubwa ni kuwafundisha vijana ujasiriamali na stadi za maisha ambazo wengi wanashindwa kuzijua kutokana na kutopata elimu ya ujasiriamali.

Lemunge alisema baada ya vijana kuhitimu mafunzo hayo TECC, imekuwa ikiwasimamia katika kuwaunganisha na taasisi zinazotoa mikopo ili wapate mtaji kwa ajili ya kuendesha shughuli za ujasiriamali.

Alitoa wito kwa vijana wa jijini hapa kuhakikisha wanajitokeza katika mafunzo ambayo yanawapa faida kubwa hapo baadaye.

Kuhusu mafunzo ya awamu ya saba yanayoendelea jijini hapa alisema washiriki 30 wamejitokeza kushiriki kwa ajili ya elimu ya ujasiriamali ambayo ni muhimu kwa jamii.

Alisema mafunzo hayo ya mwezi mmoja yanawasaidia kwa kiasi kikubwa kupata elimu juu ya ujasiriamali wanaokwenda kufanya baada ya mafunzo hayo kufikia ukingoni.

Naye mshiriki Emila Sulle, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa vijana kwa sababu yanawasaidia kuongeza ujuzi wa mambo mbalimbali ya ujasiriamali ambao wanafanya.

"Mafunzo haya yamenisaidia sana hivi sasa ninaendesha kilimo cha mboga na ufugaji samaki kwenye bwawa eneo la Nanenane," alisema Sule.





# Shein aupongeza ushirikiano na China

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameipongeza China kwa kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha maendeleo ikiwamo kuipatia wataalamu kwa ajili ya kuwafunza Wazanzibari.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alisema hayo Ikulu mjini Zanzibar wakati alipokutana na kuzungumza na Katibu wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) Dong Weihong, ambaye ni Makamu Mkuu wa Taasisi ya China National Research Institute of Food Fermentation Industries ya China.

Katika mazungumzo hayo, Rais Dk. Shein alisema kuwa Jamhuri ya Watu wa China na Zanzibar zina historia ya muda mrefu katika kushirikiana.

**Tanzania Bara na Zanzibar zinafurahishwa na juhudi za nchi hiyo za kuendeleza uhusiano na ushirikiano wa kufikia maendeleo.**

Alisema China inaleta wataalamu na wakufunzi wake Zanzibar katika sekta mbalimbali zikiwamo afya, kilimo, viwanda na elimu.

Aidha, Dk. Shein alieleza kuwa Tanzania Bara na Zanzibar zinafurahishwa na juhudi za nchi hiyo za kuendeleza uhusiano na ushirikiano wa kufikia maendeleo.

Alisema kuwa juhudi hizo zina manufaa makubwa kwa sasa na baadaye kwani ni kivutio kimoja wapo cha kupanua wigo wa masuala ya kuvutia watalii.

"Ni jambo la kufurahisha sana kwani Jamhuri ya Watu wa China walianza kutusaidia kwa kutuletea wataalamu wa afya, kilimo, viwanda, elimu, lakini leo inatuletea waatalamu wa mapishi na ukarimu kwa kweli ni jambo la kupongezwa sana," alisema Dk. Shein.

Aidha, Dk. Shein alisema kuwa kufanyika mafunzo hayo Zanzibar kunatoa nafuu ya gharama za uendeshaji na utoaji nafasi kubwa zaidi kwa watendaji watakaopata fursa ya mafunzo hayo.

Pia, alieleza kuwa mafunzo hayo yataimarisha uhusiano na ushirikiano katika kuimarisha sekta ya elimu na utalii Zanzibar kwa kupitia Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kilichopo Maruhubi ambacho hivi sasa kimeunganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Balozi mdogo wa China, Xie Xiaowu, alisema kuwa Jamhuri ya Watu wa China inathamini uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya Zanzibar na kuahidi kuendelea kutoa nafasi za masomo nchini humo sambamba na kuleta wakufunzi kuja kuwafundisha Wazanzibari.

Balozi Xie Xiaowu alisema kuwa urafiki wa Jamahuri ya Watu wa China na Zanzibar ni wa miaka 55 hadi hivi sasa, hivyo unaonyesha wazi kuwa una historia kubwa na kuna kila sababu ya kuendelezwa na kudumishwa kwa nguvu zote.

Kwa upande wake Katibu wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) na Makamu Mkuu wa Taasisi ya 'China National Research Institute of Food Fermentation Industries' kutoka China Dong Weinhong alimpongeza Dk. Shein kwa juhudi zake za kuhakikisha mafunzo hayo yanafanyika.

Kiongozi huyo alieleza kuwa juhudi hizo za Rais Dk. Shein ni lazima ziungwe mkono kwani zinaonyesha wazi kuwa ana hamu na nia ya kuwasaidia wananchi wake katika sekta zote za maendeleo na kuahidi kuwa taasisi hiyo itasimama bega kwa bega na yeye.

Aliongeza kuwa hatua hiyo inazidi kujenga uhusiano na ushirikiano mwema kati ya Jamhuri ya Watu wa China na Zanzibar.

## CCM Z'bar yajinasibu kuhudumia watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi Visiwani Zanzibar, kimetamba kutekeleza ilani yake kwa upande wa watoto ambao imehakikishia haki zao za msingi yakiwamo malezi bora, huduma za afya, elimu na kulindwa maisha yao.

Hayo yalisema na Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu (NEC), Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Catherine Peter Nao.

Nao alikuwa katika ziara yake ya kumtembelea mtoto Hajra Abdillahi Abdalla, aliyeokotwa na mbwa ikidaiwa kuwa mama yake baada ya kujifungua alimtupa msituni huko Pemba miezi kadhaa iliyopita.

Mtoto huyo kwa sasa analelewa katika kituo cha watoto cha Mazizini Unguja. Alisema CCM imeweka sera bora na rafiki za kulinda maisha ya watoto ili wapate huduma muhimu zinazowawezesha kupata mazingira bora ya kimalezi.

Akizungumzia tukio la kutupwa kwa mtoto Hajra alisema vitendo vya aina hiyo vinapingwa vikali na jamii na yeyote atakayebainika achukuliwe hatua kali za kisheria kwani mtoto hana kosa wala hatia.

Alisema mtoto huyo aliyetupwa vichakani mara tu baada ya kuzaliwa kisha akaokotwa na mbwa na kumpeleka sehemu salama za makazi ya watu ni kitendo cha kumshukuru Mwenyezi Mungu. Aliishukru serikali kwa kuchukua hatua za haraka za kulinda maisha yake pamoja na kumpatia huduma bora za kimalezi kama walivyo watoto wengine katika jamii.

Katibu huyo aliwataka walezi wa watoto hao katika nyumba hiyo, na kuwalea katika misingi ya malezi bora hasa ya kidini na kuwajengea mazingira ya kupenda kusoma ili watakapoanza kujitegemea wawe na uwezo wa kujimudu kimaisha.

Aliwasihi watoto hao kujilinda dhidi ya vitendo vya udhalilishwaji kwani kuna baadhi ya watu wanatumia mbinu mbalimbali za kuwaadaa watoto kwa nia ya kuwadhalilisha.



Mafundi wa Wakala wa Barabara (TANROADS) mkoani Shinyanga, wakifunga taa kwenye barabara kuu ya kutoka Tabora kwenda Mwanza, zinazotumia umeme wa jua mkoani humo jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Wakusanya takwimu waelekezwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Fedha Zanzibar imezitaka taasisi zinazoshughulika na ukusanyaji wa takwimu kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kukusanya taarifa hizo.

Naibu Katibu Mkuu, Iddi Hajji, alisema hayo na kueleza kuwa kufanyakazi pamoja ili kufikia malengo ya upatikanaji wa takwimu sahihi kwa umma.

Akifungua warsha ya uimarishaji wa ukusanyaji takwimu Zanzibar, alisema baadhi ya takwimu zinazokusanywa na baadhi ya taasisi zimekuwa si rasmi jambo ambalo linasababisha serikali kushindwa kuzitumia kwa shughuli za maendeleo.

Alisema ofisi ya mtakwimu katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa hizo ni vyema kwa taasisi hizo kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Takwimu ili kuzikusanya kitaalamu na kuziwezesha kukidhi mahitaji ya shughuli za maendeleo ya nchi.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mayasa Mahfoudh Mwinyi, alisema ofisi yake imeanza utaratibu wa kuandaa sera ya Takwimu ya Zanzibar itakayoweka sheria na vigezo vya ukusanyaji wa takwimu.

Alisema baada ya kukamilika kwa sera hiyo itasaidia ukusanyaji wa takwimu zilizosahihi ambazo zitasaidia kuimarisha upatikanaji wa huduma za maendeleo katika sekta mbalimbali.

Alisema Ofisi ya Mtakwimu itaendelea kushirikiana na wadau wa mashirika ya maendeleo katika kuhakikisha sera hiyo inamalizika kwa wakati ili kurahisisha ukusanyaji wa takwimu.

Akizungumza kwa niaba ya wadau wa mashirika ya maendeleo walioshiriki warsha hiyo, Rukiya Wadoud kutoka Mpango wa Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) alisema wataendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha wananchi wananufaika na huduma za maendeleo zinazotokana na ukusanyaji wa takwimu sahihi.

Alisema ili serikali iweze kufikia malengo yake ni lazima ikusanye takwimu sahihi ambazo zitatumika katika huduma za kijamii.

Aidha, alisema wataendelea kushirikiana na serikali hususani katika masuala ya elimu na fedha ili kufanikisha ukusanyaji takwimu kisasa kwa kutumia utaalamu unaotumika katika mataifa mbalimbali.

HABARI KITAIFA

# Jukwaa maalum laundwa kusimamia watumiaji maji

Na Frank Monyo

BODI ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu imeunda jukwaa maalum la watumia maji katika bonde hilo, kwa lengo la kusimamia rasilimali ya maji iliyopo ili kuleta maendeleo endelevu katika jamii hasa katika sekta ya viwanda.

Akizungumza katika uzinduzi wa jukwaa hilo uliofanyika jana, Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali za maji kutoka Wizara ya Maji, Rosemary Rwebugisa, alisema jukwaa hilo litakuwa na kazi ya kujadili hali ya maji katika bonde hilo pamoja na kujadili changamoto na utatuzi wake ili kuendelea kutunza hazina hiyo ya maji kwa kizazi cha sasa na baadaye.

**Jukwaa hili limewahusisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali na wananchi ambao ndio walengwa wakubwa wa rasilimali hiyo...**

"Jukwaa hili limewahusisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali na wananchi ambao ndio walengwa wakubwa wa rasilimali hiyo, tumefanya hivyo kwani ili malengo yaweze kufikiwa lazima wataalamu na wananchi washirikiane ili kuweza kuleta maendeleo endelevu," alisema.

Alisema kuwa wizara itaendelea kushirikiana na sekta na wadau katika kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa na kuhifadhiwa pamoja na mamlaka husika kusimamia matumizi ya maji kulingana na uwepo wake pamoja na kutatua migogoro inayohusu rasilimali hiyo.

Naye Mwenyekiti wa bonde hilo, Hamza Sadick, alisema bonde hilo ni moja kati ya mabonde tisa yanayopatikana Tanzania Bara ni muhimu sana katika kukuza na kuendeleza viwanda na hiyo ni kutokana na maeneo mengi kutegemea maji kutoka bonde hilo.

Alitaja maeneo hayo kuwa ni pamoja na Jiji la Dar es Salaam, Dodoma na miji ya Kibaha na Bagamoyo ambayo imesheheni viwanda ambavyo hutegemea rasilimali maji katika kujiendesha.



Mchuuzi wa dagaa (kushoto), akiwashawishi wateja kununua bidhaa yake pembeni ya barabara katika eneo la Mabibo Sokoni, jijini Dar es Salaam jana. Mfuko mmoja uliuzwa kwa bei ya 1,000/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanahabari wapewa jukumu wanawake kushiriki uongozi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAANDISHI wa habari kisiwani Pemba, wametakiwa kuitumia vyema sauti yao kuielimisha jamii kuhusu ushirikishwaji wa wanawake katika uongozi, ili ilete mabadiliko.

Akizungumza katika mkutano wa waandishi wa habari Mkanjuni Chakechake Pemba, Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar ofisi za Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema mabadiliko yatatokea katika jamii iwapo waandishi watachukua juhudi za makusudi kuelimisha.

Alisema mwanamke ni kiongozi bora anayejitolea zaidi, asiyependa rushwa, anayeheshimu usawa, jinsia na mwadilifu, hivyo ni vyema kwa waandishi kuelimisha jamii kupitia vyombo vyao, ili ifikapo mwaka 2020 wanawake waingie katika uongozi, jambo ambalo litasaidia kuleta mabadiliko ndani ya jamii.

"Nyinyi ni sauti ya wasio na sauti, hivyo iwapo mtaielimisha jamii, itapata uelewa na itamwona kumbe mwanamke na yeye ana haki ya kuwa kiongozi kama mwanamume," alisema mratibu huyo.

Aidha, alisema vyama vya siasa ni wadau muhimu katika kuwahamasisha na kuwatia moyo wanawake kuchukua fomu za kugombea nafasi za uongozi, hivyo ni jukumu lao sasa kuhakikisha wanapata wagombea wanawake bila ya kuwabagua.

"Mwanamke anapokuwa kiongozi anaweza kuleta mabadiliko ya mara moja, pia watajitetea mambo yao yanayowahusu ambayo wanaume hawayatetei," alisema.

Ofisa Uendeshaji kutoka TAMWA-Pemba, Asha Mussa Omar, alisema lengo la kutoa mafunzo kwa waandishi wa habari ni kusaidia na kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa mwanamke kugombea nafasi za uongozi, kwa kuwa inaonekana utetezi wa wanawake ni mdogo sana na kuna mambo yao hayajatetewa, ambayo ni changamoto kubwa inayoikabili jamii.

Akiwasilisha mada ya umuhimu wa vyombo vya habari katika kuibua masuala ya wanawake katika uongozi, Ali Mbarouk Omar, alisema vikwazo vya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni vinavyosababishia mwanamke asigombee nafasi za uongozi na kuwataka waandishi wa habari kuitumia nafasi waliyonayo kuelimisha wananchi, ili wajue haki zao.

# Ndugai kuongoza kuchangia kituo afya

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai (pichani chini), anatarajiwa kuongoza mamia ya wakazi wa Dodoma katika matembezi ya hisani kuchangisha fedha za kutanua na kuboresha Kituo cha cha Afya cha St. Lukes (Mpwapwa).

Matembezi hayo yatafanyika jijini Dodoma Jumamosi kuanzia Uwanja wa Jamhuri asubuhi na kuishia Nyerere Square ambapo Spika ataendesha zoezi la kuchangia.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Tom Mazanda, alisema huu ni uzinduzi wa chagizo ambalo litakuwa endelevu kabla ya kufanyika harambee kubwa jijini Dar es Salaam mwezi ujao ambapo mgeni rasmi atakuwa Rais mstaafu, Jakaya Kikwete.

"Tisheti za ushiriki tayari zimeanza kuuzwa jijini Dodoma kwa shilingi 25,000, ambapo washiriki watatakiwa kuzivaa wakati wa matembezi," alisema na kutoa wito kwa wakazi wa Dodoma kujitokeza kwa wingi ili kufanikisha shughuli hiyo.

Alisema mradi huo utahusisha ujenzi wa wodi ya wanawake na watoto, upanuzi wa maabara, kununua vifaa vya afya na kuongeza watendaji.

Kuhusu wanaochangia kupitia benki, mwenyekiti huyo alisema namba za akaunti ni CRDB-Mpwapwa tawi la St. Lukes Ujenzi A/C-0150507423904 na NMB Mpwapwa tawi la St. Lukes Ujenzi A/C- 50410011146 na kwa wale ambao wangependa kuchangia kwa njia ya simu namba za kutuma mchango ni 0754-363405, 0786-149840 na 0713-014681.

Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa, Dk. Jacob Chimeledya, alitoa wito kwa wakazi wote wa Dodoma wakiwamo wabunge kushiriki vikamilifu ili waweze kutimiza malengo ya matembezi hayo.

"Mradi huu utakuwa na faida kubwa kwa wana Dodoma kwa ujumla na sio wakazi wa Mpwapwa tu. Mahitaji yamekuwa makubwa kwa maana hiyo rasilimali zilizopo hazitoshi kuhudumia mamia ya watu wanaohitaji huduma katika kituo chetu ndio maana tumeamua kufanya mradi huu wa utanuzi," alifafanua.



## HABARI KIMATAIFA

# Mwili wa Mugabe waanza safari kurudi

**HARARE,** Zimbabwe

MWILI wa Rais wa zamani wa Zimbabwe, Robert Mugabe, umeondoka Singapore jana asubuhi kwenda nchini Zimbabwe ambapo atazikwa baada ya maombolezo ya kitaifa, mpwa wake Adam Molai ametangaza.

Mugabe alifariki dunia Septemba 6 akiwa na umri wa miaka 95 nchini Singapore, ambapo alikuwa akihudumiwa kimatibabu kwa miezi zaidi ya mitano.

Mugabe anatarajiwa kuzikwa Jumapili, Septemba 15 baada ya sherehe rasmi ambayo itafanyika Jumamosi.

Hata hivyo familia ya Mugabe haijakubaliana na serikali sehemu ambapo atazikwa kiongozi huyo wa zamani na muasisi wa Zimbabwe.

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa alitangaza maombolezo ya kitaifa na kumpa mtangulizi wake hadhi ya shujaa wa kitaifa, ambayo inampa nafasi kuzikwa katika makaburi ya Mashujaa wa Taifa.

**Katika makaburi hayo ndipo alizikwa mke wa kwanza wa Mugabe, Sally. Eneo ambalo lilijengwa kwa msaada wa Korea Kaskazini.**

Lakini familia ya Mugabe haijapendelea kiongozi wao kuzikwa katika makaburi hayo.

Mwishoni mwa wiki iliyopita mpwa wa Mugabe, Leo Mugabe alisema hajui ni wapi mjomba wake alitaka kuzikwa.

Leo alisema mazishi katika makaburi ya Mashujaa wa Taifa, kama ilivyopangwa kabla ya kuondoshwa madarakani, yatakuwa mazishi rasmi yaliyoandaliwa na aliyemuangusha Mugabe, Emmerson Mnangagwa. Jambo ambalo litaleta shida kwa familia.

Katika makaburi hayo ndipo alizikwa mke wa kwanza wa Mugabe, Sally. Eneo ambalo lilijengwa kwa msaada wa Korea Kaskazini.

Sally alikuwa mmoja wa wanaharakati wa ukombozi wa Zimbabwe, aliyetazamwa na wengi hadi kifo chake kama Mama wa Taifa la Zimbabwe.

Mugabe alizaliwa Februari, 1924, katika familia ya Kikristo ya Katoliki katika eneo la Kutama, Kaskazini Magharibi mwa Jiji kuu la Harare, wakati huo Zimbabwe ikifahamika kama Southern Rhodesia.

Waliomfahamu vema akiwa mtoto, wanasema alipenda sana kusoma vitabu hata wakati alipokuwa anachunga mifugo msituni.

Miaka ya 1960 Mugabe alianza harakati za kupigania nchi yake kuwa huru kutoka mikononi kwa Wazungu wachache kutoka nchini Uingereza waliokuwa wanatawala Zimbabwe.

Harakati zake za kutaka waafrika kujiongoza na kumiliki ardhi, zilisababisha akafungwa jela miaka 10 na serikali ya wakoloni kati ya mwaka 1964 hadi 1974.



Baada ya kuachiliwa huru, Mugabe alikimbilia nchini Msumbiji na kuunda vuguvugu la ZANU- PF na kuanzisha vita vya msituni kupambana na serikali ya kikoloni, wakati huo ikiongozwa na Waziri Mkuu, Ian Smith.

Wakati huo wa mapambano ya msituni, serikali ya Uingereza ilianzisha mchakato wa mazungumzo na vuguvugu hilo, na kupelekea usitishwaji wa mapigano na Uchaguzi ukafanyika mwaka 1980.

ZANU PF kilishinda Uchaguzi huo na Mugabe kuwa Waziri Mkuu wa kwanza mweusi nchini Southern Rhodesia ambayo ilibadilishwa jina na kuitwa Zimbabwe.

Baadaye, wadhifa wa Waziri Mkuu uliondolewa na Mugabe akawa Rais wa nchi hiyo kwa zaidi ya miaka 30 hadi alipolazimishwa kuondoka madarakani na Jeshi Novemba, 2017.

Wengi watamkumbuka Mugabe kama mpiganiaji huru wa Zimbabwe na kiongozi ambaye alipigania umoja wa bara la Afrika na kuwasaidia wananchi wa taifa lake kupata mashamba na elimu.

Hata hivyo, kuna wale watakaomkumbuka kama dikteta, aliyekiuka haki za binadamu na kuminya demokrasia. **RFI**

## Rwanda kuwapokea wakimbizi waliokwama

**KIGALI,** Rwanda

WAKIMBIZI wapatao 500 waliokuwa wamekwama kwenye vituo vya kuhifadhi wakimbizi nchini Libya watahamishiwa Rwanda.

Umoja wa Mataifa (UN) umesema hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za dharura za kuwahamisha wakimbizi hao. Mjumbe maalumu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi, UNHCR katika eneo la Mediterrania ya Kati, Vincent Cochetel alisema wakimbizi 500 watapelekwa nchini Rwanda, kufuatia makubaliano yaliyosainiwa kati ya Rwanda na Umoja wa Afrika (AU).

Conchetel alieleza kuwa kutangazwa kwa mpango huo kwamba, Rwanda huenda ikaongeza idadi kutoka 500, iwapo waturidhika na uendeshwaji wa mpango huo.

Libya kwa muda mrefu imekuwa njia kuu ya waafrika wanaokimbia vita na umasikini kwenye nchi zao na kutorokea Ulaya kutafuta maisha bora, tangu kiongozi wa taifa hilo Muammar Gaddafi alipoondolewa madarakani kufuatia mapinduzi yaliyoungwa mkono na Jumuiya ya Kujihami ya Ulaya, (NATO) mnamo mwaka 2011.

Mjini Geneva, Msemaji wa UNHCR, Babar Baloch akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na makubaliano hayo alisema Kundi la kwanza litatakiwa kuwa na wakimbizi 500, lakini hiyo siyo idadi kamili. Alisema kundi la kwanza lina watu 500 watakaoondolewa Libya na kupelekwa Rwanda.

Alisema chini ya makubaliano hayo, serikali ya Rwanda itapewa, lakini pia itatoa ulinzi kwa wakimbizi na waomba hifadhi ambao hivi sasa wanashikiliwa kwenye vituo huko Libya. **DW**



Raia wa Afrika Kusini akiwa ameshika Panga kwa ajili ya kuwadhuru wageni waliopo nchini humo. **PICHA: REUTERS**

## Nigeria yaondoa raia wake Afrika Kusini

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

RAIA wa Nigeria 640 wamesajiriwa katika ubalozi wa Nigeria uliopo Afrika Kusini tayari kwa kuondoka nchi humo na kurudi kwao.

Kundi la kwanza la raia hao limeshaondoka kufuatia mashambulio dhidi ya raia wa kigeni wanaoishi Afrika Kusini.

Ndege ya Air Peace iliondoka Johannesburg saa 3:00 asubuhi kwa saa za Afrika Kusini na iliwasili mjini Lagos kwa saa za Nigeria. Kulingana na taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Nigeria kwenye ukurasa wake wa twitter ilieleza kuwa raia 313 walichukuliwa kutoka Afrika Kusini katika awamu ya kwanza na waliosalia watasafirishwa kuanzia leo na kesho.

Raia wa Nigeria wanaoishi Afrika Kusini walipewa ofa ya ndege za bure kurejea nyumbani kukwepa vurugu za kibaguzi zinazoendelea Afrika Kusini.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Nigeria ilisema mmiliki wa Shirika la Ndege la Air Peace yupo tayari kuwasafirisha bure wale wote watakaotaka.

"Wote watakaotaka huduma hiyo wanashauriwa kuwasiliana na Ubalozi wa Nigeria jijini Pretoria na ofisi ndogo za ubalozi jijini Johannesburg kwa matayarisho muhimu," taarifa ya wizara ilieleza.

Mashambulizi ya biashara zinazomilikiwa na wageni nchini Afrika Kusini zimepokelewa kwa hasira kali na Wanaigeria ambao wanahisi wanalengwa na kuonewa.

Awali Waziri wa Mambo ya Nje wa Nigeria, Geoffrey Onyeama aliwaambia wanahabari kuwa kulingana na taarifa zilizowafikia, hakuna raia wa Nigeria aliyepoteza uhai kwenye ghasia zinazoendelea.

Hata hivyo, alisema watadai fidia kwa biashara zote za raia wa nchi hiyo zilizoshambuliwa.

Nigeria imesusia kuhudhuria Mkutano wa Kimataifa wa Uchumi unaofanyika Afrika Kusini kutokana na ghasia zinazoendelea. Serikali ya Nigeria tayari iliwaonya raia wake waliopo Afrika Kusini wasisafiri ama kuelekea kwenye maeneo ambayo ghasia hizo zimeshamiri mpaka pale hali itakapotengemaa.

Mashambulizi ya kulipa kisasi kwa kampuni za Afrika Kusini yaliyowekeza Nigeria pia yalifanyika hali iliyoilazimu kampuni kubwa ya mawasiliano ya simu- MTN - kufunga vituo vyake vya biashara kote nchini Nigeria.

Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari alisema kuwa anamtuma mwakilishi wake kwenda Afrika Kusini kueleza ghadhabu zao juu ya vurugu zinazoendelea.

Wiki iliyopita mwandishi na muimbaji wa muziki nchini Nigeria, Tiwa Savage alitangaza kutokwenda kwenye tamasha lililokuwa amepanga kushiriki nchini Afrika Kusini mwezi huu kwa sababu ya ghasia zinazoendelea dhidi ya raia wa kigeni.

Mwanamuziki huyo wa nyota wa mtindo wa Afrobeats alikuwa amepangiwa kufanya onyesho katika jukwaa kuu la tamasha la DSTV Delicious Septemba 21 mjini Johannesburg, mji ambao kumeshuhudiwa ghasia kubwa na uporaji wa maduka mengi yanayomilikiwa na raia wa kigeni kutoka mataifa ya Afrika. **BBC**

# Waziri wa zamani afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa zamani wa Uchukuzi na Mawasiliano kwenye utawala wa awamu ya nne, Omari Nundu (71), amefariki dunia jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Sophia Mtakasimba alisema Nundu alifariki jana mchana alipofikishwa kwaajili ya matibabu hospitalini hapo.

"Alifikishwa hapa mchana lakini ikagundulika kwamba ameshafariki dunia hivyo ndugu waliomleta waliamua kuupeleka mwili kwaajili ya kuuhifadhi katika Hospitali ya Jeshi ya Lugalo," alisema Sophia.

Nundu alikuwa Mwenyekiti wa bodi ya Shirika la Simu Tanzania (TTCL) na aliwahi kuwa Mbunge wa Tanga Mjini (CCM) kati ya mwaka 2010 na 2015.

Nundu alifanikiwa kuwa Mbunge baada ya kumwangusha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Harith Mwapachu kwenye kura za maoni ndani ya CCM kwenye uchaguzi wa mwaka 2010.

Nundu ambaye alizaliwa Agosti 6, 1948 mkoani Tanga, alipata shahada yake ya kwanza ya sayansi katika uhandisi anga chuo Kikuu cha Glasgow mwaka 1975 na baadaye kujiunga na Chuo Kikuu cha Cranfield mwaka 1978 na kuhitimu shahada ya umahiri katika Uhandisi usafiri wa Anga mwaka uliofuata.

Mwanasiasa huyo msomi alitumika katika nafasi mbalimbali za kitaifa na kimataifa ikiwamo Rais wa Tume ya Uvumbuzi wa Anga kuanzia mwaka 2018. Kabla ya hapo alishika nafasi ya makamu wa kwanza wa rais na mjumbe wa bodi katika tume hiyo.

Mwaka 2003 hadi mwaka 2010, Nundu alikuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Ushirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO). Mwaka 2002 alikuwa Mkurugenzi wa Masuala ya Kimataifa katika Mamlaka ya Usafiri wa anga Tanzania (TCAA).

Mwaka 1992 hadi Octoba, 2002 alikuwa Mkuu wa Sekta ya Usafiri wa Anga katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Balozi Mdogo wa China anayefanyia kazi zake Zanzibar, Xie Xiuowu, Ikulu mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Dk. Kilahama kuongoza usimamizi mazingira

**Na Raphael Kibiriti**

MKUTANO Mkuu wa Chama cha Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira Tanzania (WCST), umemchagua Dk. Felician Kilahama kuwa Mwenyekiti mpya wa Baraza la chama hicho.

Baraza hilo litaongoza na kusimamia shughuli za chama kwa kipindi cha miaka miwili ijayo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mwenyekiti anayemaliza muda wake, Katibu Mkuu Kiongozi staafu, Philemon Luhanjo, mkutano huo uliomalizika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, pia uliwachagua Theresia Mashao kuwa Katibu wa Heshima, Anthony Ngai kuwa Kaimu Katibu wa Heshima na Rebecca Sigallah Mtunza Fedha wa Heshima.

Aidha, uliwachagua wajumbe sita kuwa miongoni mwa watakaounda Baraza la chama hicho.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Dk . Kilahama alisisitiza juu ya umuhimu kwa Watanzania kuhifadhi mazingira na kujiepusha na uvunaji ovyo wa misitu.

"Tutambue kuwa wanyama na binadamu wanategemeana, hivyo ni vyema wakaepuka kuharibu mazingira ambayo viumbe huishi...tunapoona misitu, mimea na wanyama, tutambue Mungu aliviumba ili tupate maji, mito isikauke kwa ajili ya uhai wetu, hivyo hatuna budi kuvitunza," alisema Dk. Kilahama ambaye ni Mkurugenzi mstaafu wa misitu Tanzania.

Dk. Kilahama alisisitiza kwamba chama hicho kitaendelea kutoa elimu kwa jamii ili izingatie utunzaji na uhifadhi wa mazingira nchini.

## Auawa kikatili tuhuma za wizi

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

ISSA Hashimu (26), mkazi wa Mtaa wa Matankini Kata ya Nyasa wilayani Masasi mkoani Mtwara, ameuawa kikatili karibu na kituo cha Polisi wilayani Masasi na wananchi wenye hasira kali wakati alipokuwa akikimbilia kituo cha polisi hicho kwa ajili ya kujisalimisha.

Issa mwenye ulemavu wa kusikia, alikuwa anakwenda kusalimisha uhai wake baada ya wananchi hao kumkuta akitaka akiiba vifaa mbalimbali vya umeme wa jua.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Joseph Konyo, alisema tukio hilo lilitokea juzi alfajiri maeneo ya mtaa wa Wapiwapi 'A' karibu na kituo cha Polisi cha Wilaya ya Masasi, Issa alipokuwa akikimbilia kujisalimisha baada ya kuona kundi la wananchi hao wakimkimbiza ili wamkamate.

Alisema aliuawa na wananchi hao baada ya kumkuta akiwa ndani ya duka la mfanyabiashara wa vifaa vya sola, Omari Muhidin.

## AICC yapeleka tuhuma za rushwa Takukuru

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) kimechukua hatua ya kupeleka kwenye vyombo vya uchunguzi husussan Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), tuhuma za rushwa dhidi ya maofisa wake wanaodaiwa kuomba rushwa kutoka kwa mfanyabiashara.

Taarifa iliyotolewa jana na kitengo cha Itifaki na Mahusiano cha AICC kwa Umma, ilimtaja mfanyabiashara huyo kuwa ni Heladius Kanje, ili apunguziwe bei ya kukodi maghala ya kuhifadhi bidhaa yanayomilikiwa na AICC.

Katika habari zilizochapishwa kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii Mkurugenzi wa Kampuni ya Kangaroo Brands Shoe Cream(T) Ltd. ya Arusha, Eladius Kanje, anadai kwamba, maombi yake ya kuomba apunguziwe bei ya kukodi maghala yanayomilikiwa na AICC yalikuwa yakikwamishwa ili atoe rushwa kwa baadhi ya maofisa wa Kurugenzi ya Milki na Miradi ya AICC.

Aidha, Bwana Kanje amedai katika taarifa hiyo kwamba baada ya kukataa kutoa hongo, AICC iliamua kumpandishia kodi tofauti na alichodai kuwa ni "Bei elekezi ya serikali" ya kukodi maghala hayo yaliyopo katika kitalu namba 94A Mtaa wa viwanda Esso, jijini Arusha.

Kutokana na hali hiyo, AICC imesema imeamua kulipeleka suala hili kwenye vyombo vya uchunguzi serikalini ili lifanyiwe kazi na kusisitiza kuwa AICC ni taasisi ya umma inayoendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kanuni za maadili ya utumishi wa umma.

**Taarifa iliyotolewa jana na kitengo cha Itifaki na Mahusiano cha AICC kwa Umma, ilimtaja mfanyabiashara huyo kuwa ni Heladius Kanje, ili apunguziwe bei ya kukodi maghala ya kuhifadhi bidhaa yanayomilikiwa na AICC.**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LENYE NYUMBA NDANI LINAUZWA,** Liko eneo la Lumumba Pangani mkoa wa pwani. Lina ukubwa wa heka mbili. Kwa Mawasiliano 0767332830, 0686137871, 0686807366

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

## KUPOTEA KWA KADI


Ayuibu Mpoki Chifungamilo anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya RAV 4 yenye usajili wa namba T 452 CHC, yenye chasis namba SXA110178451.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/KIJ/RB/290937/2019

115415502

## KUPOTEA KWA CHETI



**Nyakwae Peter Charles** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye index namba P1619-0047 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Victory.

Yoyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/GOG/RB/265639/2019

215415202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

11/09/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMISI tarehe 12/09/2019** kampuni ya **TARIMO REMI STANSLAUS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **NGARAMTONI** kuelekea **LOMSHUKU,** gari hilo lenye namba za usajili: **T155BJM/T916DCG.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 17.50
   Upana –mita 2.76
   Kimo – mita 4.60
3. Njia itakayotumika **NGARAMTONI** hadi **LOMSHURU** kupitia **KIA JUNCTION,MERERANI**, gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115415602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ayuibu Mpoki Chifungamilo** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya RAV 4 yenye usajili wa namba **T 452 CHC,** yenye chasis namba **SXA110178451.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/KIJ/RB/290937/2019**

115415502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAMAKA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 65/2019**

**Ombi la FATUMA BAKARI SALUM**

**Msimamizi wa Mirathi Marehemu BAKARI SALUM LIKELE**

**Kwa yeyote ANAYEHUSIKA TANZANIA - BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 23/9/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamni waweza kukaguliwa. Tarehe 11/9/2019

115415402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI DAR ES SALAAM KISUTU**

**EXECUTION NO. 79/2019**
**(Asilia Madai Na. 31/2015)**

**BONNEY GEORGE MAJILA**
**t/a AIBO LOGISTIC……………………………………MDAI**

**Dhidi ya**

**FREGHT LINK SOLUTIONS………………………MDAIWA**

**KWA: FREGHT LINK SOLUTIONS………POPOTE ULIPO**

## KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo mnahitajiwa/unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 23 Mwezi **SEPTEMBA 2019 SAA 7:00** mchana mbele ya **Mhe. Mhina, SRM.**
**ANGALIA:** Kama hamtahudhuria/hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itaweza kutoa hukumu bila ya uwepo wako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **05** Mwezi **SEPTEMBA,** 2019.

115414702

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WU ZHOU INVESTMENT COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 804 AVK SANLG.** Chassis namba **LBRSPKB50F9003084.** Engine namba **15937425.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **UD/B.I/I/VOL.1852/2019.**

115414202

## KUPOTEA KWA CHETI



**WAITON MWIDUNDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0500/0055** kilichotolewa na WANIKE SEKONDARI mwaka 1994. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBL/S.T/B.I/20/VOL/01/183.**

115414302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi NO; 166/2019.**

**Ombi la STYLOS LEO SIMBAMWENE NA PRISCA LEO SIMBAMWENE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu LEO MSIMBE SIMBAMWENE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/09/2019.

115414402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi NO; 178/2019.**

**Ombi la EXAUTH R.MACHA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SELINA RICHARD MACHA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/09/2019.

115414502

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BOSI PSG KUMWONDOA NEYMAR JANUARI




**PARIS,** Ufaransa

MKURUGENZI wa soka wa Paris Saint Germain anataka Neymar aondoke klabuni hapo haraka inavyowezekana, kwa mujibu wa gazeti la Tuttosport.

Leonardo ameripotiwa kwamba amechoshwa na uvumi unaomzunguka nyota huyo wa Brazil kuhusu majaliwa yake na anataka kumwondoa wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alikubali kubakia kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, hadi kipindi kijacho cha majira ya joto.

Barcelona walikuwa wanapewa nafasi kubwa ya kumsajili kipindi chote cha majira ya joto, huku Neymar mwenyewe alikuwa akitaka kurudi katika klabu yake hiyo ya zamani.

Real Madrid pia walionyesha nia ya kutaka kumsajili na wanaweza wakaanzisha tena mpango wa kumsajili wakati wa dirisha la Januari.

Baba wa Neymar amesema kwamba, makubaliano kati ya PSG na Barcelona yako mbali kukamilika.

Baba huyo aliiambia Fox Sports: "Makubaliano kati ya klabu mbili bado hayajaisha."

# Southgate awaonya wachezaji England

**LONDON,** England

GARETH Southgate amewaonya wachezaji wake kwamba watakabiliwa na wakati mgumu kwenye michuano ya Euro 2020 kama watarudia kucheza kwa kujilinda kama walivyofanya Jumanne dhidi ya Kosovo.

England itafuzu kucheza michuano hiyo kama ikishinda mchezo wake unaofuata dhidi ya Jamhuri ya Czech, Oktoba baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 5-3 dhidi ya Kosovo.

Lakini ushindi huo uligubikwa na makosa ya ulinzi wakati Michael Keane, Declan Rice na Harry Maguire waliposababisha Kosovo kupata mabao matatu na la kwanza wakilipata ndani ya sekunde 35.

Southgate alisema: "Kiukweli makosa ya ulinzi yalisababisha magoli na mwanzo mbaya wa mchezo. Makosa yalikuwa yakawaida. Kuna makosa, tunatakiwa kujirekebisha.

"Wachezaji hawahitaji kuniambia mimi hivyo. Tumeshazungumza kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

"Tulifanya makosa ya kipuuzi, tulifanya maamuzi yasiyo na maana na hatukuwa na uwezo wa kurudi haraka mchezoni.


"Lakini nimevutiwa na muunganiko wa wachezaji walivyocheza na hatimaye kuweza kupata ushindi. Hata hivyo, bado tuna kazi ya ziada ya kufanya kuhakikisha hatuchezi kwa kulinda lango."

Katika mchezo huo, Jadon Sancho alifunga mabao yake mawili ya kwanza kwa kikosi cha England, huku Sterling akifunga moja na kutoa pasi za mwisho tatu.

Nahodha Harry Kane alifunga mabao mawili moja likiwa kwa njia ya mkwaju wa penalti.



# Bruyne: Nikiondoka Man City nitajiunga na Kompany




**MANCHESTER,** England

KEVIN De Bruyne amebainisha kwamba atapenda kujiunga na klabu ya mchezaji mwenzake wa zamani, Vincent Kompany pale Anderlecht wakati atakapoondoka Manchester City.

Kompany alirudi kwenye klabu yake ya utotoni nchini Ubelgiji kwa mkataba wa miaka mitatu kipindi cha majira ya joto baada ya kucheza mechi 360 katika misimu 11 pale City.

Wabelgiji hao wawili walishinda mataji mawili ya Ligi Kuu, moja la FA na matatu ya ligi wakati wakicheza pamoja kwa misimu minne hapo City chini ya kocha, Manuel Pellegrini na Pep Guardiola.

De Bruyne ameliambia gazeti la The Sun: "Natumaini kipindi cha Kompany kucheza pale Anderlecht kitakuwa cha kuvutia kama ilivyokuwa hapa City. Nimemwambia aniwekee nafasi siku moja nikimaliza hapa kucheza pengine baada ya miaka saba ijayo.

De Bruyne, ambaye aliwasili hapo kwenye dimba la Etihad akitokea Wolfsburg mwaka 2015, ameongeza kusema kwamba, Kompany ndiye aliyechangia kwa kiasi kikubwa yeye kushawishika kujiunga na Ligi Kuu ya England miaka minne iliyopita.

"Wakati ule, City walikuwa wanajaribu kunisajili kutoka Wolfsburg na Vincent alikuwa ananisukuma mimi kuhakikisha najiunga naye Manchester," amesema.

# Mkhitaryan: Sikuwa na furaha Arsenal

**MILAN,** Italia

HENRIKH Mkhitaryan amesema alilazimika kuondoka Arsenal ili kupata "presha ya kucheza tena ", baada ya kujiunga na AS Roma kwa mkopo wa muda mrefu kipindi hiki cha majira ya joto.

Alijiunga na washika bunduki hao kutoka Manchester United mwaka 2018, na alifunga mabao nane katika mechi 39 alizowachezea Arsenal.

Raia huyo wa Armenia, ambaye aliifungia nchi yake mabao mawili wakati wa mchezo wa kufuzu kwa michuano ya mataifa ya Ulaya dhidi ya Bosnia Jumapili, alihisi alitakiwa kuondoka England ili kupata nafasi ya kucheza zaidi.

Alisema: "Natakiwa kufurahia kucheza soka, bila kujali ni sehemu gani. Nchini England, sikuwa na furaha tena.

"Nilipata simu kutoka kwa wakala wangu na nilitaka kuja, kwa sababu ilikuwa ni nafasi nzuri kwa upande wangu. Sikufanya hata majadiliano na wakala wangu kuhusu fedha.

"Pengine sikuweza kuzoea haraka soka la Uingereza, hivyo nafikiri mabadiliko yalikuwa muhimu."

Winga huyo alisajiliwa Manchester United akitokea Borussia Dortmund, kabla ya kujiunga na Arsenal katika usajili uliomhusisha Alexis Sanchez kwenda Old Trafford ambaye kwa sasa naye yupo kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akicheza pale Inter Milan kwa mkopo.





# DESCHAMPS KUJADILI PENALTI NA GRIEZMANN

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps amebainisha kwamba atajadiliana na Antoine Griezmann kuhusu penalti, lakini akasema ataendelea kupiga.

Griezmann alikosa penalti wakati Ufaransa ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Andorra kwenye mechi ya kufuzu kwa Euro 2020, juzi Jumanne.

Mshambuliaji huyo wa Barcelona alikuwa na kiwango kizuri kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka jana, akifunga penalti tatu wakati Ufaransa ikilibeba taji hilo.

Na baada ya kuonyesha kiwango hicho, Deschamps alimpa nafasi Griezmann ya kupiga penalti, lakini kocha huyo alibainisha kwamba atafanya mazungumzo na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

"Antoine, anafunga. Wakati akitakiwa kuufunga, anafunga," alisema akiiambia RMC Sport.

"Nitazungumza naye kwa kina, kwa sababu kunaweza kuwa na penalti nyingine Oktoba."

Griezmann amekuwa mchezaji wa kwanza wa Ufaransa kukosa penalti mbili kwa kipindi cha misimu 10. Ufaransa inaongoza msimamo wa kundi H la kufuzu kwa michuano hiyo ikiwa imepata pointi 15 katika mechi sita.

# *Martinez afurahi kupiga 'hat-trick'*

**BUENOS AIRES,** Argentina

LAUTARO Martinez alikuwa "mwenye furaha kubwa" baada ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' wakati Argentina ikiibuka na ushindi kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Mexico, juzi Jumanne.

Martinez alifunga 'hat-trick' yake hiyo ya kwanza mjini Texas wakati kikosi hicho cha kocha, Lionel Scaloni, kikimaliza umwamba wa Mexico kutopoteza mechi chini ya Gerardo Martino na wakakubali kichapo cha mabao 4-0.

Mshambuliaji huyo wa Klabu ya Inter, Martinez, ambaye alionyesha kiwango kizuri kwenye michuano ya kombe la Copa America mapema mwaka huu.

Martinez mwenye umri wa miaka 22, sasa amefikisha mabao tisa aliyoifungia Argentina katika mechi 13 alizoichezea timu hiyo.

"Nina furaha kubwa," aliandika Martinez kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter.

"Kuna kujitoa zaidi wakati unapokuja hapa, sio kila mara unapata muda wa kufunga mabao ukiwa na jezi hii."

Wakati akifunga mabao hayo matatu, Martinez pia aliisaidia Argentina kupata penalti ambayo ilifungwa na Leandro Paredes.

Mchezaji huyo wa zamani wa Klabu ya Racing Club aliwasifia wachezaji wenzake kwa kumwezesha kufunga hat-trick hiyo.

"Ni ngumu kupata nafasi hii. Kwani kuna wachezaji wengi ambao wanaweza kupata nafasi ya kuichezea Argetina," alisema Martinez.

"Nina futaha kubwa na nawafurahia wachezaji wenzangu pamoja na benchi lote la ufundi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AVUNJA REKODI KUFUZU ULAYA WAKIUA

●●● Ni mwenye furaha na ninafurahia mafanikio haya, si kwa sababu nimefunga mabao, ila...

**VILNIUS,** Lithuania

CRISTIANO Ronaldo ameongeza rekodi nyingine katika hazina yake baada ya kuwa mfungaji wa wakati wote kwenye michuano ya kuwania kufuzu Europa 2020.

**Ronaldo, 34, alicheka na nyavu mara nne wakati Ureno ikiichapa Lithuania mabao 5-1 kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 na hivyo kufikisha mabao 25 katika michuano hiyo ya Ulaya.**

Idadi hiyo inamfanya nyota huyo wa Juventus kumpiku Robbie Keane, ambaye alifunga mabao 23 katika kinyang'anyiro hicho cha kuwania kufuzu Europa wakati akiitumikia timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland.

Hata hivyo, Keane alionyesha utani kwa nyota huyo wa Ureno amwachie rekodi hiyo naye, akiandika kwenye Instagram: "Nadhani una kumbukumbu za kutosha @cristiano."

Lakini ndani ya dakika saba, Ronaldo alitupia bao lake la kwanza usiku huo wa kuamkia jana kwa mkwaju wa penalti kabla ya kuongeza mabao mengi matatu na kufanya jumla ya mabao yake yote kimataifa kuwa 93.

Ronaldo pia aliimarisha ufungaji wake wa wakati wote kimataifa Ulaya, akimwacha nguli wa zamani wa soka Ferenc Puskas kwa mabao tisa.

Pia ilikuwa ni 'hat-trick' ya nane kimataifa kwa Ronaldo akiwa na mabingwa hao wa Kombe la Mataifa wa Ulaya.

Ronaldo, 34, akizungumzia mafanikio hayo alisema: "Nimekuwa na wakati mzuri, lakini timu ilifanya vizuri pia," Ronaldo aliwaambia wanahabari.

"Ni mwenye furaha na ninafurahia mafanikio haya, si kwa sababu nimefunga mabao, ila kwa sababu ya kiwango ambacho tumeweza kuonyesha katika miaka ya hivi karibuni.

"Ni juu yangu kuendelea kusaidia timu ya taifa."

Baada ya kutoka sare mfululizo wakati ikianza michuano hiyo, Ureno imeweka rekodi ya ushindi mnono dhidi ya Serbia na Lithuania.

## ZISIKUPITE

### BECKHAM AMFUATA MESSI

DAVID Beckham "anafanya mawasiliano" na mshambuliaji wa Barcelona, Muargentina Lionel Messi, 32, kuhusu kujiunga naye katika klabu yake inayoshiriki Ligi Kuu Marekani (MLS), Inter Miami. ***(Mirror)***

### CHELSEA YAJIPANGA KWA ATAL

CHELSEA itajaribu kumsajili beki wa pembeni wa Nice, Mualgeria Youcef Atal, 23, anayeelezwa kuwa na thamani ya pauni milioni 35, katika dirisha la Januari kama itafanikiwa kuondolewa kifungo cha kusajili. ***(Sun)***

### UNITED MPAMBANIA LUIS

MANCHESTER United inamnyemelea kiungo wa Benfica, Mreno Florentino Luis, 21, ila itakabiliwa na upinzani kutoka Manchester City. ***(A Bola via Sport Witness - in Portuguese)***

### CITY KUMRUDIA SKRINIAR

MANCHESTER City ofa yake haikufanikiwa majira ya joto kwa beki wa Inter Milan, Mslovakia Milan Skriniar, ila itajaribu tena Januari. ***(Tuttosport, via Sport Witness)***

### AMTAJA MESSI ARSENAL

ARSENE Wenger amesema moja ya jambo kubwa zaidi analolijutia akiwa kocha wa Arsenal ni kukosa kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi. ***(beIN Sports)***

### BRUYNE KUMFUATA KOMPANY

KIUNGO wa Ubelgiji Kevin de Bruyne, 28, amemuahidi mchezaji mwenza wa zamani hapo Manchester City, Vincent Kompany kwamba siku moja atakwenda kuichezea klabu yake ya Anderlecht. ***(Sun)***

### AJUTA KUCHEZA EPL

KIUNGO wa Armenia aliyewahi pia kuichezea Manchester United na Arsenal, Henrikh Mkhitaryan, 30, ambaye kwa sasa anaichezea Roma, amesema nyakati zake akicheza Ligi Kuu England kulimfanya "kupoteza mapenzi" na soka. ***(Manchester Evening News)***

### SANE KUWEKEWA KIZUIZI

MANCHESTER City inajaribu kumshawishi winga Leroy Sane, 23, kusaini mkataba mpya kabla ya Bayern Munich kupata fursa mpya ya kutoa ofa kwa Mjerumani huyo. ***(Standard)***

### GAYA AANZA KUWINDWA

CHELSEA itajaribu kumsajili beki wa kushoto wa Valencia na Hispania, Jose Gaya, wakati mkataba wake utakapomalizika majira ya joto yajayo. ***(Soccer Link, via Talk Sport)***

### AMFUNGUKIA WENGER

BEKI wa zamani wa Arsenal na Ujerumani, Per Mertesacker anaamini wachezaji wa klabu hiyo walishindwa kuthibitisha thamani yao kwa Arsene Wenger wakati Mfaransa huyo akiinoa klabu hiyo hapo Emirates. ***(Standard)***

### NICOLATO AMPA SOMO KEAN

KOCHA wa Italia U-21, Paolo Nicolato amemtaka straika wa Everton, Moise Kean, "kujifunza kutokana na makosa" kinda huyo ameachwa katika kikosi cha wakubwa cha Italia kilichopo kwenye majukumu ya kimataifa kwa sasa. ***(Gazzetta Dello Sport, via Sport Witness)***

HABARI MICHEZO

## Nyoni: Moto sasa kwa Sudan Taifa

Na Faustine Feliciane

BEKI wa timu ya Taifa, Taifa Stars, Erasto Nyoni, amesema kwa kasi ile ile sasa wanapaswa kuelekeza nguvu zao kwenye mchezo dhidi ya Sudan wa kuwania kufuzu fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Erasto alikuwa sehemu ya kikosi cha Taifa Stars kilichowatupa nje Kenya kwenye mchezo wa kwanza hatua ya awali ya michuano hiyo na pia akawa sehemu ya kikosi cha Stars kilichoitupa nje Burundi kwenye mchezo wa kuwania kufuzu kushiriki hatua ya makundi kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini Qatar 2022.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nyoni alisema hamasa kubwa iliyokuwapo kuanzia kwa mashabiki waandishi wa habari, viongozi mpaka wao wachezaji ndio imefanikisha matokeo mazuri waliyoyapata kwenye michezo iliyopita.

"Bado tuna kazi ngumu katika mashindano yote tunayoshiriki, mchezo unaofuata ni dhidi ya Sudan, kwa sasa tunapaswa kuelekeza nguvu zetu kwenye mchezo huo na kuunganisha nguvu kama ilivyokuwa katika michezo iliyopita, kikubwa tunataka kufanya vizuri na kufikia malengo yetu na ya kila shabiki na Watanzania kwa ujumla," alisema Nyoni.

## Djodi kamgusa Ndayiragije hapa

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya kukunwa na kiwango anachoendelea kukionyesha akiwa na kikosi cha Azam FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mrundi Etienne Ndayiragije, amependekeza mshambuliaji wake Muivory Coast Richard Djodi, kuongezwa mkataba mpya jambo ambalo uongozi wa klabu hiyo umelitekeleza mara moja kwa kumfunga kwa miaka miwili zaidi.

Djodi, ambaye ameipeleka Azam FC raundi ya kwanza ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kufuatia kutupia mabao mawili wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Fasil Kenema ya Ethiopia hivyo kusonga mbele kwa jumla ya mabao 3-2, alibakiza mwaka mmoja katika mkataba wake wa awali.

Hivyo, sasa ataendelea kukipiga na wakali hao wa Chamazi hadi mwaka 2022 baada ya juzi kumwaga wino rasmi katika mkataba ulioshuhudiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat'.

Ofisa Habari wa Azam FC, Jafari Maganga, jana alisema uongozi wa klabu hiyo umeamua kuingia naye mkataba mpya ndani ya muda mfupi baada ya Djodi aliyejiunga na timu hiyo akitokea Ashanti Gold ya Ghana, kuonyesha kiwango kizuri katika mechi mbalimbali za mashindano hali ambayo imemvutia Ndayiragije, aliyependekeza kurefushwa zaidi kwa mkataba wake.

"Kocha Ndayiragije amevutiwa na uwezo mkubwa unaoonyeshwa na Djodi, hivyo amependekeza aongezwe mkataba mpya mapema jambo ambalo uongozi umelitekeleza mara moja," alisema Maganga.

# ZAHERA AHISI KITU BALINYA, MOLINGA KUKOSA MABAO

Na Mwandishi Wetu

LICHA ya kuanza kuonyesha cheche zake za kucheka na nyavu, Kocha Mkuu wa Yanga, Mkongomani Mwinyi Zahera amehoji kuna nini kwa washambuliaji wake wawili, raia mwenza David Molinga aliyefunga mabao mawili wakati wakishinda 3-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Toto Africans juzi pamoja na Mganda Juma Balinya.

Molinga ambaye mashabiki wanaamini Yanga imeingia 'chaka' kutokana na kushindwa kuonyesha uwezo wa kufunga kwenye mechi za kirafiki anazopewa nafasi, katika mechi hiyo ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza alifunga mabao mawili kabla ya Zahera kumtoa, lakini pia Balinya naye akiandamwa na ukame wa mabao tangu ajiunge na timu hiyo msimu huu akitokea Polisi FC ya Uganda.

**Akizungumza baada ya mechi hiyo juzi, Zahera alionyesha kushangazwa na washambuliaji hao akiwataka wanaowabeza wajiulize kuna nini nchini kwa kuwa walipotoka walikuwa ni miongoni mwa wafungaji bora.**

"Sijui kuna nini hapa, mchezaji kama huyu Falcao (David Molinga) kule Congo alikuwa namba mbili kwa ufungaji akiwa na mabao 15 baada ya Jackson (Muleka) wa TP Mazembe na huyu Juma (Balinya) aliongoza Uganda kwa kufunga mabao 21, sasa jiulize kuna nini hapa," Zahera alihoji.

Hata hivyo, Zahera alisema ni suala la muda tu kabla ya washambuliaji wake hao kuanza kutupia huku akiwatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kuhusu kufanya vizuri kwenye mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco Jumamosi.

Zahera bado anaamini uwezo wa washambuliaji wake, huku akijipanga kutatua tatizo hilo sugu la kushindwa kutumia vema nafasi wanazotengenezewa.

Katika ushindi huo wa juzi dhidi ya Toto Africans, mbali na Molinga aliyetupia mawili dakika ya 37 na 41, bao la tatu lilifungwa na kiungo mpya, Mzanzibari Abdulaziz 'Bui' Makame dakika ya 51.

Mbali na Molinga na Balinya, safu ya ushambuliaji ya Yanga inaundwa pia na Patrick Sibomana, Sadney Urikhob na Maybin Kalengo.



Straika wa Yanga, David Molinga, akifanya vitu vyake dimbani kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Toto Africans iliyopigwa Uwanja wa Nyamagana juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Samatta kurejea uwanjani mapema*

Na Somoe Ng'itu

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars na mshambuliaji wa Klabu ya KRC Genk inayoshiriki Ligi Kuu Ubelgiji, Mbwana Samatta, atarejea uwanjani hivi karibuni baada ya majibu ya vipimo alivyofanyiwa kuonyesha, mguu wake ulipata mstuko na si jeraha kubwa, imefahamika.

Samatta alipata maumivu wakati akiitumikia Taifa Stars dhidi ya Burundi katika mechi ya kuwania tiketi ya kutinga hatua za makundi kusaka kufuzu fainali zijazo za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, iliyochezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Jumapili iliyopita kwa wenyeji kusonga mbele katika michuano hiyo.

Hata hivyo, Samatta hakuwa tayari kufanyiwa mabadiliko mapema katika mechi hiyo iliyokuwa ya "kufa ama kupona", mpaka pale alipoona hali imekuwa mbaya na hivyo kuliruhusu benchi la ufundi kumtoa nje.

Akizungumza na gazeti hili jana, Samatta, alisema anamshukuru Mungu maumivu aliyopata hayakuwa makubwa na sasa atapata matibabu na kurejea uwanjani ndani ya siku chache.

Mshambuliaji huyo alisema kwamba baada ya kupona, anaamini atarejea uwanjani na kuendelea kupambana ili kuisaidia klabu yake pamoja na taifa lake la Tanzania.

"Asante Mungu, nashukuru baada ya kufanyiwa uchunguzi, daktari amesema sehemu iliyopata majeraha imetokana na mshtuko na si kuvunjika, yaani amesema kama ingekuwa imeumia, muda wa chini ningekaa nje ya uwanja kwa muda wa miezi sita, lakini sasa nitakaa muda mchache na kurejea uwanjani," alisema Samatta.

Mbali na kupambana kwa ajili ya Genk, Samatta pia bado anajiweka sokoni kupata timu ya kuitumikia barani Ulaya na hasa akiitaka Ligi Kuu England, wakati huu akiwa amebakisha miaka miwili katika mkataba wake na klabu hiyo ya Ubelgiji.


Katika mchezo huo, Stars iliwaondoa Burundi kwa penalti 3-0, baada ya matokeo ya jumla kuwa sare ya mabao 2-2 kufuatia sare ya bao 1-1 nyumbani na ugenini.

Michezo
Alhamisi Septemba 12, 2019
Nipashe



Deschamps kujadili penalti na Griezmann UKURASA 29

NATUPIA...



Mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, akifanya yake uwanjani kwenye mechi ya kuwania kufuzu fainali za Europa 2020 dhidi ya Lithuania na straika huyo, anayeichezea Juventus ya Italia kufunga mabao manne wakati wakishinda 5-1. **HABARI UK.30**

# Kagere, Stars njia moja Qatar

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Klabu ya Simba, Meddie Kagere (pichani), ameiongoza timu yake ya Taifa ya Rwanda kuungana na Taifa Stars kuwa miongoni mwa timu zilizofuzu hatua ya makundi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar 2022 baada ya kuifungia mabao mawili wakati ikiichapa Shelisheli 7-0 juzi.



Matokeo hayo yanaifanya Rwanda kuitoa Shelisheli kwa jumla ya mabao 10-0 baada ya Alhamisi iliyopita kwenye mechi ya awali kushinda 3-0 ugenini huku Kagere akitupia moja katika ushindi huo.

Katika mchezo wa juzi uliopigwa Uwanja wa Nyamirambo mjini Kigali, mbali na Kagere aliyeziona nyavu dakika ya 27 na 51, mabao mengine yalifungwa na Jacques Tuyisenge dakika ya 28 na 34, Yanick Mukunzi dakika ya 57 na Muhadjir Hakizimana dakika ya 79.

Hakizimana na Mukunzi pia walikuwa miongoni mwa wafungaji waliocheka na nyavu katika mechi ya awali ugenini, hivyo sasa Rwanda inayonolewa na kocha mzawa Vincent Mashami inaungana na Taifa Stars iliyoitoa Burundi kwa mikwaju ya penalti 3-0 baada ya matokeo ya jumla kuwa 2-2, kusubiri kujua makundi watakayoangukia kuwania kufuzu fainali hizo.

Kagere ambaye juzi alitangazwa Mchezaji Bora wa mwezi Agosti na Bodi ya Ligi Kuu Bara, ameuanza msimu huu kwa mafanikio makubwa kwani katika mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Bara pia alitupia mabao mawili na kutoa pasi ya mwisho wakati wakishinda 3-1 dhidi ya JKT Tanzania.

# Yanga: Tutaivaa Zesco kivingine

**Na Faustine Feliciane**

## ●●● Zahera awatoa hofu mashabiki, asema tayari mkakati wa kuibuka na ushindi umekamilika na kwamba...

BAADA ya kushuhudia timu yake ikihitimisha kambi yake jijini Mwanza kwa kuvuna jumla ya mabao 4-1 kufuatia kuibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Toto Africans ikiwa ni baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Pamba, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera amewataka mashabiki wa timu hiyo kutuliza presha kwa kuwa watavaa Zesco Jumamosi kivingine kabisa.

**Akizungumza baada ya kuichapa Toto Africans juzi, Zahera alisema mbinu atakazotumia katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa dhidi ya Zesco ya Zambia ni tofauti kabisa na kwamba ana uhakika wa kikosi chake kuibuka na ushindi.**

Alisema matokeo aliyoyapata jijini Mwanza hayamtii hofu na kwamba kila mechi kwake ina mbinu na ufundi tofauti katika kukabiliana nayo.

"Siangalii matokeo haya kwenye mechi hizi za kirafiki, kwani hata wachezaji watakaocheza mechi dhidi ya Zesco ni tofauti, kikubwa kwangu naangalia namna wachezaji wanavyocheza nakutazama nani nimtumie wapi na kwa muda gani, haya yote ni maandalizi kuelekea mchezo wetu wa Ligi ya Mabingwa," alisema Zahera.

Alisema namna walivyocheza kwenye michezo hiyo ya kirafiki sivyo watakavyocheza kwenye mchezo wa Jumamosi dhidi ya Zesco.

"Naifahamu Zesco, najua ubora wao na udhaifu wao..., nimeshaandaa namna ya kuwakabili, mashabiki wafahamu tunavyocheza sasa kwenye michezo ya kirafiki, sivyo tutakavyocheza na Zesco, tutaingia uwanjani kivingine," alisema.

Aidha, amewataka mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwapa hamasa wachezaji wao ili kuhakikisha wanaibuka na ushindi siku hiyo.

Katika ushindi huo wa juzi dhidi ya Toto Africans, mabao yalifungwa na David Molinga aliyetupia mawili dakika ya 37 na 41, huku la tatu lilifungwa na kiungo mpya, Mzanzibari Abdulaziz 'Bui' Makame dakika ya 51.

Na katika mechi dhidi ya Pamba bao la Yanga lilifungwa na Molinga ambaye hata hivyo hatacheza mechi dhidi ya Zesco kutokana na kuendelea kusubiri kibali chake cha kimataifa kutoka Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf).

Ushindi kwenye mchezo huo wa kwanza utawaweka Yanga katika nafasi nzuri kuelekea mechi ya marudiano wiki mbili zijazo nchini Zambia.

Hata hivyo, endapo Yanga itashindwa kupata matokeo ya jumla katika mechi hizo mbili nyumbani na ugenini, itaangukia kucheza mechi ya mchujo na timu zitakazovuka raundi ya kwanza kutoka Kombe la Shirikisho Afrika ili kuwania nafasi ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoshika nafasi ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >